HATUA INE ILI KU UFIKIA

UAMUSHO

Kime andikwa
na
DALEN GARRIS

Revival Fire Ministries

Kime tafsiriwa
toka Kiingereza na
M. Igunzi NDAHASHUBA Michel
bamwiji@yahoo.fr (tel. +243 990 660 793)

HATUA INE ILI KU UFIKIA
UAMUSHO

Matayarisho ya Mwili wa Kristo ili kuingia kwenye
Uamusho mkubwa zaidi
kuliko uamusho wowote ulio wahi kutokea

Kimepigwa chapa kwa lugha ya Kiingereza katika Jumuiya ya Marekani - 2009

Pale pasipo tajwa tafsiri nyingine, Maandishi yote ya Biblia yamerejelewa toka Biblia ya Tafsiri ya King James (Mfalme) Yakobo.

Dalen Garris

Revival Fire Ministries
P.O. Box 822 Waxahachie, Tx 75168
(972) 938-8502

tafsiri toka Kiingereza imefanywa na
M. Igunzi NDAHASHUBA Michel
bamwiji@yahoo.fr

@Haki ya ku nakili, Dalen Garris
Haki zote zime hifadhiwa.

Hakuna sehemu hata moja ya kitabu hiki ambayo inaweza ku chapishwa upya, ao ku chungwa katika muundo Fulani ili kuja ku rudiliwa uchapishwaji upya ao ku tumwa toka mtambo fulani hadi mtambo mwengine kwa njia ya umeme, ao kwa njia ya ki ufundi wa mikono, wa ku pigwa chapwa ao ku rekodiwa,
Bila maandiko ya ruhusa toka mwandishi wa hiki kitabu.

ISBN 978-1-625-17179-5

Yaliyomo

Ingilio ……..……..12

Mzunguuko kati ya Ku iacha iamni ya kweli na Uamusho……..……..……..**12**

I.Hatua ya 1 :

I :Utambuzi ……. 20

a. Changamoto (Mutiani) …….. 20
b. Utambuzi……...20
c. Changamoto (mutiani)…..……..21
b. Agizo lake la mwisho…… .. 24
c. Andiko la Patano la ndoa…….. 26
d. Miujiza……31
e. Mashamba yana haribiwa……34
g. Ukarimu, Jambo kubwa kati ya haya yote…….…... 39

II. Hatua ya 2:
Kiu kikubwa cha ku upokea Uamusho……43

a. Kukataa Mabadiliko……...45
b. Uzaifu na kuto kujali…….……46

III. Hatua ya 3:
Kuipokea toba……51

a. Kuwaleta watu kwa Yesu……..51
b. Mwaliko kwa Utakaso wa mtu binafsi….68

c. Toba ya kundi……..73
d. Danieli……..74
e. Nehemia……..77
f. Eliya……79

IV. Hatua 4:
Kupiga Vita kwa njia ya maombi…….…..85

V. JINSI YA KU UFANYA MOTO UWAKE.…….92

a. Ile Arusi ya Kana……..96
b. Moto mulimani……..98
c. Isaya 58 – Ufunguo ili kufikia
Uamusho……100

VI. Hatua za ki vitendo……..107

VII. Jibu……..121

Kwa ku malizia……..129

Dibaji

Nina andika ujumbe huu wa Hatua Ine ili Kufikia Uamusho sababu nina amini kuwa ndiyo tumaini lililo bora zaidi katika ku tafuta suluhisho la shida nzito za kiroho ambazo dunia yetu ina pambana nazo. Sawa sawa na Wakristo wengine wengi ambao wame kuwa waki chunguza unabi wa Biblia jinsi unavyo endelea ku timilika na jinsi vyombo vya ku pasha habari vinavyo yaonyesha, mimi name nina amini kuwa tuna ishi katika siku za mwisho. Wakati ambapo wengi wana amini kuwa hatupaswi ku ogopa chochote sababu wao wana tazamia kuwa wata nyakuliwa watoke katika shida ambazo ziko njiani ku u kumba ulimwengu wote mzima, mimi naamini kuwa Kanisa; siyo tu kwamba lita kabiliana na shida zenyewe, bali pia lita pitia katika nyakati zenyewe mpaka kufikia ule wakati ambapo Kristo atapo rudi.

Kuna wakati mmoja ambapo Mwandishi maarufu wa Uingereza aliye julikana kwa jina la Shakespeare ali andika yafuatayo: "dunia yote hii nzima ni uwanja wa mashindano". Maneno hii ni kweli kabisa kuliko jinsi hata yeye aliye yasema alivyo kuwa aki wazia maneno haya alipo yasema. Siasa zote, bihashara, kazi na burudani zote za maishani si kingine ila tu mitiyani tunayo ipitia maishani na ambayo matukio yake ndiyo yata amua kule tutakapo elekea kwa maisha yetu ya milele. Katika bonde hili la maisha tunamo pitia na ambako ni kwepesi sana ku sahau hali ya mapambano ambamo tulimo, Kanisa linatakiwa kuwa ki elelezo na taa ionyeshayo njia ielekeayo Mbinguni. Ila sasa, wakati uki fika ambapo Kanisa lina poteza uvutio na nuru yake kufikia kiasi cha ku fifia, tuna jikuta kwamba tume jifanya marafiki wa vitu vingine-vingine ambavyo vina tia tu mapambo kwenye maisha yetu wenyewe

ya inje. Wakati huo tuta kuta kwamba macho yetu yana acha ku elekea kule tunako enda, na yana geukia ku elekea hapa tulipo, na mambo ya wakati huu wa sasa ya kuvutia-vutia macho na nia ya mwili ambayo ina onekana katika ulimwengu unao tuzunguuka yana chukuwa nafasi ya mbele pahali pa kuona jinsi haraka sana hukumu ya milele inavyo karibia. Halafu kwepesi tunapotea njia, tuna sahau kuwa uwanja wa mashindano ambamo tulipo ni mutiani tu, na tuna acha ku shikilia ile iliyo ya muhimu zaidi. Halafu maisha yana geuka matata yakijaa miiba na mitego, amabayo hutu kokota kwa mvutano ambao huongezeka na ku ongezeka uki tu kokotea mbali na mbali tena zaidi toka njia ya wokovu wa kweli.

Uamusho ndilo jibu moja tu. Bila kuwa na nuru yenye nguvu na inayo angaza ili kutu elekeza upande wa kweli wa Uhai, tuta jikwaa tu katika giza. Ni Uamusho tu wa Roho Mtakatifu ndio unao weza ku washa tena hizo taa na ku pelekea mienge (torches) ya nyumba zetu i angaziye watu waione njia inayo elekeza kwenye Wokovu.

Neno Uamusho linapewa maana isiyo faa mara kwa mara kutokaa na kwamba lina fanana ku eleza hali ya ku urudishia mwili ulio kufa uhai. Hata hivyo, katika historia, madhihirisho makubwa ya utendaji wa nguvu za Mungu yame wahi ku tendeka kama uasi zidi ya miundo ya kidini iliyo simamishwa na ambayo ime kumbwa na ubaridi na ku geuka ya mtindo wa kiulimwengu. Wakati ambapo mwili umekufa, ku upulizia hauwezi ku urudisha kuwa hai tena. Kinacho hitajika ni uhai mpya ku mea upya ndani ya mwili mwengine mpya wala sio ufufuko wa muundo wa zamani ambao tayari ume kufa.

Kungali bado kuta fika kipindi kimoja cha uamusho. Yesu Kiristo yu karibu sana ku rudi, ila mbele ya Yeye ku rudi, ime andikwa kwamba kuta tokea kipindi kingine kimoja na cha mwisho cha uamusho mkubwa – uamusho mkubwa sana kuliko vipindi vyote vya uamusho vilivyo wahi ku tokea. Kitabu hiki kime andikwa ni ku husu huo uamusho mkubwa na wa mwisho.

Kila palipo moto sherti kuwe na mshale wa moto ulio uanzisha. Maombi niliyo nayo ni kwamba kitabu hiki kidogo kita kuwa mushale wa moto ili ku saidia ku ziwasha ndimi za moto wa uamusho utakao waka ulimwenguni mzima.

Ingilio

Muzunguuko kati ya Kuikana Imani ya Kweli na Uamusho

Tunapo chunguza historia tokea zama za nyakati za Yoshua, tunakuta kuwa Ukengeufu (Kuikana Imani ya Kweli) na Uamusho hufuatana Jambo moja liki futana na lingine. Kila nafasi ambapo pame wahi kuzihirika Uweza mkuu wa utendaji wa Mungu, Kanisa hupewa nguvu na ku geuzwa kuwa sehemu yenye uvutano na inayo vutia sana maisha ya washirika wake. Furaha na ku changamuka ni dalili za nyakati sawa hizo. Kufanikiwa na maisha Ku inuwa, sio tu Kanisa peke yake, ila pia jamii yote linalo li zunguuka. Na huo ni wakati mzuri sana ajabu.

Ingawavyo, baada ya mda mfupi, nuru huanza ku fifia na baraka zile za ajabu za kule kuweza ku tembea kwa ushirika wa karibu katika Roho huanza ku chukuliwa kama ni

jambo ambalo tayari limesha kuwa mateka ya wale ambao wame zionja baraka zenyewe na halafu wao hu anza ku ji tenga na ile furaha itokanayo na zile baraka na mara moja ku anza kuzi badilisha kwa ku vutwa na udanganyifu wa mambo ya ki fahari za dunia. Hili linapo tokea, halafu polepole, malengo yetu yanabadilika toka mtazamo wa mambo ya umilele hadi kuelekea malengo ya mtazamo wa mambo ya mda, mambo ya ku pita ; toka mambo ya nia ya nafsi zetu za ndani kuelekea kunako tamaa za miili yetu ; toka ahadi za Mungu kuhusu mambo yasiyo onekana na macho ya mwili hadi kuelekea yale mambo tunayo yaona na ambayo ni ya wakati wa sasa. Wokovu na dini vina geuka kuwa mateka ya neema ya urahisi-rahisi na isiyo na bei ghali – aina hiyo ya neema ambayo haiji husishi na aina gani ya maisha tunayo yaishi na ambayo hai ombi mengi ku ji tahidi kufikia utakatifu. Njia iliyo pana ina onekana kwa wakati ule kuwa ndiyo inayo vutia nayo ina anza ku onekana ndiyo iliyo rahisi ku ipitia. Na pamoja na hayo, twaanza ku jiuliza, kwa nini tu pitiye kwenye mateso wakati ambapo Yesu ali pata mateso msalabani kwa ajili yetu ? Dini ina geuka kuwa iliyo pangwa-pangwa kabisa, yenye taratibu zilizo chorwa mtindo wa ki dunia, iliyo weka nguzo zake ndani ya jamii ambamo hai oni haja ya ku ionyesha mambo yanayo hitaji ya nyooshwe. Yale mateso ambayo hapo mbeleni yali pelekea kuwaka kwa moto wa uamusho ambao uli anzisha makanisa yetu sasa yametoweka na hayatambulikane tena kama kitu cha mhimu. Ni kama tayari tume fika, na tayari tume tosheka.

Wakati ambapo haku hitajiki garama ya ku toa ili ku upata, Ukristo wa kweli hauonekane kuwa kitu cha samani, na halafu, sawa-sawa na jinsi ilivyo kwa vitu vyote visivyo na bei gali kuvipata, yaanza kuonekana kuwa ni rahisi sana ku

uweka Ukristo pembeni.

Jinsi ambavyo moto wa uamusho unavyo zimika na ku geuka vi inga vya moto vinavyo anza kuwa majivu tu, bado Kanisa lina zidi ku linda umbo la nje na Mipangilio, ila tayari lina upoteza moyo wake. Uamusho ndio pumzi itokayo kwenye Moyo wa Mungu, na kuvuta walio potea kwa Yesu ndio pumzi ya moyo wa uamusho. Yesu hakufa msalabani ili tuweze kuwa na nyumba nzuri ya jengo la kanisa na maisha ya mafanikio, ila alikufa ili ku waokoa walio potea. Kila tunapo sahau ku shugulikia jambo hili, tuna kosa kujuwa maana halisi ya Msalaba.

Wakati tunapo jikuta kwamba tume furahia sana na kuvutwa kabisa na uzuri ule ambao tuna uhisi tokana na mububujiko wa Roho Mtakatifu kiasi cha ku sahau ku ililia mioyo ya wale ambao bado hawaja upokea wokovu, ni kama tuna ziba murija ambamo uli tiririka ule mububujiko na halafu tuna jikuta tuna poteza kila kitu na kubaki na kile tunacho endelea ku ki ita eti « kanisa ». Mara nyingi mno, mambo yana endelea ku pungua na ku pungua zaidi na zaidi, bila sisi ku tambua, hadi pale tunapo poteza ule mububujiko na kufikia kiasi cha toni ndogo tu, na halafu hapo tunajikuta tuna anza ku rizika na mipango ya ki binadamu pahali pa upako. Halafu, polelepole kinara chetu cha taa kina ondolewa na hatua kwa hatua tuna anza ku zoeya hali ya ku enenda katika giza, hadi pale tunapo fikia kiasi cha kutokuweza ku tambua kuwa sasa tuna anza ku shindwa ku uiona Kweli.

Kila wakati ambapo mambo yanapo fikia kiasi hiki, Mungu huwatuma nabii wake ili watualike ku tubu. Kazi ya nabii siyo kuja ku piga ramli ili ku tu eleza kuhusu siku zetu

za usoni –hilo ni jambo tuwezalo kuli soma kila siku katika magazeti kwenye ukurasa wa ku angalia bahati na sibu zinazo tuhusu- ila kazi yake nabii ni ku waalika watu wa Mungu ku tubu. Nayo ni kazi ambayo akuna hata mtu mmoja anaye ipenda. Haipendwi na yule anaye itwa awe nabii na pia haipendwi na wale ambao yeye nabii ame itwa ili aende ku watolea unabii. Na kutokana na hali hii, mara nyingi sana, wanadamu hawa wajali manabii, ao huwa tupilia mbali ao tena huwa tesa na ku wauwa. Ujumbe wao kamwe haukubaliani na maoni ya watu wala hau changamukiwi na watu, bali unakuwa ujumbe unao tolewa ili u kwaruze kwa sababu una tumwa uipindue misingi ya matendo mafu.

Moja kati ya alama ya ukengeufu wa imani (alama ya ku jitenga na Imani ya kweli) ni ku ongezeka sana kwa manabii wanao tangaza amani na mafanikio. Wana ongezeka, kama magugu inayo mea toka udongo uliyo potoka nao wana pata mizizi katika hiyo hali ya kanisa kuingiliwa na mambo ya kiulimwengu. Manabii wa uongo hawa tualiki ku geuza nia zetu; wao hutu alika tu pumuzike. Kamwe katika unabii wao hakuna ujumbe unao wa weka watu mbele ya changamoto (mitiani), ila tu ahadi za amani na mafanikio. Hawa tualike kuwa na woga wa Mungu, ila hutu zamisha hasa ndani ya upendo wa Mungu. Shida ni kwamba maana ambayo wao hu upatiya upendo wa Mungu ni kana kwamba ni jinsi ya ku ji hisi joto, ku punga hewa – « uhusiano » wa raha pamoja na Mungu ambaye ni « Baba » yetu. Ingawavyo, Neno la Mungu lina fasiria upendo wa Mungu kama ni kuzichunga amri Zake, ambazo –kama isemavyo Mizali 16 :6- kwa njia ya hizo tuna wezeshwa kuishi katika woga wa Mungu. Ila wao, sawa-sawa na wapiga minyuzi inayo vutia ndege, huzi paza sauti ambazo miili yetu inazo zi furahia kuzi sikia, nao hutu

ondoa kwenye mstari kwa njia ya maono yaliyo tiwa chumvi pahali pa matunda ya toba.

Ingawa kama ni mara haba sana ndiyo ma nabii wa kweli hukubaliwa na watu katika wakati wao, mbegu wanayo ipanda huipata ardhi yenye rotuba katika kizazi kinacho fuata kizazi chao. Sawa-sawa na alivyo fanya Gideoni, kizazi kile kipya kita ji sikia kwamba muundo wa dini uliopo sasa haulete majibu yanayo ihitaji mioyo yao, na halafu kuanza ku tafuta kitu kinacho zidi u kawaida ambao baba zao wamekuwa waki watolea. Nabii Yoeli ana eleza hali hii kama hali ya kondoo wa mafugo wanao lia ili kupata majani ya malisho na huku waki yakosa. Katika jitihada yao ya ku utafuta Ukweli, wata kutana na maneno ya wale manabii ambao baba zao wame watupilia mbali. Maneno haya yana ji zihirisha kuwa ya kweli kwa nafsi zao na ku anza ku mea na ku komaa mioyoni mwao ili ku watia bidii ya kuji penyeza juu katika ku tazamia ku fikia mumiminiko mpya wa ujazo wa Mungu.

Gideoni ali ipepeta ngano yake kwa siri ndani ya shinikizo (kinu), na ndivyo hufanya hawa watafuta-ukweli. Huipepeta ngano ya Neno la Mungu katika shinikizo (kinu) cha maombi kwa ajili ya ku i tafuta kweli ya Neno la Mungu mbali na liturjia zilizo shimikwa ndani ya muundo wa kanisa ambalo limesha geukia kuto ku stahili kiasi cha ku ikana imani ya kweli.

Ndivyo inavyo tukia kila wakati. Je hali hii ina tukia sababu ndio mpangilio anao ufanya Mungu, au je ni dalili ya uzaifu wa mwanadamu mwenye mwili ? Mimi binafsi sina jibu la kutoa kwa swali hili, bali kile ni juacho ni kwamba, kama

na jinsi Yesu yeye mwenyewe alivyo tokea wakati ambapo udongo ulikuwa ni mkavu na ndivyo hivyo vipindi vya mavuno makubwa hutukia katika wakati wa ukame wa ki roho.

Na hiyo kabisa ndiyo hali ya wakati tunao uishi ndani yake sasa. Tupo tayari kwa ajili ya mvua itakayo kutupeleka kwenye wakati wa mavuno, ila kwa kipindi hiki mububujiko wa Roho Mtakatifu wa Mungu uta zidia kabisa vipindi vingine vyote vilivyo wahi kutangulia mbele. Wakati tunapo ondoka toka ile njaa ya kiroho aliyo itabiri Yoeli kwamba ita tokea mbele tu ya kuja kwa pili kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ni wakati wa kuanza kwa ule uamusho ulio mkubwa zaidi kuliko vipindi vyote vya uamusho vilivyo wahi ku tokea.

Bali kamwe hakuja wahi kuwepo na uamusho ambao hauna gharama yake. Ujumbe wa kitabu hiki kidogo una husu ile gharama inayo hitajika ili uamusho ku tokea.

Kanuni za Uamusho

Kuna kanuni ine tunazo hitaji kuzi elewa mbele ya sisi ku ufikia Uamusho.

Kanuni ya kwanza yaku elewa ni kujuwa kwamba Uamusho hauji kwa ajili ya kuleta hali yaku jisikia vizuri, hali ya kuwa na ibada za kanisa zenye mchangamko, au kuzipokea Baraka za ajabu kabisa. Uamusho huja kwanza, hasa na siku zote – ni kwa ajili yakuzitafuta nafsi zilizo poteya. Kimusingi ni kwa ajili ya shabaa hii ndiyo sababu Mungu hu utuma uamusho – ili kwamba Kanisa liweze ku simama na ku eneza Nuru ya Wokovu iwa angazie ma milioni ya nafsi za watu wanao elekea moja-kwa-moja hadi Jehanum. Nia ya Mungu si kwamba hata nafsi moja iungue

motoni Jehanum, bali Yeye hu utumia Mwili wake ili kuzi pelekea hizi nafsi ujumbe wa tumaini. Yesu amesema kuwa, atakapo inuliwa, Ata wavuta wote kwake yeye, na hiyo ndiyo sababu ya Uamusho.

Kanuni ya pili ni kwamba Ujumbe wa Injili ya Yesu Kristo si kwa ajili yako wewe. Ni kwa ajili ya wengine, wengine na wengine. Una takiwa ku geuka na kuweka mtazamo wako ku elekea pande zote. Kauli ni kwamba, au mtazamo wako una uelekeza kwa wengine na kama sivyo, mutazamo wako una uelekeza kwako wewe mwenyewe. Ikiwa bado hauja shikilia kwenye huu ukweli, basi wewe bado hauja uelewa Msalaba. Yesu alikufa ili kuwa okoa walio potea, Naye ana tualika kumu fuata katika ku uitikia mwito huo. Naye Mungu hawezi ku uleta uamusho, mpaka pale unapo fikia kiasi cha kuondoa mtazamo wako na kuacha kuji tazama wewe mwenyewe.

Kanuni ya tatu inayo bidi ku eleweka ni kwamba kuna garama inayo takiwa ku lipwa ili ku ufikia uamusho. Hakuna kitu kinacho toka kwa Mungu bila gharama. Na gharama inayo hitajika ili uamusho utokeye ni kubwa – na kwa kweli ni kubwa sana kiasi kwamba hiyo ndiyo sababu ni mara haba sana kuona vipindi vya uamusho wa kweli uletwao na Roho Mtakatifu viki tokea. Huwezi ku tazamia kuketi umetulia kitako ndani ya kanisa na halafu ungojee kwamba Mungu ata shusha uamusho juu ya mapaja yako – kamwe haiwezi ku tendeka. Kwa kiwango fulani, una takiwa ku simama na ku tenda jambo fulani... na halafu usipo tenda lolote, na hakuna lolote liwezalo ku tokea. Na, uki endelea ku tenda yale ambayo siku zote una yatenda, halafu uta kuwa na vile-vile vitu ambavyo siku zote uko navyo; ila ukitaka kitu kipya,

unatakiwa kutenda kitu fulani kipya. Kuna gharama ya kulipa.

Kuelewa kanuni hizi ni jambo la muhimu sana ikiwa tuta taka kuona utendaji wa Mungu katikati yetu.

I. Hatua 1 : Utambuzi

"Nika toka nje usiku, kwa njia ya lango la bondeni, nika shika njia iendayo kisima cha joka na lango la jaa ; nika zitazama kuta za Yerusalemu, zilizo kuwa zime bomoka ; na malango yake yameteketezwa kwa moto. Kisha nika endelea mpaka lango la chemchemi, na ziwa la mfalme; lakini hapakuwa na nafasi ya kupita kwa yule mnyama aliyekuwa chini yangu." Nehemia 2: 13-15.

Kwa wakati wowote, hatua ya kwanza ili kufanywa tena upya ni kutambua kuwa hatupo tena katika nafasi ya Baraka ambapo tuli kuwa mbeleni. Kuta zetu zime bomolewa, hekalu limebomolewa, na makanisa yetu yamepelekwa Babeli ambako bado tuna jaribu ku shikilia mikutano yetu ya kidini ili kujaribu kuji fariji wenyewe kuwa mpaka sasa mambo ni sambamba kati yetu na Mungu.

Nehemia ali kabiliana na kuta ambazo zilikuwa zime vunjwa hadi chini, ila mbele hata yaku ianza kazi yaku jenga upya, ili mu bidi akiri dhambi za watu wake mbele za Mwenyezi Mungu. Kufunga pamoja na dua za maombi yasiyo koma ya mchana na usiku vili bidi vitangulie kazi yoyote ile ya ujenzi mpya. Pasipo ile hali ya kwanza, ku tanguliza kule kukiri na kutubu, Yeremia bado angeli baki kule kule Babeli. Na ndivyo ilivyo pia, ikiwa kanisa halita weza ku kiri kujitenga kwake na Imani ya kweli na ku tubu, Mungu

hawezi kuli huwisha (kuli leteya pumzi nyipya) sababu kama sivyo lita rudia tena moja-kwa-moja katika hali hiyo iliyo lipelekeya kwenye kujitenga na imani ya kweli.

Ni mara haba sana kwa watu ambao wameingia pole-pole kwenye hatua ya ku ikana Imani ya kweli kuweza ku ona kuwa hali hii ya kuikana Imani ya kweli imeanza kuji penyeza ndani ya kanisa lao na wakubali kuwa kanisa lao lina elekea kufa. Utaratibu ulio zoewa wa kuzifuata desturi za kidini zilizo wekwa na baba zetu hufunika kisiri matangukano yanayo tokana na ukiwa wetu wa sasa. Hatuwezi ku yaona sababu hatuko makini, na tena ina sumbua sana ku yafikiria. Ni rahisi zaidi ku sikiliza wapiga firimbi na tarumbeta wanao tu eleza kuwa mpaka sasa Mungu ana tupenda bila kujali lolote lile; kuliko ku pambana na kweli isiyo na uvutio inayo tueleza kuwa tayari tume uacha uwepo wa Mungu na kwamba sasa tuna kabiliana na hukumu.

Hatu oni hali hii sababu hatutaki kuiona.

Changamoto (mutiani)

Nimekuwa niki hubiri katika makanisa zaidi ya kumi katika inchi za ngambo, na karibu katika yote hayo, wana tazamia Muinjilisti mkubwa mzungu atokaye Marekani ata wabariki na neno la ku tia moyo. Pahali ya hiyo,neno la kwanza ninalo waeleza ni kwamba mimi sije hapo ili waweze ku barikiwa, ili waweze kupata pesa, waweze kupata mume ao ili mimea ya mashamba yao izae zaidi – mimi nina fika ili kuwa onyesha ukweli.

Mtiani wangu wa kwanza ni ku wauliza ikiwa wana amini kwamba wana kanisa nzuri. Ikiwa wana tosheka na kanisa lao pamoja na mwenendo wao wa kikristo, halafu

hakuna sababu tena ya mimi kutaka ku endelea mbele. Hebu nilikute kundi la kanisa ambalo lina njaa ya kupata kitu fulani cha zaidi katika kutembea kwao na Mungu kuliko kuendelea tu kuwa na ibada za kanisa. Mimi si mtafute mtu yule ambaye hayupo katika ku tafuta – nina watafuta tu wale ambao wapo katika ku tafuta.

Ni nafsi ngapi zime mpokea Yesu Kristo juma lililo pita ? Na halafu, mwezi ulio pita ? Vema, halafu mwaka ulio pita ? Hii ndio chombo cha kipimo ili ku upima Ukristo. Haijalishi kanisa lenu lime jengwa vizuri kiasi gani, au kiasi gani mchungaji wenu ni wa ajabu kiasi gani, au kiasi gani munapendana nyinyi kwa nyinyi – je muna zivuta nafsi za walio potea na ku zileta kwa Yesu? Ndio au hapana.

Kila juma una keti kwenye kile-kile kiti na una zunguukwa na zile-zile sura. Muna elezeana nyiyi kwa nyinyi mambo yale-yale mazuri mazuri muliyo ya zungumuzia juma lililo pita. Muna elezeana kuwa muna taka uamusho, ila mupo katika ku ngoja kwamba ita shuka tu mara moja toka mawinguni hadi kwenye mapaja yenu pale munapo keti hapo kwenye kiti cha kanisa kama walio zidiwa na unene na bila ku tenda lolote. Kama na vile isemavyo mizali ile ya zamani, uki endelea ku tenda yale-yale mambo unayo yatenda, siku zote uta endelea kuwa na vile-vile vitu ulivyo navyo; lakini uki penda kuwa ni kitu tofauti, una takiwa ku tenda kitu fulani cha tofauti. Na usipo fanya chochote, hakuna chochote kitakacho tokea.

Kuna wakati ambapo ina bidi ku tambua kuwa hakuna kitu chochote kipya kinacho tokea kanisani mwenu. Roho wa Mungu hayuko tena, na nafsi za walio potea hazipo ziki

upokea wokovu – na hai fanani kuwa kutakuwepo sasa na mvutano mpya wa wenye dhambi ambao wata chukuwa hatua na ku elekea kwenye madhabao yenu hivi karibuni. Na kwa nini wafanye hivyo? Muna nini yaku wapa wao isipo kuwa hayo masemi ambayo yame zoewa na ambayo yame rudiliwa mara nyingi sana kiasi kwamba nuru ya masemi hayo ya mwanzoni ime geuka kuto ku ngaa na kwa mwisho haya maanishi chochote kile kwa masikio ya wasio mjuwa Yesu Kristo kama bwana na Mwokozi wao. Labda hawaji kanisani kwenu sababu wana ogopa waweza wakaja kugeuka na ku wafanana ninyi jinsi mulivyo.

Kuna makundi ya watu ambao hawajali. Ibada zao za kanisa zinafanyika sawa-sawa na jinsi wanavyo furahia zi fanyike nao hawataki kitu chochote ki pindue mipangilio yenye starehe ambayo wao huifurahia kwa sasa. Wao ni vyombo vizee ambavyo havina uwezo wa kuwekwamo ndani mvinyo mpya navyo hu chukia mabadiliko yoyote yale. Ingawavyo, sherti tufikie hatua ambapo tuna weza ku kiri kuwa kuna kitu fulani ambacho tume pungukiwa na ya kwamba moto tayari ume zimika kwenye mazabau zetu. Ni kwa wakati ule tu ambao tuna fikia kiasi cha ku kiri kuhusu hali hii ya mambo ndipo tunapo geuka mioyoni mwetu na ku uitikia mwito wake kwa ajili ya Uamusho.

Agizo Lake la Mwisho

Wakati wake wa ku ondoka ulipo fika karibu kabisa, jambo ambalo Yesu Kristo alilo tu agiza la mwisho lilikuwa ni kuihubiri Injili ulimwenguni pote, naye aka tuachia ile Kazi Kubwa. Wakati ambao mtu fulani tumpendaye anapo karibia ku agana nasi kwa mara ya mwisho, huo unakuwa ni mda wa

pekee. Anapo simamisha hatua zake kwenye mlango ili ku ondoka na ku ivuka miimo ya mlango na halafu ana tu geukia akiwa na jambo la mwisho ambalo ana tu omba, ni jambo ambalo tuna lishikilia sana moyoni mwetu. Ombi la mwisho ni jambo la muhimu. Baba anaye karibia kifo na ambaye ana wa elezea wana wake jambo la mwisho analo waomba kuli fanya ili aweze ku hakikisha kuwa aweza kufa kwa amani hali aki fahamu kwamba wao wata li timiza. Yesu alitu achia ile Kazi Kubwa. Hili lilikuwa ndilo kusudi lake hasa la Yeye kufa msalabani. Yesu alikufa ili ku waokowa wenye dhambi waepuke moto wa Jehanum, naye alituachia kazi yaku imalizia huduma hiyo. Yeye haku tu agiza kamwe tu fanywe kuwa wasomi walio funzwa, waongozi mashuhuri wa jamii ao wachunguzi wa kidini. Ali tuagiza wazi-wazi – ku watafuta walio potea. Jikane nafsi yako, uchukuwe msalaba wako na Uni fuate. Na halafu Yeye aka elekea wapi ? Golgotha kwenda ku yatoa maisha yake ili ku watafuta walio potea.

Je tume ichaguwa ile-ile njia nyembamba, ao tume kuwa tuki zunguuka-zunguka na ku tanga-tanga katika njia pana za dini ambazo hazi ongozi watu popote ? Je mioyo yetu ina tu hakikishia wazi kuwa kwa njia ya kuja kwetu kanisani tuna endelea kuitimiza ile nia ya mwisho aliyo ionyesha Yeye? Je ku furahia ushirika kati ya watakatifu kume chukuwa nafasi ya kazi yaku waokoa wenye dhambi ? Je tuna rizika sababu tayari sisi tume okolewa, ila mtazamo wetu una ishia kwenye eneo linalo zunguukwa na vibambazi vya kanisa ? Wakati ambapo uangalifu wetu unapo baki uki elekezwa kwenye mambo ya ndani na hali tuki pungukiwa ku wa tazama walio inje ina maanisha kwamba tumefika ku shindwa ku shikilia kwa nguvu lengo la wokovu wetu sisi. Na wakati kanisa lina kosa ku angalia zaidi ya eneo lililo kati ya kuta

zake lenyewe, tayari lina kana sababu hasa ya hilo kanisa kuwepo.

Hatuku okolewa kwa ajili ya faida yetu wenyewe. Ikiwa kama lengo nzima la wewe ku okolewa lili kuwa wewe kwenda Mbinguni, halafu kwa nini basi isiwe wewe kuja mbele kwenye madhabau, ku omba ombi la ku tubu, na halafu ushikwe na mushtuko na kufa ? Kwa nini kuenda huku na kule ? Ni kama una endelea ku poteza tu pumzi. Kwa nini ku endelea kua kwenye dunia hii ? Nenda zako. Hebu uondoke hapa. Nenda zako Mbinguni na uachane na dunia !

Lakini sasa, wewe haukufa wakati ule. Sivyo ? Labda ni kwa ajili ya kitu fulani cha ziada zaidi ya wokovu wako wewe binafsi. Labda tume pokea kipawa hiki cha wokovu ili ili tuweze ku kifikishia wengine. Kama sivyo, kwa nini basi tungeli weza kuwa bado tungali hapa ?

Wakati ambapo madhabao zetu ziko tupu, tuna endelea kuli sahau agizo hili la mwisho la Mwokozi wetu ambaye ali utowa uhai Wake kwa ajili ya nafsi hizi ambazo tume zi sahau. Tunazo karamu zetu na tume waalika marafiki wetu, ila tumeshindwa ku watafuta vipofu, walemavu na maskini sawa-sawa na Yesu alivyo tu agiza ku fanya.

Patano la ndoa

Katika Biblia, muungano wa ndoa una onyeshwa kama picha ya uhusiano wetu na Mungu. Yesu Kristo ni Bwana, na sisi ni bibi-arusi. Kila kitu tokea hali ya uchumba hadi habari yaku wazaa watoto kina ulinganisho wake na uhusiano wetu na Yeye. Ina onekana kama Mungu ame tupatia picha hii

ikiwa ime chorwa kwa rangi zilizo wazi, na ambayo ina husisha mahusiano yalio ya muhimu sana hapa duniani, ili iwe kumbukumbu la wakati wote na iliyo wazi sana kuhusu jinsi Maisha yanavyo takiwa kuwa. Maisha ya ndoa hayaishii tu kwenye uhusiano wa kujuwana kimwili, ingawa kama jambo hili ni sehemu ya uhusiano wetu na ambayo, iki ambatanishwa pamoja na mapenzi ya Roho wa Mungu, ni jambo nzuri sana. Wala ndoa hai ishii tu kwenye ku shugulikiana bwana na mke wake, ku itunza nyumba iwe safi na ku tunza kitanda, kukipika chakula ao ku ondoa taka-taka. Mambo haya yote yana ufananisho wake katika maisha yetu ya ku tembea na Mungu, ila lengo la musingi la muungano wa ndoa ni ku weza ku zaa na ku ongezeka na ku ijaza Inchi kwa uzao. Ndivyo alivyo wa eleza Adam, Nuhu, Abraham, na Yakobo. Tuli olewa na Yesu ili tumu leleye jamaa.

Mwanamke akiwa tasa, hasa kwa wakati wa Agano la Kale, lilikuwa ni jambo la aibu kwa mwanamuke ule. Leo hii, ni kweli kwamba, tokana na hali ya akina mama wetu ambao wana zamiria hasa kuwa kwenye kazi mbali-mbali, kuli leya jamaa hakupewe ule ule umuhimu ulio upewa mwanzoni, lakini bila kujali jinsi watu wanavyo itumiya leo, picha hiyo bado ina baki wazi – bibi ali takiwa awazae watoto na ku lileya jamaa. Mzigo huu una wekwa juu ya Kanisa, Bibi Arusi wa Kristo.

Nime wahi kusikia watu waki ji tetea kuto kuji husisha na kuwa tafuta walio potea kwa kusema eti matunda tunayo takiwa kuya zaa ni kwa kweli yale matunda ya Roho amabayo yana zungumziwa katika Barua kwa Wagalatia 5: 22. Mimi sikubali kuwa ndivyo ilivyo. Yale matunda ni matukio ya Roho Mtakatifu atendaye kazi ndani yetu, wala siyo kazi tulio

bebeshwa sisi kuitimiza. Kazi Kubwa tulio achiwa sisi hai tualiki kuji jengea vitambulisho vizuri, ila ina tualika ku ondoka na kuzileta nafsi za walio poteya. Uwazi wa Injili una geuzwa vyepesi na kufanyizwa jambo ngumu la kuleta leta visababu wakati tunapo kataa ku ji toa na ku acha njia zetu za starehe za ki binafsi.

Twaweza kuviona vielelezo vizuri sana viwili vya nia ya kimingu ili ku zaa matunda kwa ku waangalia ANA na RAHELI, wote wakiwa ma bibi tasa wawili na ambao wali weka viapo kwa Mungu kuwa hawakubali kubaki na aibu ya ndoa isiyo zaa matunda. Tayari walikuwa wame shikwa na aibu kabisa ingawa kama wao wali kuwa wao ndio wanawake wapendwa sana wa waume wao. Shabaa ya maisha yao haikuwa wawe tu ma bibi wa bwana ila ilikuwa hasa: kuzaa watoto. Na huku kuzaa watoto hawaku kutaka kwa ajili ya faida yao wao wenyewe, bali wali liona jambo hilo lenye umuhimu ili kuwa heshimisha waume wao. Ndivyo tupassavyo kumu heshimisha Kristo.

Kanisa leo limekuwa mke tasa. Haijalishi yeye ni mrembo kiasi gani, haijalishi yeye ni tajiri kiasi gani, haijailishi amesoma na kupata ma shahada kiasi gani, ikiwa Kanisa hali watafuta na ku wavuta walio poteya, hili limekuwa mke aliye tasa. Tuna onekana ku onyesha uweza wa kuji jengea majengo makubwa ili ku onyesha mafanikio na mapato yaliyo nayo kanisa letu, ila tuna tumia ni mda mdogo sana kushugulika na ku tafuta mioyo itakayo jaza yale majengo. Nafasi za kufanyia mazoezi ya ku jenga miili nazo nyumba za mikahawa ya kikristu ni rahisi ku jenga kuliko kuji shugulisha na ushuhuda wa uso kwa uso kati yetu na wale ambao bado hawaja upokea wokovu. Hiyo ndiyo njia tunayo

tumia ili ku ji epusha na utata. Na tuna tumaini kuwa bado tuna weza kuwa washuhuda pasipo sisi ku kabiliana moja-kwa-moja na ugumu wa ku aibika kwa ajili yaku jiweka wazi mbele ya mtu yeyote.

Je hiyo si kweli ? Je hau yaoni hayo karibu nawe ? Ni wakati gani ambapo kwa mara ya mwisho kanisa ao wewe binafsi mume wahi kuondoka na kwenda kwenye mitaa na ku shuhudia kwa watu musio wafahamu kuhusu habari ya Wakovu ? Na mbona agizo liko wazi katika Luka 14 : 23 ili kuenda kwenye njia kuu na ku wa leta waje katika nyumba ya Baba ili chumba cha Karamu ya Arusi ya Mwana-kondoo kijae watu. Nini inacho kuzuiya ku tenda sawasawa na agizo hili ? ikiwa ni kwa ajili yak u mu ogopa mtu fulani, ina maanisha wewe haumu ogopi Mungu. Ikiwa ni kwa ajili yak u epuka ku aibika, ina maanisha kuwa wewe hau wapendi wengine. Ikiwa ni kwa ajili ya ku huzuria kunako mikutano ya ki jamii, ina maanisha kuwa wewe ume ambatanishwa na ku fungwa na dunia. Ikiwa una fikiri kuwa wewe una wazo nzuri kuliko hiyo, basi una takiwa ku elewa kuwa wewe kamwe huwezi ku ji pangia njia ya mafikiri yako binafsi ili kufika Mbinguni. Ni jambo la ku amini na ku tii tu. Na utiifu ni bora kuliko sadaka za ku teketeza, lakini uasi ni sawa-sawa na zambi ya uchawi.

Jambo kubwa zaidi ambalo lina tu zuiya tusiwe mashahidi wanao fanya kazi yao vizuri mbele ya walimwengu walio nje ni kuto kujali kwetu. Tuna pungukiwa ule moto wa mchangamuko unao takiwa kutu sukuma bila kujali kuona aibu katika ku waelezea watu tusio wajuwa kuhusu mambo makubwa na ya ajabu ambayo Mungu huyatenda katika Kanisa letu na pia kuhusu yale ambayo Yeye anaweza kuwa

tendea. Tuna pungukiwa moto. Mbele ya sisi ku ufikishia ulimwengu moto, ina bidi kuwepo kwanza na moto kanisani mweteu. Na ikiwa huko kanisani hakuna moto, wasio okoka bado wata geuka na rudi nyuma kwenye mambo ya Ulimwengu. Kwa nini wabaki hapo. Una nini yaku wapa isipo kuwa mawazo yako ya elimu ya ki philozofia kuhusu Mungu ? Tuna takiwa kuwa na kitu tunacho weza ku wapa na ambacho wana kihitaji. Wakati moto unapo kuwa uki waka kanisani, uta tupatia msukumo unao ongoza ili tu gawiye wengine nao sehemu ya furaha hiyo tulio nayo – kwa yeyote ule, kwa kila mtu. Bila huo moto, tuwezacho kuki fanya ni ku endelea ku tenda mambo katika ukawaida wa ubaridi-baridi sababu tuna hisi kuwa ndivyo tunavyo takiwa ku tenda tu. Tunacho kihitaji ni moto unao waka kiasi kwamba joto lake lina weza ku sikika dunia nzima. Hilo ndilo jambo linalo utenda uamusho.

Miujiza

Yule yule Roho anaye bubujika ili ku zi ita nafsi zilizo potea kuja mbele ya madhabau ndiye Yule Roho Anaye waponya wangonjwa, Anaye wafufua wafu na Anaye tenda miujiza. Wakati ambao ina weza ika onekane rahisi ku toa visababu vya ki teolojia na na vya ki dini ili ku ji tetea kuhusu madhabau yalio tupu, ni vigumu ku kanusha kule kukosekana wazi kwa uweza wa Mungu uwezao ku tenda ile miujiza ambayo Biblia ina eleza kwamba ita fuatana na waaminio. Nabii Yoeli ana tangaza kuwa Mungu angeli katiza mche wa mahindi (ule mche wa ngano unao zalisha Mukate wa Uzima), mvinyo (ile roho ya maombi) nayo mafuta (mafuta ya upako wa Roho Mtakatifu). Kwa usemi mwengine, hatupokei sasa utimilifu wa Neno Lake, ule undani wa maombi unao tu peleka kwenye uvutio wa juu wa uwepo Wake, ao ile miujiza

ambayo yaweza kutokea kwa njia tu ya Roho Mtakatifu. Miujiza haitendeki sababu mububujiko wa mafuta ume katika.

Gideoni aliona hali ya huzuni iliyo lipata taifa la Israeli. Waisraeli wali mu lilia Mungu awa komboe na shida hiyo, ila jibu la Mungu kwao huko Bochine lilikuwa kwamba alikuwa ame wapa Sheria Yake ili waifuate ila wao wali chagua ku uiga ulimwengu ; na sasa maadui tayari ali shambuliya na ku vamia inchi. Na ndio sababu sasa ili mu bidi Gideoni ku pepeta ngano kwenye shinikizo (kino), kwa siri. Kule ku pepetwa kwa ngano, inayo zalisha Mkate wa Uzima, na lile shinikizo (kino) cha maombi ambayo tuna yatumiya ili ku utafuta uso wa Bwana vili tumiwa kwa siri. Na kumbe, ni katika ile nafasi ya siri pamoja na Mungu, ndipo maombi hu jibiwa.

Mungu akamutuma malaika ambaye ali muita Gideoni kuwa mtu mwenye nguvu na wa maana, ila jibu la Gideoni kwa malaika lili kuwa ku uliza ikiwa miujiza ile ambayo wali isikia habari zake toka vinywa vya ma baba zao ime kwenda wapi basi ? Mashamba ya mavuno ambayo sasa yalikuwa yaki chukuliwa na ku porwa na Wameleki yalikuwa ni ushuhuda wa mambo mabaya wa mambo yanayo tokea wakati unapo ku baliana na mambo ya Shetani. Wakati ule tunapo ruhusu dunia ku vamia mashamba ya mavuno, ina tukia kwamba tuna saliti haki yetu ku shugulikia yale mavuno. Tuna baki wazaifu na wasio na uwezo wowote mbele yao wakati ambapo ni sisi wenyewe tulio wa ruhusu watuingilie kwenye mipaka yetu.

Gideoni ali kiri hali ile ya ukiwai iliyo kuwepo na aka I pepeta ngano yake katika ile shinikizo (kino) la Bwana wakati

ambao wangine wali ona radhi ku kubaliana jinsi ambavyo mambo yalivyo kuwa yaki enda, hata kiasi cha ku mu jengea Baali madhabau ili ku wa furahisha adui. Wakati ambao wangine wali tosheka na kanisa lisilo na uhai ndani yake, Gideoni yeye haku tosheka.

Jibu la malaika kwa Gideoni lili kuwa ni ku mueleza eti: « Enenda kwa uwezo wako huu na uta li komboa taifa la Israeli.» Uwezo ule ulikuwa ni nini ? Uwezo wa Gideoni ulikuwa ni kule ku tambua kwake hali ya taifa lao ku ikana imani ya kweli na kule kuji tenga kwao na Mungu na tena kule kuto kukubali kwake yeye Gideoni ku jiunga na hali hiyo ya machukizo mbele ya Mungu.

Kwa lini, kwa mara ya mwisho ulipo ona mgonjwa aki ponywa, mufu aki fufuliwa, mumiminiko wa Roho Mtakatifu ndani ya ibada zetu, watu waki miminika mbele ya madhabau ili kuja ku upokea wokovu ? Ikiwa kama makanisa yetu ni mazuri kiasi Sasa jibu alilo mu rudishia malaika kwa haraka lili onyesha hali ya mtu ambaye tayari ame kata tamaa :

« Eh Bwana wangu, ikiwa BWANA yu pamoja nasi, mbona mambo haya yote yametupata ? iko wapi miujiza yake ya ajabu walio tuhadithia baba zetu, wakisema, Je ! Siye BWANA aliye tuleta huku kutoka Misri ? »

Ndiyo. Hilo ni ulizo njema. Miujiza iko wapi ? hiki, halafu Roho wa Mungu ame baki wapi ? Miujiza iko wapi ?

Uponyaji kwa imani ume kuwa haba ni sababu haut u tazamie. Na tuna shikilia ki karatasi cha ku mu alika Daktari Muganga katika mikono ile ile tunayo iinua ili kuwa ombea wagonjwa wetu uponyaji. Sisi tuna sema huu ndio uangalifu, ila Mungu Yeye ana uiita ni ukosefu wa imani. Na je huja

subutu ku muombea mufu afufuke ! Waki jizuiya kabisa kukulaumu wata sema : hilo ni kuvuka mipaka ; la sivyo, wata sema : ni jambo la ku rukwa na akili.

Sisi, katika ku kubaliana kwetu na ukiwa wa kiroho, tuna tazamia kupata aina fulani ya amani ambayo kamwe hai wezi kupatikana katika ku afikiana na ulimwengu. Lakini walio wa Mungu kama Gideoni, huona kwa macho ya imani yale yasiyo onekana bado kwa macho ya mwili na wao hukataa ku rizika mpaka wakati wanapo ona linatendeka.

Ku zimika kwa miujiza ndani ya makanisa yetu ina zihirisha ku zimika kwa Roho Yule anaye fanya miujiza yenyewe kutokea. Na mbona tuna baki katika kuto kujali na ku ji hisi kuwa tuna tosheka pahali pa ku kubali ku pambana na jinsi hali ya mambo yalivyo kiasi kwamba uweza wa Mungu ume tuacha tukiwa na kanisa tupu lililo na vibambazi vilivyo vunjika.

MASHAMBA YALIYO HARIBIWA

*Yaliyo sazwa na tunutu yameliwa na nzige ; yaliyo sazwa na nzige yameliwa na parare ; na yaliyo sazwa na parare yameliwa na madumadu***.** Yoeli 1 :4

Sura ya kwanza ya kitabu cha Yoeli kina eleza kuhusu kuikana imani ya kweli na kuhusu uwamusho mbele ya Kuja kwa pili kwa Bwana. Mashamba ya mavuno ita kuwa ime haribiwa na wadudu waharibifu wamoja baada ya wengine hadi kuwe hakuna kilicho baki. Ana waalika watunzaji wa mizabibu pamoja na wale wanao utumia divai, wale walio itwa ili kuitunza mizabibu na mtini wa Bwana, na ku tangaza kuwa ile divai ita ondolewa toka vinywani mwao wa toka nyumba ya Bwana. Nafaka (Neno la Mungu) lita tupiliwa,

divai mpya (ushirika wa maombi) itanyauka, na mafuta (mafuta ya upako wa Roho Mtakatifu) ungeisha. Hata sadaka za ku teketezwa zita ondolewa katika Nyumba ya Mungu.

Bwana ana waalika watumishi wake ku lia na ku omboleza kwa ajili ya Kanisa kuwa katika hali ya ukiwa. Kondoo wanalia kupata malisho, wana tangatanga ku jaribu kupata malisho, ila malisho hayapatikani. Maghala na nafasi ambapo mavuno yana takiwa kulindwa pamebomoka. Hata vile vijito na visima vya maji ya uzima vime kauka. ukiwa ulimo kanisani

Tayarini, enyi wakulima ; pigeni yowe, enyi watunzaji wa mizabibu ; kwa ajili ya ngano na shayiri, maana mavuno ya shamba yamepotea. Yoeli 1 : 11.

Hili ndilo neno la makaripiyo makubwa tunayo karipiwa. Mavuno ya nafsi zisizo ujuwa upendo wa Mungu zipo ziki potea na kwenda Jehanum, na Mungu ana tu laumu. Sisi ni watendakazi ambao tuli stahili kuyaleta mavuno katika Nyumba ya Bwana. Lakini, je tuna iona aibu kwa kuto kutenda hivyo ? Hatuioni aibu. Tuna lemewa na shuguli za ibada za makanisa yetu kiasi kwamba tuna shindwa hata kutambua jambo hili.

Hii ndiyo picha ya kanisa wakati ambao siku ya Bwana itakuwa ime karibia. Amosi alisema kuta kuwa njaa, na si njaa ya chakula wala kiu ya maji, bali njaa ya ku yasikia maneno ya Mungu. Makanisa yame enea kila nafasi ila hatu lishwi na mambo ya kindani ya Mungu. Ni ajabu, una weza kuona vitabu vya ma Biblia kila unapo angalia, ila sawa-sawa na alivyo lia Isaya katika sura 29 : 11, kitabu kime wekwa

muhuri (kime kuwa fumbo) kwetu sisi – tuna kisoma, ila ku elewa kwetu kuna shika kwa shida hata ki juu juu tu. Nafaka, kina cha ndani cha Neno la Mungu, kime kauka. Tuna uguwa, ila hatujuwi tuelekee wapi ili tupate chakula sababu upeo wote wa kiroho ume haribiwa.

Kama ningali kuwa kipofu asiye na ufahamu kuhusu hali ya ulimwengu unao nizunguuka, sura hii ya Unabii wa Yoeli pekee yake ingeli tosha ili kunifanya niamini kuwa katika siku za mwisho kanisa litakuwa lime jitenga mbali na Mungu kiasi kwamba kungeli baki sehemu ndogo tu au hata hakuna sehemu yoyote ya mashamba yenye mbolea ya mavuno sawa-sawa na jinsi ilivyo kuwa mbeleni wakati mavuno ya nafsi zinazo okoka zili kuwa ziki miminika, huku kukiwepo na mububujiko wa Roho wa Mungu. Ulimwengu wa makanisa yetu ume kufa ila tume zoea kule kuwa kwetu mbali na Imani ya kweli kiasi kwamba tuna kataa ku kiri jinsi hali ya mambo ilivyo hata wakati ambapo Maandiko Matakatifu yana ishuhudia mbele ya macho yetu.

KIZUIZI CHA UGUNDUZI

Kwenye hatua fulani, katika mwenendo wa kujichunguza, tuna paswa ku fikia kuelewa kuwa, hata kama tunge lipenda kanisa letu kiasi gani, ikiwa kama hatuzi vute nafsi za walio potea, ina maanisha kuwa hatuna uamusho. Ingawa kama kauli hii yaweza ika onekane rahisi na wazi sana, swali la ku fikia ku uelewa ukweli huu ndicho kizuizi kikubwa zaidi kinacho zuiya mengi sana kati ya makanisa yasi uone utendaji wowote wa kipekee toka Mungu ndani yao.

Yesu ali sema kuwa hakuna yeyote awezaye kuja

kwake kama Baba haku muita. Na tuki fikiri kimusingi, ikiwa kama ni Roho wa Mungu ndiye anaye zivuta nafsi za watu kwa toba, na basi ikiwa nafsi haizionekani ziki elekea kwenye madhabau yako, basi ina ingia akilini kuwa Mungu hawavutii hapo. Na una takiwa uji ulize ni kwa sababu gani.

Sisi ni chumvi ya dunia, ladha inayo kifanya chakula kuwa na onjo nzuri. Ikiwa kama tume poteza tayari onjo (ladha) yetu, halafu hatuna tena chochote kile ambacho kina ladha nzuri. Dunia ina weza ikawe na kiu cha ukweli, ila hawataki kile kitu ambacho sisi tuna wa tolea sababu hakina ladha (onjo) nzuri.

Je madhabau yako ni matupu ? Je kuna ukame wa miujiza na ma zihirisho ya ki ungu ? Je ibada zenu zime isha ku geuka kuwa mafunzo makavu kuhusu Mungu kwa njia ya nukta 5 ya maneno, shairi fulani, na halafu habari kama kadhaa za ku chekesha ? Je uweza wa Roho Mtakatifu hau miminike tena ndani ya ibada zenu kama upepo wenye nguvu uvumao ? Je ime wahi kuwa hivyo mbeleni ? Labda huu ndio wakati wa ku kabiliana na jinsi hali inavyo onyesha kuwa mambo yame enda kabisa vibaya kuhusu kanisa lako. Kuna kitu cha muhimu kinacho kosa katika kutembea kwenu pamoja na Mungu na nyinyi muna takiwa kuki rekebisha tena. Musipo fanya hivyo, halafu pahali pa ku endelea ku tembeya Naye, muta jikuta kuwa mupo muki zunguuka kwenye mambo yasiyo na malengo.

Kwa hakika yawezekana muna weza kuwa mume tosheka kabisa nalo kanisa lenu jinsi lilivyo. Ikiwa ndivyo ilivyo, halafu muta yapata kabisa yale munayo yataka. Mungu Yeye hata wasukuma kutaka kuwa peleka umbali musio taka

ku ufikia. Kama aki fanya hivyo, kamwe hamuta kuwa tayari ku chukuliana na beyi ile ita kayo wa hitaji kui gharamia, nanyi hamuta komaa kamwe kufikia ukomavu wa ku walea watoto wachanga katika Kristo ambao Yeye angeli taka kuwa tuma kwenu. Ali toa uhai Wake kwa ajili ya nafsi hizi ambazo ni za bei ghali mbele ya macho yake, naye kamwe hawezi ku ziweka mikononi mwa watu wasio jali vya kutosha kiasi cha wao pia ku towa maisha yao kwa ajili ya hizo nafsi.

Kanisa lisilo zivuta nafsi zilizo potea ni kama mtini ulio nyauka pasipo kuwa na matunda. Mzabibu wenye matawi yalio nyauka. Yesu ali laani mtini ingawa kama hayakuwa ndiyo majira. Hakuna aina yoyote ile ya sababu uwezayo ku ji tetea na ambayo ita igeuza hukumu ya Mungu kwako kwa ajili ya ku kosa matunda. Hakuna wakati ambao sio majira bora kwa kazi ya kuzivuta nafsi za walio potea.

Mtini usio zaa matunda una takiwa ku katwa sababu ni mti ulio kufa na ambao hauwezi kamwe ku rudi kwenye uzima na uta ichosha sehemu hiyo ya shamba bila sababu. Wakati ambapo umaji maji wenye uhai unapo kosekana ku bubujika kwenye kanisa lenu, lime kufa na halina faida yoyote isipo ku tupwa na ku chomwa kwenye moto. Wakati ambao hauoni tena nafsi zilizo potea kuja na ku upokea wokovu, na wagonjwa ku ponywa, miujiza na mazihirisho ya Roho Mtakatifu yaki onekana, labda huo ndio wakati wa ku kiri kwamba kanisa lenu limekufa.

Ukarimu, Jambo kubwa zaidi katika hayo

Mara nyingi nawasikia watu wanao kuwa tayari saa zote kulitetea kanisa lao kwa njia ya ku onyesha kazi za

matendo mema. Wana fanya mipangilio ya ukusanyaji wa chakula kilicho wekwa kwenye vibweta ili ku tolewa kwa maskini, matoleo yanayo itwa ya Santa Claus ili ku yatolea watoto wadogo, na kazi zingine za kujitolea kwa ajili ya watu tunao ishi nao. Haya yote ni mambo mazuri ila sizo alama za uamusho.

Kuna hesabu kubwa ya matendo mema mengi ambayo tuna weza kuyatenda – na tuna takiwa ku yatenda- sisi kama Kanisa la Yesu Kristo. Ila wasio okoka bado nao pia hutenda matendo haya. Je hii ina maana kwamba wame jazwa na Roho Mtakatifu. Upendo, upendo wa kweli, ni zaidi ya kuwa na matendo mema. Upendo ni kule kuji tolea mwenyewe kwa sababu ya pendo ili nafsi za walio potea waweze ku okolewa. Ni kule ku mu vaa Yesu Kristo, na ndicho kiini hasa cha Ukristo na maana ya kwanza ya Msalaba. Lengo lake la kwanza kabisa ni ku zileta nafsi zilizo potea ziupokeye Wokovu na pia kuzilea. Wakati ambao upendo wa kweli upo kanisani, washirika wata waleta walio potea waje kuisikia Injili. Wakati ambao upendo huo una kosekana, hakuna anaye guswa moyoni kwa ajili ya ku hurumia wanao potea, na halafu madhabau yanabaki utupu.

Yesu ame tupa amri ya ku waalika walio wagonjwa, walemavu na maskini kwenye karamu zetu za upendo, sio tu marafiki wetu, ila tunapo tazama katika mikutano yetu, sura tunazo ziona ni zile zile za zamani ambazo tuna ziona kila wiki. Ikiwa ndivyo ilivyo kanisani mwenu, ina maanisha kuwa kuna kosa upendo na hapo na ni alama kuwa hakuna kabisa uamusho mahali hapo.

Sura ya 6 ya kitabu cha Amosi ina onyesha hali ya

watu walio tosheka na ku tulia, waki furahia baraka za ki maisha, ila mioyoni mwao hawa huzunikie kupotea kwa wengine wasio na wokovu… Wao hulala kwenye vitanda vyao vya shaba bila ku huzunika kuhusu mateso ya Yusufu. Hawa ndio wata kuwa wa kwanza ku onja uchungu wa hukumu, sababu hukumu ita anzia nyumbani mwa Mungu. Hili silo jambo la kutaka ao kuto kutaka na ambalo halina madhara. Ikiwa kama wewe hau sukumwi na upendo ili kuwa tafuta na kuwa leta wale walio potea, ku uwasha moto kanisani mwako na ku anzisha mububujiko wa maji ya uzima yatokayo Mzabibu wa Kweli, halafu uji andae kukutana na gadhabu ya Mungu sababu wewe huku jali kuhusu nafsi ambazo Yeye ali utoa uhai wake ili kuzi okoa.

Mizali 29 : 18 ina tueleza kuwa, pasipo na maona, taifa hupotea. Maona yako yanabidi yawe makubwa kuliko jinsi ulivyo, makubwa kuliko kule kuhuzuria kwako ibada ya Jumapili, makubwa kuliko maoni yako ya ki dini – maono yako yana bidi yalenge uamusho wa ku liletea kanisa uweza na ku zivuta nafsi zilizo potea zimujie Kristo. Mbali na hilo, mengine yote ni kanisa la mfano tu.

Ni nini itakayo ku pelekea uelewe kuwa kuna kitu fulani ambacho kanisa lenu lina pungukiwa ? Tume baki mda mda mrefu sana bila uamusho wa kweli kiasi kwamba sasa tume shindwa ku juwa alama wazi zinazo onyesha hali yetu ya kukosa uhai na halafu tuna ji wekeya vi sababu huku tuki jilinganisha na kanisa lingine jirani ambalo nalo halina uhai ili tuweze kuji tuliza mioyo kuwa bado mambo yetu ni «mazuri».

Ikiwa wewe una taka tu kuwa «wa kawaida» na una

endelea na njia ya urahisi urahisi ku elekea Ukristo wa ku changa-changa (wa ku afikiana), kamwe huta uona utendaji wa uweza wa Mungu katika maisha yako. Ikiwa ni hali hiyo ndiyo unayo rizika nayo, na ni hiyo hali tu ndio uta endelea kuwa nayo. Lakini kama uki taka ku jionea uwezo mkuu na utimilifu wa nguvu za Mungu, ni lazima kwanza ukubali ukweli kwamba kwa sasa hauna uamusho.

Ni wakati ule tu ndipo sasa una weza ku piga hatua nyingine ili kujionea jambo lililo la kiungu lisilo la kawaida liki tokea na ambalo lita zungumziwa milele yote.

II. MWENYE KIU KIKUBWA CHA KUUPOKEA UAMUSHO

« Na wakati Rakeli alipo ona kuwa hamuzalii Yakobo hata mtoto mmoja, Rakeli aka muonea wivu dadaye ; na aka muambia Yakobo , Nipe watoto , na kama sivyo, nita kufa .» Mwanzo 30 : 1

Kutambua kuwa hamuna uamusho ndani ya kanisa lenu ni kitu kimoja, ila ni kitu kingine tofauti kabisa kutaka ku upokea uamusho. Twaweza tuka fikiri kwamba ni kawaida mambo haya mawili kuenda pamoja, ila sivyo ilivyo.

Rakeli hakuwa aki omba baraka kwa ajili yake yeye mwenyewe – alikuwa na shauku kubwa kwa ajili ya nafsi za watu. Hapa ndipo wengi kati yetu wame kwenda inje ya mstari. Jambo hili si kwa ajili yetu – ila kwa ajili ya wengine. Na si Uamusho kwa ajili ya uamusho tu, au siyo utendaji wa Mungu ili tuweze kuji sikia vizuri kuhusu sisi wenyewe. Ni kule ku guswa kweli kweli ndani ya mioyo yetu kuwa nafsi za watu walio umbwa kwa mfano wa Mungu zita ishia kwenye Jehanum ya Milele ikiwa sisi hatu fanyi chochote ku zuiya jambo hili lisi tokeye.

Shauku yako ya Uamusho ni ya kiasi gani ? Sawa sawa na Rakeli, una takiwa kuwa na kiu ya Uamusho kiasi ya kuwa tayari kufa kwa ajili yake, kuwa tayari kutoa uhai wako ili kuona nafsi zikiokoka. Kama sivyo, mengine yote ni kama chombo kinacho fanya kelele, – kelele nyingi zisizo na faida. Au kama na jinsi Waraka wa Pili wa Petro unavyo izungumzia : ni kama visima visio na maji, mawingu yasio na maji. Tuna sema kuwa tuna taka Uamusho sababu tuna

fahamu kuwa hilo ni jukumu letu kama wakristo, ila ulizo ni kujuwa ni kwa kiu cha kiwango gani tuna uhitaji ? Gharama inayo hitajika ku lipwa ili ku ufikia uamusho wa kweli ni kubwa sana kuliko jinsi mwanadamu mwenye mwili awezavyo kuwa tayari ku itoa. Ina bidi kazi ya Roho wa Mungu ili kutu fikisha kwenye hali ya musukumo wa kujikana na ambao uta tuongoza kuzi acha hali zetu za starehe na ku jitwika wenyewe mateso ya Mwili wa Kristo.

Na hii siyo ku teseka bila kufikiri kwa ajili tu ya kuji acha uteseke, ila ni ukubalifu wa ku jitoa nafsi zetu, roho pia mwili, kwa ajili ya uzihirisho wa ushindi wa lengo la Ufalme wa Kristo. Katika kitabu cha Ufunuo, Mungu hasemi kwamba wale watakao jaribu ku tenda watakula matunda ya Mti wa Uzima : ni wale *washindao*. Kizuio kikubwa zaidi tunacho pambana nacho ni nia ya miili yetu wenyewe. Ina tubidi kwenda juu zaidi ya ukawaida na starehe na ku fikia mwenendo wa kutembea na Mungu unao fikia kiasi cha ku sulubisha zile nia za mwili kiasi kwamba tuweze kutembea katika Roho wa Mungu. Huo ndio mutiani ambao Mungu ana uweka mbele yetu ili ku upima uamuzi tulio uchukuwa. Huo huwatenga kondoo na mbuzi na ku wainua kwenye daraja lililo juu kuliko uvuguvugu, waume na wake halisi walio upande wa Mungu.

Upinzani zidi ya Mabadiliko

Watu wengi hawa taki jambo lolote linalo leta mabadiliko. Wanapo fikia wakati ambapo tayari wame weka mpangilio wa mambo katika muundo wanao ufikiria kuwa ndivyo unavyo takiwa uwe, wao hu tetea muundo huo kwa nguvu zao zote. Kuna watu wengi ambao wana upenda huo

usitiri wanao uhisi wakiwa katikati ya vibambazi vinavyo wa zunguuka ili wasikie kwamba wako salama. Kila ufa unao jitokeza katika huo usalama wao unaonekana kwao kama tishio zidi ya jinsi ambayo tayari wame ya pangilia mambo katika fikara zao. Wao huona kuwa ni shida sana kutembea bila ku kunyaga ardhi kavu inayo shikilia kidete chini ya nyayo za miguu yao, kiasi kwamba wana ona kuwa ni rahisi zaidi ku shikamana na lutirjia ya kitamaduni ambayo wamekwisha kuizoeya pahali pa ku ji unga na jambo linalo fanana kuwa halija fanyiwa jaribio na tena ni la kimapinduzi. Wao wame banwa katika «ibada sawa na ilivyo kawaida» - mitungi mizee isiyo weza kujitanua na kuibeba divai mpya.

Shida iliyopo ni kwamba misingi walio i jenga juu yake ime simikwa juu ya vyanzo visivyo vya kweli. Dini ni uwakilishi wa kimwili wa mwenendo wetu pamoja na Mungu, ila tukiya shikilia yaliyo ya kimwili ili kutaka kuweka imara yaliyo ya kiroho, tutajikuta tume kumbatia fungu la mchanga mtupu. Imani ni kuwa na uhakika wa mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo YASIYO onekana. Ikiwa kama tumaini lenu lina jengwa juu ya mambo ambayo muna weza ku ya ona kwa kuwa hamuwezi nyinyi ku yashikilia yale ambayo hamuwezi ku yaona kwa macho, halafu ita kuwa vigumu kwenu ku yapokea mabadiliko ya kiungu katika kanisa lenu.

Lazaro ali itwa aondoke toka kaburi lililo chongwa katika mwamba (wa jiwe kuu), hali aki fungwa mikono na miguu kwa mavazi ya ki mazishi ya kidini na mila na uso wake ulikuwa umefungwa na kitambaa kiasi kwamba asingeli weza kuona. Sawa sawa na ilivyo kuwa kwa Lazaro, watu wengi leo wame fungiwa ndani ya makaburi ya miamba (ya mawe makuu) na wana kosa njia ya kutokea. Amri ya Yesu

ilikuwa kwamba wamu fungue Lazaro toka hivi vifungu vya desturi na kumuacha huru. Mkono wa Mungu una hitajika ili kuli viringisha jiwe ili kuwa acha huru hawa watu, ila agizo lake kwetu sisi ni kwamba tuwa funguwe toka vifungo vilivyo oza vya mila na desturi. Hawawezi ku jifungua wenyewe. Tuna takiwa kuleta mahitaji kuhusu watu hawa katika maombi yetu, sababu ni Mungu pekee yake anaye weza kuwa hakikisha wafunguliwe na kule kubanwa katika vifungo vya kamba za ngozi ngumu za desturi za kale.

UZAIFU NA KUTO KUJALI

Kuna watu wengine ambao uzaifu wao mkubwa una wazuiya ku uhitaji uamusho. Hata mtu aliye mjinga yeyote yule ata fahamu kuwa kuutafuta uamusho ni neno linalo andikwa kwa matamko yafuatayo : K-U-T-U-M-I-K-A, wakati ambao kuna aina ya watu ambao hawajali kamwe kuji shugulisha kiasi hicho. Kwao, si shida ikiwa kama mtu mwingine ata jitoa ku ifanya hiyo kazi au la, ila tu usi waombe wao kuisulubisha miili yao, hasa kwa ajili ya mtu ambaye hawajawahi kukutana naye mbeleni. Siyo shida kwao ku ingia kwenye kipindi cha maombi, ila isiwe kipindi cha maombi ya usiku mzima, hasa wakati ambapo ni maombi yasiyo elekeya mahitaji yanayo wahusu wao binafsi. Kwao siyo shida ku shuhudia ila tu iwe ni kumu tolea ushuhuda mtu ambaye tayari ame kwisha ku okoka na ambaye ana kubaliana na maoni yao, ila usi waelezee waende kwenye njia kuu na kwenye njia ndogo-ndogo kushuhudia kwa walio potea. Wana shikilia kwenye wokovu wa ukawaida ambao una wapelekea kudhania kuwa wanaweza ku shikilia tu kwenye sehemu ya koti wanazo zivaa wachungaji wao na kwa njia hiyo ku ingia Mbinguni. Ila, fahamu kuwa, hata wakati

ambapo yawezekana uji fiche kwa kuketi kwenye kiti cha nyuma kabisa kanisani, huta weza kuji ficha mbele ya Kiti cha Hukumu cha Mungu.

Wakati nilipo kuwa bado mchanga katika Bwana, nili wahi kumuuliza ni sababu gani watu wamoja huupokea wakovu ila wengine sivyo ; kwa nini wamoja husimama katika wokovu huku wengine huanguka na kurudi nyuma. Aka sema nami moja kwa moja : «*kuna wanao jali, na wengine hawajali lolote. Ni hivo tu.*» Hili lilikuwa ni moja kati ya mambo ya ndani sana ambayo nime wahi kuya sikia. Siku zote maji huji sawazisha yenyewe. Mtu yeyote ana weza kutambua hilo hitaji, ila ikiwa sisi wenyewe hatujali kabisa, sherti tuta rudi nyuma na kurudilia kwenye kiwango kile ambacho tuna dhani kuwa kina tutosha. Ila sasa, tuki hitaji uamusho, tuna takiwa ku kivuka kiwango kile cha nia zetu za kimwili. Ikiwa tutajaribu kuinuka juu kuliko viwango vya nia zetu za mwili bila mioyo yetu ku washwa na upako wa Roho wa Mungu, punde si punde tuta jikuta kuwa tumekwisha tena rudilia viwango vyetu ambavyo tuna jihisi tuna tosheka navyo. Ni Mungu tu ndiye anaye weza kutupa ule msukumo, na ni kwake Yeye tuna takiwa kuomba tuweze kupewa kiu kitakacho tuwezesha kwenda juu ya kule kuridhika kwetu na jinsi tulivyo … ila ni lazima tuombe.

Katika Luka, ime andikwa kuwa ikiwa mwana ata muomba baba mkate, je babaye ata mpa jiwe ? Basi je Baba yenu aliye Mbinguni hata wapa Roho Wake wale wamuombao ? Halafu, dhambi yetu sisi ni kwamba hatuku jali sana ku omba. Kama tungeli fanya hivyo, kwa kweli Mungu angeli tupa sisi kile kiu pamoja na mamlaka ya ku ubeba ule mzigo anao tu alika sisi ku ubeba.

Sawa-sawa na vile ule baba alivyo musihi Yesu ku mu saidia katika kutokuamini kwake, kama inavyo andikwa katika Marko 9 : 24, hebu nasi tu mu lilie Mungu ili aweke kiu kikuu na cha kweli kwa ajili ya uamusho, ndani ya mioyo yetu. Sisi ni wenye mwili, nasi tupo jinsi tulivyo, ila Mungu ana uweza wa ku uweka kwa nguvu, ndani ya mioyo yetu, mzigo ule wa kiu ya uamusho, kiu ya utakatifu, na kiu ya kuwaendea walio potea kiasi cha ku fanya tubadilike na kuwa tofauti na jinsi tulivyo. Ikiwa kama hatu ombi kwa ajili ya ku wekewa mzigo huo, haita chukuwa mda mrefu mbele ya sisi kurudi nyuma na kufikia tena kiwango chetu cha mbeleni.

Ingawaje, kama hatua ya kwanza kuelekea uamusho ni kutambua na kusimama ili ku kabiliana na jinsi hali ya mambo ilivyo, nina amini kuwa hatua hii ya pili ya ku kumutafuta Mungu ili achocheye kiu ndani yetu kwa ajili ya Uamusho ndio mtiani wa kwanza ambao tuna takiwa ku ushinda ili tuanze ku uona utendaji wake. Lazima uwe na kiu ; kiu kikubwa sana cha uhamusho kiasi kwamba una ugua moyoni kuutaka. Kwako hakuna njia nyingine pasipo hilo wala hakuna mlango wa kurudia nyuma ikiwa haujionyeshi. Nafsi yako ina bidi itikiswe toka usingizini kwa njia ya moto wa juhudi hadi hapo Uamusho uta kapo tokea. Ila ni Mungu anaye weza kukuwezesha kufikia hilo. Hali hii haijileti ki kawaida tu – ni kwa neema Yake Mungu mwenyewe. Na ndio sababu tuna takiwa ku utafuta uso wake Bwana ili kulifikia. Tuna takiwa ku chukuwa uamzi wa ku anza kuufuata mstari huu wote mzima kwa njia ya ku muomba Mungu atu saidie kuhusu kuto kujiweza kwetu ili auwashe moto wake mioyoni mwetu. Ikiwa kweli tunayo shauku hii, tuta endelea ku omba hadi tutakapo upokea. Tuki katiza maombi yale mbele ya sisi kuupokea, halafu tuta kuwa tume pungukiwa na wito ule tulio

tolewa na Bwana, na tutakuwa tume chagua kwa hiari yetu sisi wenyewe ku kosa kufikia lengo letu, si mbele ya mtazamo Mungu peke yake, ila pia mbele ya mtazamo unao tustahili sisi binafsi pamoja na zile nafsi zote nyingi mno za wale ambao wangeli fikia ku uelekea wokovu kwa ku pitia kuamka kwetu sisi.

Mungu hata zituma nafsi anazo ziona kuwa za bei ghali zielekeye mahali palipo watu ambao hawazijali kiasi cha ku funga na ku ziombea. Sababu akifanya hivyo, nafsi hizo zita kufa kwa kuwa pale hakuna atakaye chukuwa mzigo wa ku wa nyunyizia maji, kuwa lisha na ku uacha moto uendelee ku waka. Ila ikiwa kama walio katika kanisa fulani wana kiu kikuu mioyoni mwao kiasi cha kuwa na mioyo iliyo pondeka na ku utafuta uso wa Mungu kwa ajili ya nafsi zinazo potea, halafu wakati Mungu anapo zituma nafsi kwa watu kama wale, wata iona bei ya nafsi zile kama zawadi zenye thamani amabazo walizo zifanyia kazi.

Tunapo lishinda giza la mtazamo wa macho yasiyo weza kuona mbali na kuwa na maoni yanayo ona umbali upitao mipaka ya macho ya mwili, tuta muona Mungu ambaye Yeye daima hutungojea ili tumuamini ayafanye mambo yasiyo ya kawaida. Hizi ndizo nafsi aminifu ambazo Mungu aweza ku zitumia ili kuuleta uamusho. Walio zimia, wasio amini na waoga kamwe hawata fikia ku inuka juu vya kutosha ili kuweza kutazama toka mlima Pisga ili waweze kuiona Inchi ya Ahadi ya Uamusho. Tuna panda kufikia kuufaulu mtiani kwa njia tu ya Neema Yake, ili katika yote, utukufu wote umurudilie Mungu.

HATUA YA TATU – KUPOKEA TOBA

«*Ikiwa watu wangu, walio itwa kwa jina langu, wata jinyenyekeza na kuomba, na kuni tafuta uso wangu, na kuziacha njia zao mbaya ; basi nita sikia toka mbinguni na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya inchi yao*» 2 Nyakati 7 :14.

Andiko hili ambalo lime nukuliwa mara nyingi, lime andikwa kama kichapo kwenye kitambaa cha ku bambwa kuwa alika watu kuhusu Uamusho ; lakini, ili kuiletea inchi yetu roho ya toba, sherti kuwe na mtu aliye kwenye magoti. Sherti jambo hili lianzie mahali fulani.

Umuhimu wa ku waleta watu kwa Yesu

Tuna takiwa ku fahamu kile tunacho kitubu, mbele ya sisi kwenda kwenye magoti ili ku tubu. Toba ambayo Nabii Yoeli ana tualika kuifikia ni ile ya «ku i rarua mioyo, wala si ku rarua mavazi ». Toba ya kweli hutokeza moja-kwa-moja tokea ndani kabisa ya moyo ulio pondeka na kama sivyo halafu siyo toba ila unafiki wa ki laodikia. Je ni kwa sababu ibada zetu za kanisa hazikuwa nzuri vya kutosha ? au hatuku imba kwa sauti za kutosha ? Au hatukuwa na vicheko vya kutosha ? Kiini cha tatizo ni kipi hasa ? Ni kwa sababu ya kitu gani hasa tuna takiwa kutubu ?

Joeli anasema kuwa nafaka, divai na mafuta vime kosekana Nyumbani mwa Bwana sababu tume ya acha mashamba ya mavuno kuharibika. Hii ina maanisha kuwa nafsi za watu zipo ziki angamia ndani ya mashamba ya mavuno, na Mungu ana tulaumu sisi. Yesu ali toa uhai wake

ili kuwa okoa wenye dhambi ila ikiwa sisi hatu jihusishi vilivyo ili kwenda inje na ku waleta nyumbani mwa Mungu, halafu Mungu ata ondoa uvuvio wa Roho wake juu ya kanisa. Na hii ndiyo sababu imepelekea makanisa yetu kuwa mafu kiasi hiki.

Ikiwa kama sababu kuu ya Mungu kuutuma uamusho ni kwa ajili ya ku vuta walio potea waupokee wokovu, ina maanisha kuwa ni jambo hili ndilo tuna takiwa kuji husisha nalo zaidi ya yote. Pale ndipo palipo kitovu cha tatizo. Ina tubidi kuuondoa mtazamo wa macho yetu na kuacha kuji angalia sisi wenyewe, ili kuanza ku wa angalia wengine.

«Nime tangaza habari, nimeokoa, nime onyesha, na hapakuwa mungu wa kigeni kati yenu ; kwa sababu hiyo ninyi ni mashahidi wangu, asema Bwana, nami ni Mungu». Isaya 43:12.

Nime gundua kuwa ndani ya makanisa mengi, watu wana muelekeo wa kuamini kuwa kama tu wao wanajitolea kwa nguvu zao na kwa mali zao ili kuli inua kanisa lao, kwa njia fulani hii ita pelekea watu wengine kuja na ku upokea wokovu. Halafu wana waachia wachungaji wa makanisa yao kushugulika na kuchukuwa huo mzigo. Je, kwa ajili ya hilo ndiyo sababu wachungaji hulipwa mishahara ? Jibu langu mimi ni kwamba si Wachungaji wanao zaa kondoo ; kondoo ndio wanao zaa kondoo. Jukumu la kuwa tolea ushuhuda wanao potea Mungu Yeye huliweka kwenye mikono yetu sisi sote. Naye hueleza wazi-wazi kuwa siyo swali la kutaka ao kuto kutaka, ila hapo ndipo nafasi tunapo simama ndani ya Mungu tuki tenda kwa ushirika pamoja Naye. Nalo si kama jambo moja la ku tenda katikati ya mengine mengi tunayo

alikwa ku yatenda, ila HILI NDILO jambo la kutenda.

Kuwaleta walio potea kwa Yesu siyo tu huduma moja kati ya huduma nyingine, jambo ambalo tuna ji husisha nalo wakati tunapata wakati, ao jambo ambalo tuna waachia viongozi wa kanisa kuli shugulikia. Silo jambo la kulinganishwa na mipango kama ile ya ku kusanya chakula, ao mipango ya kukusanya vitu vidogo-vidogo vya michezo kwa watoto ili kwamba siku ya Noeli tuvitolee jamaa zilizo maskini, au ku pangilia kampeni ya wanao toa msaada wa damu za ku ongezea wagonjwa. Kuwaleta walio potea kwa Yesu ndicho kiini cha ndani na cha sababu ya kuwa ya wito wa Kristo ; huo ndio mdundo wa moyo wa Mungu. Ni kwa sababu ya kazi hii ndiyo umeitwa kwenye wokovu ili uifanye. Nalo ni moja kati ya kazi mbili za ki msingi za kanisa. Yesu alisema kuwa ametuweka ili tukazae matunda mengi na kwamba matunda yenyewe yadumu. (Yahana 15 :16). Mbele ya matunda yako ku dumu, tuna takiwa kwanza kwenda nje na Kuwaleta walio potea kwa Bwana.

Kanisa la Efeso

Katika Ufunuo sura ya 2, Mungu anali onya Kanisa la Efeso kuwa anazijuwa kazi zao, na taabu na uvumilivu wao na hata jinsi wanavyo zichukia dhambi. Oh ! Wao ni tajiri katika kila aina ya « mambo ya kanisa », ila … wame uacha upendo wa kwanza.

Ule upendo wa kwanza ndio ule ulio kuwa nao wakati ule wa kwanza ulipo okoka. Je unakumbuka jinsi ulivyo ji hisi wakati ule ambao ule mzigo wa dhambi ulipo ondoka kwako ? Wakati ule ulipo jisikia huru kwa mara ya kwanza maishani ?

Wakati ule ulipo jisikia kweli kwamba umepita toka Mautini kuingia Uzimani ? Uli jisikia ku changamka sana kiasi kwamba uli kufikia kumu elezea yeyote yule kuhusu yale ambayo Yesu Kristo ame kutendea. Huo ndio upendo wa kwanza.

Ila tume upoteza ile furaha ya kwanza na ku baki tu na «kawaida ya kanisa ». Ule msukumo na furaha vime poa pamoja na wakati nasi hatuna tena ndani yetu ule moto mtakatifu uwakao. Tume uacha upendo wetu wa kwanza.

Na Mungu ana tueleza nini ? Au tutubu na ku tenda yale matendo ya kwanza, au tofauti. Ata kuja haraka –bila ku chelewa- na kukiondoa kinara chetu. Bila kinara kinacho waka Taa yake, tuta jikuta kwenye giza, tukijikwaa na ku tangatanga. Ku yafanya « mambo ya kanisa » , kuhuzuria ibada za kanisa, ku imba nyimbo, kuwa gawia walio maskini chakula na kutolea watoto vitu vya michezo yao kwa ajili ya siku ya Christmas ni mambo mazuri ku yatenda… lakini hiyo yote haita tuepusha hukumu ya Mungu.

Kuzaa matunda

Katika ku zungumza kuhusu Adamu na Eva, katika 1 Timoteo sura ya 2, Paulo ana tueleza «walakini ataokolewa kwa uzazi wake…». Je Paulo anataka kutu eleza kuwa wanawake wote wasio kuwa na watoto wapo njiani ku elekea Jehanum ? Sivyo hata kidogo. Hapa ana zungumuzia kuhusu Kanisa ! Kanisa, ambalo ni Eva wa pili, ndiye Bibi Arusi wa Kristo, na ndivyo hivi anavyo agizwa ku yazaa matunda. Hebu tusi danganyike ku fikiri kuwa hili ni zungumzo la haraka haraka na rahisi tu ambalo Paulo analo li zungumzia hapa. Hapa ana li zungumzia agizo mhimu kuhusu umuhimu wa kuwaleta walio potea kwa Yesu.

Mara ine katika maandiko (Mat. 3:10 na 7:19, Yoh 15:2, na Luka 3:9) tuna ambiwa kuwa kila mti usio zaa matunda uta katwa na ku tupwa motoni. Katika mfano wa Mzabibu wa kweli Yohana sura ya 15, Yesu ana sema kama tuki kaa ndani Yake tuta ya zaa matunda mengi. Tusipo kaa ndani Yake, ndipo tunapo kauka na ku katwa kisha kutupwa motoni. Yoo ! Motoni ? Je neno hili lina semwa hapa kwa ku bahatisha tu ? Mimi sizani hivyo. Msimamo uko wazi – lengo letu kubwa ni ku kuwaleta walio potea kwa Yesu. Tusipo timiza hilo, sisi ni matawi yalio kauka – matawi mafu na makavu yasiyo na maji ya Roho Mtakatifu ndani ili ku tiririka ndani yetu na halafu tuna usumbua udongo bila faida yoyote.

«basi zaeni matunda mengi, ili Baba yangu atukuzwe… »

Nimewahi ku sikia kuwa shabaa ya Maisha yetu ni ku mtukuza Mungu. Vema, hivi ndivyo Baba hutukuzwa, wakati ambapo wewe una ondoka na kuwaleta watu kwa Yesu. Kuimba nyimbo za sifa na kuinua mikono yako juu ili kutukuza ni vizuri sana, ila ikiwa kama nafsi za watu ziko njiani ku angukia Jehanum wakati ambao wewe uko hapo hali uki ziimba nyimbo, halafu Mungu ana tukuzwaje katika hali hii ?

Na agizo lina shuka tena ndani zaidi anapo ongeza – «… ndipo mta kuwa wanafunzi wangu. »

Na sasa kuna tokea nini wakati sisi hatuzai matunda mengi ? Aha, je umeisha kutambua ninacho taka ku kisema ? Mwenendo wetu pamoja na Mungu, shabaa yetu kubwa yakuwa hai, ina ambatana moja-kwa-moja na kuwatafuta walio potea.

Mfano wa Talanta

Kuna mifano miwili, mfano wa talanta (Matayo 25) na mfano wa fedha (Luka 19) ambayo kimusingi yote miwili ina eleza mafundisho mamoja. Hapo Mungu ana tupatia sote hesabu fulani ya vitu vya muhimu ambavyo tuna takiwa ku vi chukuwa katika mambo ya ulimwengu na ku vitumia kwa ajili ya ku ujenga Ufalme wa Mungu. Ila katika mifano hii yote miwili, kuna watumishi wawili ambao wao hawaku fanya jambo linalo elezwa. Mumoja ali ificha talanta yake udongoni, na mtumishi mwengine ali ificha fedha yake kwenye kitambaa. Wote wawili wali fahamu kuwa Mungu ni «Bwana mgumu». Vema, sasa kwa nini huku taka ku tumikisha kwa njia moja fulani yale ambayo Mungu amekupa ? Hawaku enda hata ku iweka kwenye benki ili Bwana aweze basi ku ichukua pamoja na faida itakayo tokana na uwekezaji wa hiyo. Wala hawaku itowa kwa mtu fulani mwengine aitumikishe na halafu wapate hata ku zalisha sehemu moja ya kumi atakapo irudisha yule anaye itumikisha !

Na sasa, Bwana aka wafanya je ? Mumoja wao, Bwana ana muita « mtu mubaya » na yule mwengine Bwana kamutupa « katika giza la nje ». Maneno haya ‘katika giza la nje’ siyo picha ya Mbinguni – hiyo ni nafasi iliyo wekewa tayari kwa wenye dhambi.

Je habari hii ina utofauti na Mfano wa Karamu ya Arusi tunao upata habari zake toka Luka sura ya 14 ? Kila mmoja alitoa vi sababu kujitetea kuhusu kilicho mu pelekea kuto ku mutumikia Bwana. Na Bwana ali kasirika. Hata leo hii, amri yake ina simama :

"Toka upesi, uende katika njia kuu na vichochoro vya mji, ukawalete hapa maskini, na vilema, na vipofo na viwete… Uka washurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa"

Na nini kuhusu wale ma bwana walio toa vi sababu ? Hakuna yeyote kati ya wale walio pewa aliko –hata mmoja wao- hakuna atakaye onja kwenye Karamu ya Arusi. Kwa nini ? Sababu wote wali yajali mambo yao wao wenyewe pahali pa ku mtumikia Bwana.

Hukumu ya Kondoo na Mbuzi

Moja kati ya mistari ya Neno la Mungu ambayo ina simama mbele yetu sote ni hukumu ya kondoo na mbuzi kama inavyo elezwa katika Matayo 25:31-46. Bwana ana wagawanya kwenda Jehanum ao Mbinguni si kufuatana na matendo ya kila mmoja binafsi ao si ku fuatana na kazi za ki dini ao si hata ku fuatana na jinsi kila mmoja alivyo ji hesabia kuwa haki binafsi. Tunakuta, Bwana ana wagawanya kwenda Jehanum ao Mbinguni ni kufuatana na moyo wa huruma walio u onyesha kuelekea wenye ku potea na wenye mahitaji.

Je ume walisha walio njaa kwa ku wapa Mkate wa Uzima ? Je ume wapa walio na kiu kunywa maji ya Uzima ? Je ume waleta wageni wapate nafasi katika Nyumba ya Bwana ? Je ume watembelea wale wanao fungwa katika vifungo vya dhambi ? Hapana ? Uliji ketia kwenye kanisa lako naku tumaini tu kuwa kwa njia moja ao nyingine wao wata jileta ndani ili waokolewe. Je uli fikiri kuwa wata kuja ku jitupia humo tu kwa ghafla na kwa kwa ku shtukia tu ? Je huku elewa kuwa kule kuto kutenda kwako pamoja na ku kosa

kwako moyo wa ukarimu wa kweli vita kuwa vitu vya ku wafungia mlango wasi ingie ?

"Na hawa wote wata elekea kwenye adhabu ya milele: bali wenye haki wata elekea kwenye uzima wa milele."

Na hapa kuna somo lengine linalo tunalo takiwa kuli chunga mioyoni: haitoshi kuwa Bwana hu hesabu ku pungukiwa rehema kama sababu yaku tosha ili ku kutupa wewe kwenye moto wa Jehanum, bali pia hu hesabia wale walio na moyo wa rehema kuwa elekea wengine ya kwamba ni wenye haki.

"huruma hujitukuza juu ya hukumu" Yakobo 2:13.

Lakini … "*Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi"*. Yakobo 4 :17.

Mfano wa Msamaria Mwema

Yesu ali kabiliana na mwana sheria aliye jaribu ku mu wekea mtego kwa njia ya ulizo ambalo kwa wakati wote ndilo swali la muhimu kuliko maswali mengine yote – Nifanye je, niweze kufika Mbinguni ? Mimi sitaki ni ungue kwenye moto wa Jehanum, hebu Yesu uni julishe siri ya ku uepuka. Sasa, tuna juwa sote jinsi gani wana sheria siku zote hutafuta mahali pa ku ji shikiliza ili kauli zao zishinde. Huyu jamaa ali fikiri kuwa angeli faulu ku mu tega Yesu kwa njia ya maneno ya sheria na mikataba ambayo ingeli leta kivuli juu uwazi wa Ujumbe wake Yeye. Halafu Yesu aka mjibu kwa njia ya Mfano wa Msamaria mwema.

Hebu uchukuwe mda mfupi pamoja nami, tuchunguze habari hii :

Hapa tuna mkuta mtu anaye toka Yerusalemu ku elekea Yeriko. Yerusalemu ndio mji unao patikana kwenye eneo la juu sana katika Israeli nzima, mji wa Mungu ; huku Yeriko ukiwa ndio mji unao patikana eneo la chini sana kando ya Bahari ya Chumvi na ni mji ambao Yoshua ali u laani, mji wa dhambi. Basi, picha hii ni mfano wa mtu anaye angukia dhambini na ana shambuliwa na Shetani naye ana achwa karibu mfu kando ya njia. Ana dondokwa na damu karibu kufa mavumbini, akifa katika dhambi zake.

Huku anatokea Kuhani. Mtu huyu kiongozi wa ki dini, anaye tazamiwa kuwa mtu wa Mungu na ambaye tunge mtazamia kuwa wa kwanza ku wanyoshea mkono wa huruma wale wanao potea na ku kuelekea kufa dhambini. Ila ana fanya nini ? Ana mu hepa kabisa-kabisa mtu huyu aliye karibu kufa ! «Hapana Jamani, huyu mwenye dhambi si angeli wahi kuja kanisani mbele ya hili kumupata na pale angeli weza ku sikia ujumbe wa Mchungaji na halafu si angeli weza ku okolewa. Ila sasa yeye huyu haku taka kuja na sasa huyu hapa anaenda zake kufa katika dhambi zake. Sawa, ni hili ndilo fungu alilo li chagua na sasa ita mu bidi abebe mateso ya matukio ya alilo lichangua» … na Mchungaji ana jiendea.

Na halafu anatokea Mlawi. Walawi wali kuwa wahudumu katika madhabau – kwa maneno mengine, walikuwa ndio watu wa kanisa wa ule wakati wao. Wale ambao ni Wakristo miongoni mwetu, tunakuwa aina ya Walawi. Na nini kafanya huyu Mkristo thabiti aliye nyooka aki

tembea shingo wima kwenye hii njia ? Ana tenda sawa sawa na alivyo tenda kuhani ! Ame vaa mavazi safi na mazuri sana yaliyo pigwa pasi, mavazi yake ya Jumapili na, sifa kwa Bwana ! yuko njiani kwenda kanisani. Kama aki kunjama na ku anza kumu okota huyu mwenye dhambi, mavazi yake mazuri na yaliyo safi yata chafuka yote kabisa na kupatwa na madoa ya damu, na halafu hata weza tena kuenda kwenye ibada. Ndiposa, ana muacha huyu afe hapo ndani ya uchafu. Labda huyu mwenye dhambi hata fikia kamwe kuokoka. Yeye ni mlevi tu, au kahaba, au aina nyingine ya mwenye dhambi mchafu tu.
Ni wa ngapi kati yetu ambao hawaja wahi ku fanya vivi hivi wakati tunapo nyoosha njia yetu, huku tume vaa vizuri sana tu wezavyo, tuki elekea kanisani ?

Halafu huyu hapa anakuja Msamaria mmoja, mtu wa tabaka ya chini sana katika Jamii ya Wayahudi, na yeye huyu, siyo tu kwamba ana simama, bali pia ana mimina divai na mafuta ili kuvi ponya vidonda vya huyu mtu. Divai ina wakilisha Roho wa Mungu na mafuta ina wakilisha upako wa Roho Mtakatifu. Huyu mtu ana mu ombea mwenye dhambi huyu pale pale alipo kwenye mavumbi ! Ndiposa ana mu chukua na ku mupeleka kanisani (kwa watunzao) ambako ana wa agiza wanao shugulika hapo wa hakikishe kuwa mtu huyu ana shugulikiwa vizuri … sababu yeye atarudi tena.

Na sasa, ulizo la ki musingi ni gani ?

Jambo hapa si swali la jinsi ya kuwa tu Mkristo ao swali la jinsi gani ya kujuwa ku tenda matendo mema – swali hapa lilikuwa kuhusu namna gani huyo aliye uliza apate ku ingia Mbinguni ! Kujuwa ni wapi wewe utakapo kuwa milele

yote haku tegemeye huduma gani unayo kanisani au namuna gani utu wako una onekana inje katika Ukristo. Jambo lote hilo linategemea huruma wewe ulio nayo kwa walio potea na walio karibu kufa. Ni kwako wewe kuchagua upande gani una taka kuwa, ila kwangu mimi, siku zangu zinapo fikia mwisho; sitaki kamwe ku elekea mahali pale ambapo Kuhani pamoja na yule Mlawi walipo imalizia safari yao.

"Uwaokoe wanao chukuliwa ili wauawe; na walio tayari ku chinjwa uwaopoe. Ukisema, Sisi hatukujua hayo; Je ! Yeye aipimaye mioyo siye afahamuye ? Naye ailindaye nafsi yako siye ajuaye ?" Je ! hatamlipa kila mtu sawasawa na kazi yake ? (Mithali 24:11-12).

Kipofu Bartimayo

Kuna sehemu nyingi za maandiko zinazo fanana na hii na ambazo nina zi tumia ninapo fundisha kuhusu uamusho. Mda hauruhusu tuzi rudilie zote, ila siku zote kuna ujumbe fulani ambao nina furahia ku malizia nao. Ni habari ya Kipofu Bartimayo.

Katika Marko 10, Yesu yuko akipita katika mji wa Yeriko na ana elekea Yerusalemu. Sasa yuko njiani kuelekea kifo Chake huko Kalvari. Na wakati anapo pita katika mji, watu wote wa mji wana kuja ili kukutana Naye. Ni wakati Yesu karibuni amefikia mwisho wa Huduma Yake halafu ameisha ku julikana na watu yakuwa Yeye ni nani, nao wame isha kusikia habari za matendo makuu Aliyo yafanya. Kila mmoja yupo hapo – Meya wa Mji, wanasiyasa, maaskofu na wachungaji, washiriki wote wa kanisa. Kila mmoja ana taka

kuwa angeli weza hata tu ku mu pamba jicho huyu jamaa ambaye wengi wana mu fikiria kuwa ndiye Masiya –Mpakwa mafuta wa Mungu.

Njiani kuna kipofu maskini anaye omba omba msaada anaye keti kando ya njia. Hebu sasa wewe uji weke kwa nafasi ya huyu mtu. Wewe ni kipofu, ume tupiliwa na jamii na una hesabiwa kuwa u mchafu. Hakuna yeyote anaye taka aku guse na yeyote anaye fanya hivyo hu hesabiwa naye kuwa ni mchafu. Tena hakuna mfuko au kasha ya fedha ya msaada iliyo wekwa kando na yeyote ili kukushugulikia, na hata familia yako ime ku tupilia. Ume achwa hapo uketi kando ya njia pamoja na uchafu wote wa wanyama wanao pita hapo. Una kumbwa na njaa, nawe una omba-omba upewe hata ngozi-ngozi zile zilizo achwa za mkate ili ziku wezeshe ku umaliza mchana. Na hayo ni madogo – shida kubwa ni kwamba huna tumaini lolote. Kesho nayo ita kuwa ni hivi hivi sawa na leo, na labda hata itakuwa mbaya zaidi. Daima uta kuwa u kipofu, mwenye njaa na mwenye ku tupiliwa.

Na halafu una sikia kama Yesu ata pitia ile ile njia. Huyu ni mtu aliye waponya vipofu macho yao. Amewaponya na wenye ukoma, na kufufua hata wafu, naye ana sema pamoja na mamlaka ya Mungu. Hii ndiyo bahati yako – bahati moja ya pekee maishani mwako ! Na sasa ana pita pale-pale mbele yako. Si una takiwa uguswe na Yesu !

Na halafu wewe unaanza kupaza sauti, "Yesu, Mwana wa Daudi ! Uni rehemu !" Lakini sasa wanamemba wa kanisa wana fanya nini wakati huo? Wana ku eleza ukae kimya. "Una muudhi Bwana". "Na wewe ni maskini muombaji mchafu aliye

laaniwa ! Una wezaje ku thubutu kupaza sauti !”

Hata hivyo Bartimayo ana paza sauti zaidi tena, “Yesu, uni rehemu”. Na Yesu ana simama. Ana waomba wamulete kwake na ana mu uliza, “una taka niku fanyie nini ?”

“Oh, Bwana wangu, Nataka kuona. Mimi naishi gizani, wala sioni. Nina hitaji Nuru ya Yesu Kristo. Nina hitaji ku okoka tokana na kifo hiki cha dhambi. Oh Yesu, okoa nafsi yangu !”

Wakati mmoja nilipo soma mambo haya, Bwana aka ni funulia kuwa, sababu ya ule umati wa watu ulio mu zunguuka Yesu, asingeli weza ku sikia kwa masikio yake sauti ya Bartimayo. Yesu alisikia sauti ya moyo wa huyu mtu kipofu. Jambo hilo ndilo lilimu pelekea Yesu kusimamisha safari yake.

Rafiki mpendwa, je waweza ku sikia sauti ya moyo wa mtu kipofu ? Sauti hii haitokei ndani ya vibambazi vya kanisa lenu. Ni sauti inayo sikika toka mitaani huko nje, toka kwake aliye maskini, aliye kipofu, mgonjwa, na kiwete – ni sauti inayo toka kwa wale ambao hawa shiriki kwenye kanisa lenu. Je sisi ni kama wale watu walio mzunguuka Yesu wakiwa na misimamo yao ya ki dini na ambao wana waeleza watu eti wa kae kimya ? Au je tuna weza ku vi sikia vilio vya mioyo yao.

Bwana tusamehe ! Tusamehe kuhusu kurizika kwetu kwa kuwa tuna ibada zetu kanisani. Tume sahau Wewe umetuokoa ili tu fanye nini. Tume lemewa na kuji tazama wenyewe kiasi kwamba tumeshindwa ku visikia vilio vya walio potea.

Habari nyingine moja ya mwisho

Najuwa kuwa tumekwisha ku chukua mda mrefu ku lifasiria jambo hili, ila naku omba uni ruhusu niku eleze mbele ya kumalizia maelezo haya; habari iliyo ni tokea miaka michache iliyo pita. Jioni moja nili kuwa kwenye maombi ya uamusho – labda niseme kuwa: hivyo ndivyo wao wali yaita yale maombi – ila kwa kweli mimi nili tambua kuwa wali kuwa waki ombea ni makazi yao, kuombea wachungaji wao, wagonjwa, vyombo vya musiki, … walikuwa waki ombea kila aina ya hitaji, kila kitu na kila aina ya watu isipo kuwa tu hawaku ombea wale walio dhambini na wanao elekea kupotea milele. Halafu nika jiuliza kwa nini wao walikosa ku ki ombea kitu cha muhimu zaidi ambacho kwa ajili ya hicho Mungu hu uleta Uamusho?

Na nilipo kuwa bado naketi hapo, Mungu aka nionyesha maono. Nili ona ulalo (kama mashua) kubwa liki jitokeza kwenye bahari. Ulalo huu ulikuwa na ukuu mara tatu kuliko upana wa ulalo (wa mashuwa) wa kawaida nalo lilikuwa lina jaa watu. Niliona ilikuwa siku nzuri yenye mwanga wa jua na hao watu walikua wame vaa mavazi mazuri yenye rangi za ku ngaa. Kila mmoja wao ali onekana kuwa na furaha na nili weza kuona furaha ya Bwana iki onekana kwenye nyuso zao. Ni watu walio kuwa wame okoka kweli na walikuwa waki mtukuza Yesu. Kila mmoja ali zunguuuka huku na kule na wali takiana baraka. Niliona wengi kati yao waki wawekea watu mikono na ku toa unabii kuhusu wale wanao wa wekea mikono yanayo husu mambo ya ajabu ajabu. Jambo nzuri la kutazama !

Na halafu, macho yangu yakaelekea mbali zaidi kui

angalia bahari iliyo wa zunguuka. Tofauti kubwa na zile rangi zenye ku ngaa nilizo kuwa nime ziona humo chomboni, bahari ili onekana yenye giza-giza na yenye baridi na yenye rangi kama ya ki majivu majivu – ili onekana kama kwamba ili kuwa na rangi nyeusi iliyo changanyika na rangi nyeupe. Maji yake yalionekana kuwa yana inuka na kushuka na yenye mawimbi -mawimbi yanayo vuma kila upande. Na halafu humo humo majini nika ona mamia ya watu wanao zama majini na wengine tayari kuanza ku shuka chini sana wakizama majini huku waki pepea mikono angani na ku lalamika ili wapate ku saidiwa tokana na jinsi mawimbi yalivyo kuwa yaki ji mwaga juu yao. Nili jaribu ku waita watu hao nilio kuwa nime waona wanatulia kando kando ndani ya merikebu ili waweze kuwa saidia hawa watu, wapate kuwa tupia vyombo vya ku kusiadia ku ogelea, au basi waji tupe kwenye maji na ku wakokotea kwenye chombo wasife. Ila hakuna aliye weza ku sikia sauti yangu.

Halafu nika tambua kuwa, si kwamba watu wale walio kuwa kwenye huo ulalo (wa mashua) hawaku wajali wale walio kuwa waki zama majini kando kando yao… shida ni kwamba hawakuwa na sikia sauti za hao wenye ku zama. Mambo ya kanisa lao ilikuwa ime wa jaa sana kiasi kwamba sauti walizo weza ku zi sikia ni zao wenyewe tu.

"Azibaye masikio yake asisikie kilio cha maskini, yeye naye atalia, lakini hata sikiwa" (Mithali 21: 13)

Wito wa Utakatifu wa mtu binafsi

Bila toba, hakuna uamusho. Kila kipindi cha uamusho

ambacho kili wahi ku tokea wakati wowote ule, kili tanguliwa kwaza na kipindi cha toba itokayo ndani ya mioyo iliyo pondeka inayo pelekea kwenye hali ya utakaso ndani ya kanisa. Mbele yaku uona utendaji wa Mungu kanisani, utendaji huu una takiwa uwe na msingi safi na mtakatifu ambako utasimama. Tuki taka ku uona utendaji wa kimungu, sherti dhambi zozote zi safishwe toka hekalu letu ili kuwe na nafasi kwa ajili ya Uwepo Wake. Mungu hawezi ku shirikiana na dhambi.

Toba ya namuna hii, haipaswi kuwa toba ya bandia. Haitakiwi wewe ku weza ku i nena tu kwa maneno ya kinywa sababu una fikiri kuwa ndivyo ulivyo paswa ku fanya. Inapaswa itoke ndani ya moyo, mububujiko wa toba itokayo ndani kabisa ya moyo. Mambo haya siyo mahitaji ya ki juu juu ya midomo tu tunayo yasukuma haraka haraka ku mu onyesha Mungu kwa ku ya fanya matengenezo ya haraka haraka kuhusu kitu fulani cha ujinga tulicho ki tenda. Hiki ni kilio cha ku omba msamaha, ambacho kamwe hatuku wahi kukipitia, na pamoja na hilo, kina bidi kiwe na uhakika ili sauti hii iweze kulifikia sikio la Mungu Mtakatifu.

Paulo ana tuonya katika Waebrania sura 10 ya kwamba hatu takiwi ku tosheka tu na hali ile tulio ipitia wakati ule tulio upokea wokovu mwanzoni. Maisha yetu yana takiwa yaonyeshe mwenendo wa ku tembea katika utakatifu mbele ya uso wa Mungu, na madhaifu yetu yana takiwa kuji onyesha tofauti, huku yaki jidhihirisha mbele ya nuru ya Ule Utakatifu. Ni haya makosa katika maisha yetu ambayo ni lazima yaletwe katika nuru ya hukumu na rehema za Mungu ili yaoshwe na ku samehewa kabla vyombo vyetu viweze ku wekwa tayari ili kutumiwa na Bwana.

"Basi, ndugu zangu nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumupendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mugeuzwe kwa ku fanywa upya nia zenu, mpate kujuwa hakika ya mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumu pendeza, na ukamilifu". Warumi 12:1-2

Hata aina ile ya dhambi ambayo kwa macho yetu yaonekana kana kwamba haina madhara, zina ji dhihirisha wazi kuwa mbaya pale ambapo zinapo simama ku linganishwa na mwanga wa utakatifu wa Bwana Mungu Mwenye Nguvu Zote. Jinsi ambavyo uwepo wa Mungu unavyo karibia zaidi na ndivyo dhambi hizi zaendelea ku dhihirika kuwa giza zaidi, hadi pale ile nuru kuu ipigayo upofu itapo angaza na kuweka wazi kila kona iliyo gizani ndani ya mioyo yetu. Hapo tuna fikia ku hisi uzito wa dhambi zetu uki lemea sana kiasi cha kuto kuji zuiya kushuka kwenye magoti katika hali ya maombi ya kuomba huruma kwa jinsi ya pekee ambayo kamwe hatuku wahi kuji nyenyekeza.

Nime wahi kuwaona Wakristo waki tetemeka bila kuweza kujizuia kwa ajili ya mambo ambayo siku moja mbeleni walikuwa wame yaona kuwa ni sehemu moja ya maisha yao ya kawaida tu. Ni Nuru kubwa sana kiasi kwamba hata sehemu ndogo sana iliyo na giza ita jidhihirisha kuwa iko tofauti. Wana jikuta kuwa haita wezekana kuvumiliya mambo hayo yaendeleye ku watenga na Mungu. Wana jisikia kuwa wana hatia sana na kujihisi kuhitaji kabisa ku tubu pamoja na sauti kuu ya kilio kitokacho moyo, hadi kufikia ku kiri kwa sauti kuu mbele ya kusanyiko lote kuhusu mambo ambayo kamwe hawaku wahi kuya chunguza mbeleni.

Katika kukiri kwa namna hii kuna kitu cha pekee kinacho safisha kiasi kwamba kina wajaza watu furaha yaku tulizwa ambayo ina ngaa kwenye nyuso zao. Kule ku vivunja vile vifungo vya siri vilivyo kuwa viki wafunga watu huleta aina ya uhuru amabao si wengi ambao wamesha wahi ku uonja, nao huji sikia kuwa kuna aina fulani ya uzito ambao una ondoka toka mabegani mwao na ambao wali kuwa wame ubeba tokea siku nyingi sana. Watu wana jisikia wame funguliwa! Ni hali inayo wafanya kusikia kwamba wangeli mu elezea kila wanaye muona habari hii na halafu hawa jali tena huyu ao yule ata fikiri nini kuwahusu. Wako huru!

Bila huo uhuru wa utakaso, Mungu hawezi ku tenda. Tusipo kuwa watakatifu, utendaji wa Mungu uta fifishwa na sakafu ya tope linalo funika mioyo yetu. Chini ya sheria ya Walawi, madhabau yalibidi ya takaswe kwanza kwa damu ili yawe yame wekwa takatifu vilivyo ili kuwekewa juu dhabihu anazo tolewa Bwana. Pale ambapo dhambi zote tayari zime safishwa toka kanisani na mavumbi yote ya kale ya uvuguvugu yame ondolewa toka madirishani, madhabau yatakuwa yame takaswa na hekalu litakuwa lime safishwa. Ni hapo sasa, na ni kwa wakati ule tu, ndio Mungu hu kaa kanisani kwa utimilifu wote wa utakatifu naye hutu andaa sisi kugeuzwa kuwa dhabihu zisizo zuilika zitolewazo kwa ajili yaku mu abudu Yeye.

Uhuru huo tokana na kila aina ya kivuli cha dhambi huleta ujasiri na nguvu mpya ya imani kwa waamini. Na hapo tuna weza sasa kuki sogelea Kiti cha Enzi cha Mungu tukiwa na ujasiri mpya wa haki katika Damu ya Yesu ili kuzishiriki ahadi za Mungu.

Na kwa kuwa wenye haki wana ujasiri kama simba, huu utakatifu halisi huinua sasa imani ya ki shujaa katika wa ume na wake walio na ujasiri mtakatifu ku elekea moja kwa moja hadi kunako Chumba cha Kiti cha Enzi ili ku omba wapewe haki zao, toka Kiti cha Enzi. Hawa si tena kondoo wanao woga wanao ogopa ku musumbua Bwana wao, ila ni askari wa Mungu wanao simama katika usafi na kuzishika pembe za madhabau ili ku zidai ahadi za Mungu. Kamwe hawa ondoki hapo mpaka Mungu anapo tenda.

Utakatifu wa hali ya juu huleta ujasiri wa hali ya juu – hadi ku fikia ule ujasiri wa ku ingia kwenye Chumba cha Kiti cha Enzi cha Mungu pamoja na migurumo ya sauti za askari wa imani. Hii ndio aina ya imani ambayo humu pendeza Mungu na hu mpelekea ku toa majibu. Mungu hu baki mwaminifu kwa Ahadi anazo zitoa Mwenyewe katika Neno Lake ili kujibu kwa maombi ya aina hii yanayo tolewa ili ku uomba Uamusho. SHERTI Mungu ata jibu kutokana na uaminifu wake mkubwa. Wanaume na wanawake ambao tayari wamesha wahi kufikia kwenye ngazi hii ya imani wanajuwa ukweli huu usio weza ku kanushwa.

Kutubu huleta utakaso, na utakaso hu iacha huru imani, na imani hu hamisha milima. Pale twaweza ku simama mbele za Mungu na ku udai utimilifu wa ahadi Zake, hali tukijuwa kuwa; sababu tume takaswa mbele zake, ita mu bidi Yeye atujibu.

Uamusho unakuja. Tuna fahamu hivyo. Tuna uhitaji. Kwa sasa tunayo imani ili kuamini kuwa ata uleta. Nao unakuja.

Haki hudhibitisha ahadi za Mungu.

TOBA YA PAMOJA

Toba ya kila mtu binafsi ndio inayo ujenga msingi ili hatua nyingine ifuate, nayo ni hatua ya toba ya kundi. Kwa njia ya ule uwazi unao tokana na uhusiano ulio fanywa upya kati ya mtu binafsi na Mungu, itakuwa ni rahisi kutambua umbali gani maanguko yetu yame tufikisha. Sasa tuna tambua kwa kiasi gani, sio sisi wenyewe binafsi, ila pia jinsi ambavyo taifa letu lote nzima, jinsi ambavyo makanisa yetu yote pamoja, na jinsi ambavyo ndugu na dada zetu tume jitenga na Mungu. Mambo ambayo mbeleni yali onekana yapo sawa au tuseme yaliyo onekana kuwa yawezayo ku kubalika, sasa yaanza ku onekana yenye kivuli cha giza ambayo ina jidhihirisha kupitiya nuru ya mwanga Wake. Hapo tuna anza kuji uliza ime kuwaje hata tusingeli weza ku tambua hali hii mbeleni, lakini ni kwa sababu macho yetu yalizoea mwanga finyu (uliyo fifia) makanisani mwetu.

Tuki utaka Uamusho utakao pita na kwenda mbali zaidi ya jengo la makanisa yetu, tunatakiwa kumu sihii Mungu alete ule ule msamaha juu ya inchi yetu yote. Kivuli cha ku iacha imani ya kweli kime jitanda juu ya taifa letu nzima kama wingu jeusi, na ina tubidi ku omba kwa ajili ya msamaha wa Mungu juu yetu sote.

Ufunguo hapa, kwanza ni ku tambua kuwa majirani wetu, wanainchi wenzetu, washirika wenzetu tunao shiriki nao makanisani kwa bidii tuki hudhuria yale ambayo tunayo yaona sasa kama ni mikutano vuguvugu ya kidini, ku tambua

kuwa hawa nao wapo katika hali ile ile ambamo nasi tulimo kuwemo mbeleni. Ku usikia ule mzigo wetu kuhusu wanao potea sherti uanzie hapo. Mioyo yetu ina bidi ivunjike kwa huruma tokana na wale wanao teswa chini ya ile hema ya kutokuwa na imani ya kweli, na ambako sisi tume bahatika ku ponyoka hivi karibuni tu.

Yesu ali muita Lazaro aondoke inje ya kaburi, ila Ali waalika wanafunzi wake wamu fungue toka yale mavazi mafu ya tamaduni za kale za kidini. Ndivyo nasi tunavyo alikwa kutoa duwa la kuliombea Kanisa. Na tukiona mbali kuliko tofauti za majina ya mashirika ya kikanisa, ina tubidi ku ombeana kila mmoja aki muombea mwengine. Hukumu ita anzia katika nyumba ya Mungu, na vivi hivi pia ndivyo ina takiwa maombi ya kuiomba rehema ya Mungu ianze kuiombea kwanza, nyumba ya Mungu.

Danieli

«Katika mwaka wa kwanza wa ku miliki kwake, mimi Danieli, kwa ku visoma vitabu, nalifahamu hesabu ya miaka, ambayo neno la Bwana lilimjia Yeremia nabii, ya ku utimiza ukiwa wa Yerusalema, yaani miaka sabini. Nika mwelekezea Bwana Mungu uso wangu, ili kutaka kwa maombi na dua, pamoja na ku funga, na kuvaa nguo za magunia na majivu».
Danieli 9 :2 ,3.

Katika Biblia, habari ya kujengwa upya kwa mji wa Yerusalemu ni mmoja kati ya maelezo yaliyo makuu zaidi na tena yenye kufasiri kwa unaga ubaga kuhusu uamusho. Hapa hatuna nafasi kubwa ili tu rudilie jinsi taifa la Israeli lilifikia ku anguka, jinsi nabii walivyo lililia mbele za Mungu na pia

kuhusu hukumu za Mungu. Ila katika kila hukumu Mungu anayo itowa tunakuta ndani mukiwemo mbegu ya uamusho utakao ifuata. Na Danieli yeye alikuwa moja kati ya zile mbegu, sawa sawa na alivyo kuwa Isaya ambaye ali changia ili mfalme Sairas atoe tangazo ; sawa sawa na Estha aliye mu tia moyo mfalme Dario ili aidhibitishe ; sawa sawa pia na Nehemia, na Ezra na wengine. Unabii uli tolewa, matayarisho yali fanyizwa, ila ni Danieli ndiye alikuwa ame liombea jambo hilo.

Unapo soma kuhusu jambo fulani moja kwa moja toka kwenye Neno la Mungu, hebu fahamu kuwa hilo ni kweli – lime andikwa ; Mungu ame linena ; nalo sherti lita timia. Danieli ali soma katika kitabu cha Yeremia kuwa Kushikiliwa kwao mateka kule Babeli kuta dumu kwa mda wa miaka 70 na baadaye Mungu alikuwa amepanga ku usimamisha tena ufalme wa Israeli, pa Yerusalemu. Wana wa Israeli walikuwa wamepotoka mbali na haki ya Mungu nayo matokeo ya huo uasi wao yakawa kwamba walienda utumwani, ila pamoja na hayo rehema za Mungu zili funuliwa kwao kwa njia ya ajabu ! Miaka 70 ilikuwa karibu kumalizika naye Danieli ali fahamu kuwa wakati wa marejeo ulikuwa ume fika.

Ingawa kama tayari ilikuwa ime andikwa katika Neno la Mungu na tayari wakati wa marejeo ulikuwa umewadia, je Danieli ali waita rafiki zake ili waanze ku imba na ku furahi ? Je wali anza ku sherekea kuhusu tumaini hili jipya la marudilio ? Hapana, Danieli alikuwa mmoja kati ya wenye hekima ya juu zaidi ambao wamewahi ku ishi, na ali fahamu kuwa pasipo toba haiwezikane kuwepo na Uamusho.

Ili kushiriki mwito huu wa ajabu wa kuirudilia Neema

ya Mungu, toba ilibidi itafutwe, na siyo tu kwa kila mtu binafsi, ila kwa watu wa Mungu hao wote kwa jumla. Kuli takiwa kuwe na mtu ashukaye chini kwenye magoti, na Danieli akawa ndiye huyo. Maombi yaliyo marefu kuliko yote katika Agano la Kale ndiyo hayo maombi ya Danieli kwa ajili ya ku samehewa kwa watu wa kwao.

E.M. Bounds ame wahi kuandika kuwa Mungu hatatenda chochote bila maombi ambacho awezacho kukitenda pamoja na maombi. Na ni kweli. Mungu aweza ku litenda moja kwa moja… ila halitendi. Hutumia watu wenye mwili. Sisi ndio mwili Wake, mikono na miguu ya Injili. Ni maombi yetu ndio yanayo ifanya mikono Yake ku funguka ili ku tenda na ni imani yetu ndio inayo hamisha milima. Hii ni sehemu ya mpango alio upanga Yeye Mwenyewe ili sisi tuwe vyombo vya rehema Zake na tu ufuate mfano wa Mwanawe Yesu Kristo.

Jinsi tunavyo utafuta uso wa Mungu katika ku tubu kwetu kwa ajili ya watu wetu, tuna iondoa laana na ku ufungua mlango ili marejeo yaanze.

Nehemiah

Nehemia naye pia ali ufahamu ukweli huu. Ali lia alipo pata habari jinsi ambavyo mji wa Yerusalemu ume haribiwa na kubaki mabomoko. Mji uli stahili kujengwa, kusimama hali uki pendeza kama Mnara wa Utukufu wa Mungu. Lakini sasa uli kuwa ume haribiwa sababu ya dhambi za walio kuwa wakaaji wake, watu wa Mungu. Moyo wa Nehemiah uli vunjika.

Yeye kama munweshaji wa mfame, alikuwa na ruhusa ya kuingia mbele ya Yule aliye kuwa na uwezo wa ku amuru mji ujengwe upya, ila pia ali fahamu kuwa pasipo yeye ku tubu mbele za Mungu kwa ajili ya dhambi za watu ambazo ndizo zilizo pelekea mji kubomolewa, ombi lolote awezalo kulitoa lita kuwa kufanya kazi bure. Usiku na mchana , Nehemia ali funga na ku omba Mungu aweze ku wa samehe watu wake na kwamba amupe kibali wakati huo alipo lileta hitaji lake mbele ya mfalme.

Haya ni maombi halisi – kufunga usiku na mchana, siku nzima mwanzo hadi mwisho pamoja na kiuu kikubwa cha kupata jibu toka kwa Mungu. Kuna nyakati ambazo hutakiwi kubakilia kwenye hatua ya «labda Mungu ata tenda ». Ukiwemo katika hali ambamo inabidi – hakika inabidi kabisa upokee jibu toka Mungu, hapo utaweka pembeni damu na nyama na kila kitu kingine kiwezacho kuwa kizuiyo katika njia na kuji weka wewe mwenyewe mbele Yake yeye awezaye ku kufungua na halafu utaketi hapo mpaka jibu lifike. Nehemia alijua jambo hili, na ali lihitaji jibu kwa ajili ya ndugu zake walio endelea ku angamia katika hali ya utumwa. Hapakuwepo na suluhisho lengine.

Sisi nasi ni wanyweshaji wa Mfalme, na tuna keti katika hali ya utumwa katika inchi ya wapagani hali Kanisa likiwa katika hali ya mabomoko ya kiroho. Kuta za wokovu zimebomolewa na hekalu kwa ajili ya Roho Mtakatifu lime haribiwa hali likili acha Kanisa bila vifaa vya kuji linda dhidi ya adui. Kama Nehemia na Danieli, lazima tutambue chanzo cha hali yetu ya sasa na tumulilie Mungu ili ali samehe taifa na pia makanisa yetu.

Tusipo shugulikia hali hii, Mungu ata geuzaje hukumu zake ? Tusipo kiri kuhusu hali ilivyo pamoja na mioyo iliyo wazi kukiri jinsi mambo yalivyo kwa mioyo iliyo pondeka, hali yetu haita boreka kuliko jinsi tulivyo kuwa mbeleni, na watu wetu watarudilia haraka sana hali zao zile zile za kidini ambamo walikuwa mbeleni.

Huu ndio mtiani wa moyo wa Mkristo. Je kweli tuna huzunikia dhambi zetu ? Je twaomboleza na kuingia katika hali ya machozi kwa ajili ya ku mrudia Mungu kiasi cha kuwa tayari kuomba na ku funga usiku na mchana ? Je tuna sononeka kwa ajili ya dhambi na ma anguko ya watu wetu na kumu paziya Mungu sauti kwa mioyo yetu yote ili Yeye mwenyewe awa rehemu watu wake ? Hali tuki juwa kuwa hukumu ya Mungu iko, twajuwa pia kuwa rehema Zake zipo pia ikiwa mioyo yetu ina jiweka wazi, na kwamba tuna weza ku igeuza gadhabu yake Mungu kwa njia ya toba itakayo penya hadi mbingu juu na kukifikia kiti Chake cha Enzi.

Lakini, maombi toka mioyo iliyo gawanyika nusu na nusu hayawezi ku tenda hilo. Yeye hawezi kukijaza chombo ambacho kwanza hakiku wekwa wazi kwa njia ya toba.

Eliya

Eliya aliwahi ku kabiliana na ukuta wa jiwe la kundi la mioyo ya watu wasiojali kutubu, huko juu ya mlima wa Karmeli. Aliitwa na Mungu kumtumikia katika wakati ulio jawa na watu wenye hali kama hiyo. Hali kukiwepo na mashamba yenye rangi mbichi kabisa na huku akiiona upande wote mito inayo tiririsha maji kwa uwingi, ali simama mbele ya mfalme na ku tangaza kuwa hakuta nyesha tena mvua yoyote. Kila

aliye kuwa hapo alimu chekea na ku mu dhihaki, lakini miaka mitatu baadaye, hakuna aliyekuwa aki dhubutu kuendelea ku cheka. Kuenea kwa ukame kuli zihirisha ukiwa wa kiroho ambamo taifa lilikuwa lime ingia, ila wote wali fikiri kuwa hilo lilitokana na kosa la nabii huyo wala silo kosa lao wao. Jinsi gani ilivyo vigumu kwetu ku tambua hali yetu ya kurudi nyuma! Na jinsi gani ilivyo rahisi kuwalaumu wale ambao Bwana huwainua ili kuutangaza ujumbe wa toba!

Eliya aliitisha watu kwenye onyesho la mwisho kati yake yeye na mpangilio wa kidini uliokuwepo wakati ule. Manabii wengine wote wa Mungu walikuwa wame uawa, isipokuwa sehemu ndogo kati yao ambao walikuwa mafichoni. Na hapa palikuwa sasa pame simama makuhani pamoja na manabii 850 wa Baali wanao jipanga dhidi ya nabii mmoja pekee wa Mungu.

Israeli ilikuwa ni inchi ndogo na isiyo na miji mikuu mingi, na hii ina maanisha kuwa hesabu kubwa kiasi hiki ya ma nabii wa Baali wali takiwa wawe walikuwa ndio viongozi wa makanisa ya mahali toka kila jiji ndogo la inchi ya Israeli. Hapa walikuweko yule baba aliye ibarikia ndoa ya mabinti na ya wana wako, yule baba aliye wahi ku wabatiza watoto wako, au wale wa baba ambao ni viongozi wa makanisa yenu ya mahali. Na ulikuwa una wa juwa kila mmoja kwa jina lake. Walikuwa ndio waongozi wa watu. Lakini walikuwa wame kubaliana na kujiunga na dini ya uongo ya wakati ule. Na wao hawaku dhani kuwa wao wame mukosea Mungu. Kwa hakika walidhani kuwa Mungu ange wasikiliza na kutuma moto ushuke ili wamu onyeshe huyu nabii mzee apendaye kuwa hukumu wengine kwamba ni wao ndio walio kuwa wakitembea sawa na mapenzi ya Mungu… na ni vivi hivi

wafanyavyo hata leo hii.

Ila Eliya yeye ali fahamu kuwa wakati sasa ume fika ili Mungu ajidhihirishe kuwa Yeye ni Mwenye Haki. Ila moto ulipo shuka, je uli uleta uamusho katika watu ? Siyo kabisa. Ingawa kama wali paza sauti "Bwana, ndiye Mungu, Bwana ndiye Mungu!", ku kiri hakuja maanisha ku tubu. Wali kuwa tayari ku simama hapo wakati ule ambao wachungaji wao wa mahali walipo kuwa waki uawa katika tendo la usafisaji huko kwenye kijito cha Kishoni, ila hawakuwa tayari ku anguka kwenye magoti pamoja na huzuni ya mioyo iliyo pondeka tokana na dhabi zao. Walijiona kuhusika zaidi na maisha yao binafsi pahali pa ku jihusisha na maisha ya Kanisa lao. Hapaku kuwepo na toba ya kundi ili ku uregeza ule udongo mgumu wa lile taifa.

Eliya hakuwa na uamusho, na vivi hivi Elisha naye pia, aliye kuja nyuma yake. Ina bidi kuwepo na toba ya kundi ili kundi liamushwe kama mwili mmoja, na hilo hali fiki isipokuwa baada ya miaka ifuatayo. Hata kama nabii huyu alikuwa mtumishi mwaminifu wa Mungu, udongo wa Israeli haukuwa ume regea ili kuipokea mbegu, na halafu isinge wezekana kuwe na mavuno yawezayo ku inuka na ku mea toka huo udongo mkavu na mgumu.

Wapo wapi watu kama Eliya wenye ujasiri leo? Tumezoeya sana mipangilio ya dini inayo tawala maeneo yetu ya kwamba yeyote asimamaye kuwa tangazia kuwa wao tayari wame potoka hu kataliwa eti yeye ni mushabiki wa mawazo yake pekee, naye ni mwenye kupenda tu kuwahukumu hukumu wengine kuipita kiasi. Leo hii, sawa sawa na ilivyo kuwa kwa wakati ule wa Eliya, ujumbe unao husu hofu ya Mungu una chukuliwa kuwa wa kuwagawanya

watu, wakati ambapo ujumbe unao simamia pande zote mbili kuhusu upendo bila utakatifu unachukuliwa kama ndio mzuri na ndio ulio wa kimungu. Tumechagua njia za ki uzembe ila wale manabii wa Mungu wao walikubali ku hatarisha maisha yao.

Kwa nini macho yetu yamepofuka kuhusu mambo ya kiroho? Kwa nini ime kuwa vigumu kwetu kuwa na mioyo iliyo pondeka kiasi cha kuto kuhitaji chochote isipo kuwa taifa letu kumurudiya Mungu, isipo kuwa ku fikia kiasi cha ile toba ya mioyo iliyo pondeka anayo itaka Mungu? Nia hii iki changanywa tu na uadui pamoja na mateso vita tuletea huzuni. Kwa namuna fulani, inabidi katika kuchanganyika huku kuwemo na kiu cha utakaso, na hamu kuu ya jambo fulani linalo zidia kile ambacho dunia hii yaweza kututolea katika starehe na mafanikio ya aina yake. Kwa kweli, nina amini kuwa watu hao pale juu ya mlima wa Karmeli wali tawaliwa hasa na nia ya kuya rudiliya maisha yao ya mafanikio, kuliko ku urudilia utakatifu. Mioyo yao haikuwa ime pondeka tokana na dhambi zao – ni kama walikuwa tu wamefikia, kwa shida, hatua ya kuyatambua makosa yao.

Kuna aina mbili ya ulimwengu wa mambo. Ule tunao uona, na pia ule wa Umilele. Kwa kiwango ambacho tuna zama ndani ya mmoja, ndivyo kadiri tunavyo pungukiwa kuji tambua katika ule mwengine. Wakati wowote ambao bado kiu cha utakatifu hakija inuka ndani ya mioyo yetu, starehe za ulimwengu huu hupofusha macho yetu isione mbali kuliko maisha haya tulio nayo. Kitabu cha Mithali kina tuonya: “pasipo na maono, taifa hu angamia”. Tunatakiwa kuwa na macho yawezayo kuona mbali kuliko Mlima wa Karmeli na kuweza kuona inchi tambarare ya Beulah iliyo mbali na hapa

tulipo na tuwe na shauku ya hiyo kama ndiyo makao yetu pekee. Ni pale tu tunapo yavusha macho yetu ku vuka pazia ya dunia hii ili ku shika kiini cha mambo yatarajiwayo, ndipo tu tuwezapo ku (relinquish) kushikamana kwetu na mambo ya mwili.

Nia ya utakatifu hufunua hitaji letu kwa ajili ya toba, siyo tu toba yetu sisi wenyewe, bali pia toba ya watu wetu, ya taifa letu, na ya makanisa yetu. Tunapo fikia hatua hiyo, tuta uvunja kwa hiari, ugumu ule wa ardhi ya mioyo yetu ili kuipanda mbegu ya uamusho. Jambo hili lahitaji mda na tena moyo ulio kusudia kuwa hauta toshelezwa na chochote kingine kile cha tofauti bila kujali kuwa mda ungeli pita kiasi gani. Na hakuna chochote cha ku chukuwa nafasi ya hilo, bila kujali kiasi gani kanisa laonekana kuwa nzuri. Isipo kuwa tu halisi unao toka kwenye madhabau ya Mungu ndio uwezao kutosheleza matazamio na kiu ambacho Mungu amekiweka ndani ya mioyo ya Watumishi wake.

Hii ndiyo sababu iliyo mupelekea Nahemia ku omba kwa bidii sana – alitaka auone uamusho halisi. Hii ndiyo sababu iliyo mupelekea Eliya ku kubali ku hatarisha maisha yake, ndiyo sababu iliyo mu fanya Danieli kushuka kwenye magoti; na ndio sababu wale ambao huguswa na kilio cha Rakeli “Nipe mutoto ao nife” hu jitoa kwa njia ya kufunga na kuomba hadi Mungu atakapo jibu.

Uamusho hauwezi kutokea hadi hapo rehema inapo patikana.

4. HATUA YA INNE – KUPIGA VITA VYA MAOMBI

"*Tena hapo mtakapo kwenda kupigana vita katika inchi yenu kupigana na adui awaoneaye ninyi, ndipo mtakapo piga sauti ya kugutusha kwa tarumbeta, nanyi mta kumbukwa mbele za Bwana Mungu wenu, nanyi mtaokolewa na adui zenu*" Hesabu 10: 9

"*Pigeni tarumbeta katika Sayuni, pigeni na kelele katika mlima wangu mtakatifu wenyeji wote wa inchi na watetemeke maana siku ya Bwana inakuja. Kwa sababu inakaribia*" Yoeli 2:1

Tarumbeta mbili za fedha zilitumiwa ili kuliita kusanyiko pamoja. Wakati tarumbeta hizi zilipo tumiwa ili ku toa onyo la tahadhari, zili wakusanya watu wa Mungu ili waingie vitani. Sisi nasi tume itwa ili tuingie vitani, na silaha ambazo Mungu anazowapa Wakristo zina uwezo wa kuweza ku angusha chini kila kitu kiji inuacho dhidi ya maarifa ya Mungu. Paulo ana tueleza kuwa Neno la Mungu ndio upanga wetu, Haki ndio dirii yetu, Wokovu ndio Kofia yetu, na Imani ndio Ngao yetu. Sisi tume itwa kama mashujaa wa imani ili tuingie vitani kuvipiga vita vizuri vya imani. Mzozo kati ya Nuru na Giza ndicho kiini kikuu cha vita tangu wakati wa Kitabu cha Mwanzo hadi kufikia kile cha Ufunuo, na huo ndio unao funua wazi jinsi tulivyo itwa kuwa askari wa Bwana wa majeshi. Tupo vitani, nasi hatuta pumuzishwa hadi tutakapo fikia mauti.

Hatuwezi tukawe wapiganaji wa kweli ikiwa hatuna kile ambacho tunakipigania ili tukipate. Mioyo yetu haita jitolea, nasi hatuta kuwa na uamuzi usio tikiswa; ujasiri na kukata

kwetu shauri la kujitoa waviwezi ku simama isipo kuwa sisi kufikia kukusudia kuto kujali hasara ya chochote kile kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Jambo hili haliwezi ku fikiwa na kanisa ambalo bado halija fikia hatua tatu za mwanzoni ambazo ni kujitambua, kutaka uamusho na kutubu. Ni pale tu tunapo kuwa tayari tume pitia vipindi hivi, ndipo tunapo fikia kuwa tayari ku pigana hadi kifo kwa ajili ya kweli ya Mungu.

Naye Mungu anaita :

"*Pigeni tarumbeta katika Sayuni, Takaseni saumu, kusanyeni kusanyiko kuu; Kusanyeni watu, litakaseni kusanyiko, Kusanyeni wazee, kusanyeni , na hao wanyonyao maziwa; Bwana arusi na atoke chumbani mwake, na bibi arusi katika hema yake; Hao makuhani, wahudumu wa BWANA, na walie Kati ya patakatifu ma madhabau; Na waseme, Uwaachilie watu wako, Ee BWANA, Wala usiutoe urithi wako upate aibu, Hata mataifa watawale juu yao; Kwani waseme kati ya watu, Yuko wapi Mungu wao ?*

Hapo ndipo BWANA alipoona wivu kwa ajili ya inchi yake, akawahurumia watu wake. BWANA akajibu, aka waambia watu wake; Tazameni, nitawaletea nafaka, na divai, na mafuta, nanyi mtashiba kwa vitu hivyo; wala sitawafanya tena kuwa aibu kati ya mataifa". Yoeli 2:15-19.

Huo ni mwaliko wa maombi halisi. Si mwito wa maombi kwa ajili ya mguu unao uma, maombi kwa ajili ya kupata kazi nyipya, au maombi ili tupate pesa (« nipe ! nipe ! nipe !). Huu ni mwito wa ku furika hadi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu ili ku uona uamusho wa inchi nzima. Ni kuachana na mitazamo ya ki juu-juu iliyo ya kidunia hii, na ku achana

na kule kutosheka na « kuingia na kutoka : ibada za kanisani za kawaida ». Huu ni mwaliko wa kuingia kwenye mapambano.

Watu walio kwenye jeshi ambalo Yoeli ana li eleza kwenye sura ya 2 husema na kutenda bila kuona haya, maneno yao ni magumu na tena yana kwaruza, nao hawa hafikiani ; wao ni tofauti kabisa na wale tunao waona kwenye viti vya makanisa yetu leo. Hawajali kitu chochote kati ya yale dunia inayo yatoa, na hawana hofu ya kujiuliza ni akina nani wanao kwazika tokana na ujumbe wao mkali wa kuwaalika watu kuwa na moyo wa toba. Moto wao umewashwa moja kwa moja toka Madhabau ya Mungu na hauta zimika kamwe hata Yeye atakapo rudi. Hakuna kitakacho wazuiya. Bwana ame waweka kazini Naye huwa ongoza kwa sauti Yake kuendelea mbele, nao hutangaza ujio wa Bwana kwa nguvu na mamulaka ya Utashi wake mkuu.

Je hii ndiyo aina ya ujumbe tunao usikia kwenye mimbari yetu au kwenye televisheni leo ? Hii siyo aina hiyo ya Injili «nyororo sana, ya ki utaratibu sana» ambayo wachungaji wetu hutulisha nayo. Huu ni ule wivu wa Mungu unao waka ndani yetu kiasi cha ku wa chapa fimbo wabadilishao pesa hekaluni. Wivu kama huo hauwezi ku dumu kwa urahisi ndani ya kanisa la ukawaida sababu hauta pata mahali pa ku simamia ili ku dumu hapo. Ni moto ulio kusudiwa kuchoma makapi ili kuitakasa inchi.

Aina hii ya vita vikali vya kujitolea huanzishwa na aina hiyo hiyo ya maombi ; maombi makali ya kujitolea. Maombi ya urahisi ya «nyakati za utulivu» hayata pamba moto vya kutosha ili kuuwasha huu moto. Ku «zungumza kwa

machache tu na Yesu» hakuta ipelekea ile milango ya Chumba cha Enzi ku funguka ili kuli anzisha jeshi la aina hii. Hili ni jambo linalo yahitaji maombi yalio na nguvu, maombi yenye bidii yanayo tolewa na wapiga vita walio tayari ku ugua kwa machozi na kulia kwa machozi ili ku itikisa misingi ya kuta za mbingu ili kuuona utendaji wa Mungu. Hii ni hiyo aina ya imani isemayo «hakuna atakaye niondosha kwenye msimamo, hakuna atakaye ni katalia, na kamwe sita kata tamaa. Nita shika pembe za madhabau na ku zidai ahadi za Mungu mpaka nizione Mbingu zikitenda, na dunia iki tikisika sababu Mungu ana umwaga uamusho !

Kabla ya sisi kuzi chukuwa silaha na ku kimbia kuelekea mitaani huku tukivaliya mavazi ya mapambano ya kujikinga, lazima tuelewe kuwa ushindi katika mapambano haupatikani huko kwenye mitaa isipokuwa kwanza tumeupata huo ushindi katika chumba cha maombi. Na haitoshi tu yawe maombi ila inabidi yawe maombi yaushindani yanayo dumu hadi kulifikia jibu. Uweza katika Mungu hutokana na ushindi ulio patikana kwa juhudi ngumu toka kwenye chumba cha maombi, na pasipo ule uweza, hatuna chochote tunacho weza kukionyesha walio potea isipokuwa uadilifu wa kimwili unao pungukiwa na Roho wa Mungu. Tukitaka tuuone utendaji toka Mungu, sherti kwanza tumu tikise Mungu. Mwili haulete faida yoyote. Musemaji aliye mashuhuri kuliko wote dunia nzima anaweza tu kuzi fanya akili za watu kuyakubali maneno yake, ila ni Roho wa Mungu pekee ndiye awezaye ku igusa mioyo.

Unaweza ukawe na ndoano na mshipi wa ku opowa samaki ulio bora zaidi ya mishipi yote duniani na pamoja na chambo (chakula cha ku tegea) kilicho kizuri kuliko chochote, ila ikiwa samaki hawana njaa, kamwe hawata ikaribia hiyo

ndoano yako ili kula kile chambo. Kabla ya sisi kukutana na nafsi zilizo tayari Maombi yanahitajika ili Roho wa Mungu uzushe njaa ya Kuijuwa Kweli ya Mungu ndani ya mioyo yao. Tuki jaribu ku kimbia tu huku tukisukumwa na bidii yetu pekee na isiyo lindwa salama kwa njia ya maombi hatuwezi kufanikisha lolote.

Mashujaa wale wa maombi wa zama za kale wali eleza mara nyingi jinsi ambavyo wao walivyo «liombea jambo hili» - na waka endelea kabisa kabisa kuliombea – hadi hapo walipo pata jibu toka Mungu. Kuna nafasi fulani ambapo katika utaratibu wetu wa kuyashugulikia mambo kwa mtindo wa ki sasa, tumeupoteza ule uweza wa ku gonga kwa nguvu kwenye Milango ya Mbingu. Tunasema kuwa tuna imani, ila imani siyo kuamini kuwa Mungu anao uweza wa kutenda lolote. Mpumbavu yeyeote anaweza ku amini hilo. Imani ya kweli ni kuamini kuwa ata tenda, na kwamba huta acha kuomba mpaka pale atakapo tenda ! Chochote kile kilicho tofauti na hili: siyo imani, ila madhanio. Lakini je, leo hii tuna iona wapi aina hii ya imani ? Imesha sahaulika ile mikutano ya maombi-ya-usiku-kutwa ambako watu waliomba usiku kutwa hadi mapambazuko kwa ajili ya nafsi zilizo potea. Kupaza sauti pamoja na kiu kikubwa kama alivyo fanya Rakeli kumegeuka kuwa ni minunguno mitupu. Wakati wowote ule ambao bado tuta kuwa hatuja fikia kiwango kile cha kujitolea bila kugeuka nyuma, bado hatuta pata ule msukumo na nguvu ya ku tupeleka mbele.

Tume ziruhusu starehe zetu kuiyeyusha ile huruma yetu kubwa kwa ajili ya nafsi za wanao potea, na matokeo yake ni kwamba tume liondolea Kanisa nguvu zake za kiuume. Tuna omba kama wanawake, sio kama askari wa vita

(au labda niseme ni kama wasichana wadogo, kwa sababu kati ya wanawake, kuna wale wanao unda jeshi la askari wa maombi wenye nguvu kiasi cha kutuacha sisi ku aibika). Mungu ametuita kama ma askari na tuna takiwa ku omba pamoja na ushujaa wa ki askari ili kuvi vunja vibambazi vyote vya ki mapepo, kuvipasua wazi vizuizi vyote vya ki roho, na kupambana ili ku uona uamusho ambao tuna utazamia kwa kiu kikubwa unasimama.

Kabla Bwana haja jibu, Yoeli analialika Kanisa kujitakasa na kujitolea kusio na masito kwa ajili ya maombi. Hili ni jambo liwezalo kufanywa na wale tu walio na kiu kikuu cha ku uona utendaji wa Mungu. Hakuna chochote kiwezacho kuwa tosheleza isipokuwa ku uona uamusho uki enea inchi nzima. Hili ndilo Mungu alilo liweka ndani yao. Nalo haliwashwi kama kidude cha ku uwashia umeme, ila hutakaswa kupitia moto wa mpangilio mzima unao zichoma nia na shauku zingine zote. Bila kujali jambo lingine lolote. «Nipe kuzivuta nafsi zisizo kujuwa bado, na kama sivyo nife !»

Ni pale tunapo fikia kiasi hiki ndipo Mungu husikia kilio chetu naye hu jibu. Kwa habari ya wana wa Israeli huko Misri, ilichukuwa zaidi ya miaka 400 ili wafikiye kukata tamaa kuji husu wenyewe ili waweze kumulilia Mungu. Na walipo fikia kiwango hicho, mbinguni alipo Mungu aka yasikia maombi yao na aka watumia Mukombozi. Na sisi, itatuchukuwa mda gani ili kufikia kiasi hiki cha kiu iliyo kuu sana kiasi kwamba isi weze tena ku ngojea ?

Tuki mulilia jinsi ile ile walivyo mmilia, Yeye atatusikia.

III. Jinsi ya Ku ufanya moto uwake

Ni rahisi kutoa toa maneno yanayo kuwa yana sauti nzuri na yanayo zungumzia malengo mazuri, ila bila kuwa na fikara zinazo elewa wazi vya kutosha jinsi gani malengo haya yatakavyo fikiwa, tuna baki tuki tanga-tanga bila muelekeo. Katika hali kama hiyo, baada ya mda mfupi tu, shauku yetu kubwa inapo patwa na kutoku ridhika vilivyo, tutaanza ku rudi nyuma katika hali ile ile hafifu tuliko tokea. Tuna takiwa kujuwa jinsi gani tuta uwasha moto utakao anzisha kuguswa ndani ya kanisa letu na kutupa nguvu pamoja na shauku kuu, moto ambao uta endelea ku enea kwenye jamii yetu. Tuna ipata wapi nguvu na utashi, shauku kuu na uweza wa ku jitolea ; na ule musisimuko wa kuweza kuzi sukumia mbali nia za mwili hata kufikia kukitenda kile tunacho fahamu kuwa ndicho tunacho takiwa kukitenda ? Tuta fanya je ili ku uanzisha moto kanisani mwetu kiasi cha ku ueneza hadi kwenye jamii yetu na ku anzisha musisimko unao letwa na uamusho ?

Yesu alisema kuwa sisi ni chumvi ya dunia ; sisi ndio hiyo ladha inayo ileta chumvi katika chakula tunacho ki tolea waulimwengu. Chumvi yetu inatakiwa kupelekeya chakula kiwe na ladha nzuri kwa wale ambao bado hawaja okoka ili kwamba wahitaji kupewa zaidi na zaidi ya hiyo ; lakini ikiwa kama chumvi yetu tayari imepoteza ladha yake, basi haifai. Tuki muleta asiye amini ndani ya kanisa ambamo hamuna moto wowote uwakao, ambamo chumvi haina ladha, basi yule asiye amini ata geuka na kurudi kule aliko toka. Ikiwa wewe huna lolote uwezalo ku mutolea tofauti na yale ambayo dunia iliyo kuwa iki mpa huko nje, basi kwa nini wayatoe maisha yao kwa ajili ya dini yako hiyo iliyo kufa ?

Injili ni nguvu ya Mungu kwa ajili ya Wokovu. Siyo muundo wa mawazo wa aina fulani kuhusu Mungu, siyo mawazo ya ki elimu yanayo kuwa tu na mtazamo mpya kuhusu uhai na Umilele. Ikiwa ni yale tu ndio uliyo nayo kwa ajili ya kuyatolea wale waingiyao, basi wewe huna Injili hata kidogo ; nawe huna sasa lolote la kuzitolea zile nafsi ambazo bado zinayo njaa ya ku ipokea Kweli. Tunahitaji kuwa na ujumbe uliyo na nguvu pamoja na makanisa yaliyo na moto. Ujuzi wote wa kitheolojia ulio duniani hauwezi ku fanya lolote bila hii nguvu. Ila moto unapo waka kanisani, kila jambo hujitukiza bila kusukumwa. Musisimuko hutokea katika kila mushirika wa kundi kiasi kwamba hujikuta wakia anza ku kimbia na kuyafikia makundi yalio nje na ku waelezea wengine kuhusu yale yanayo tendeka kanisani mwao. Majirani wao waweza kui tazama kwenye nyuso zao wanao yaeleza na kuweza pia kuisikia kwa masikio yao, na musisimko huanza ku sambaa. Ni kama moto katika shamba la majani makavu, unapo shika tu, hauwezi ku zuiliwa.

Kinacho weza ku uanzisha moto ni moto mwengine pekee yake. Ili tuelewe kinacho hitajika ili kuwa na urahisi wa ku uanzisha moto wa uamusho kanisani, ina tubidi kwanza ku uanzisha moto ndani ya watu wanao hapo. Moto huwaka toka chini kuelekea juu wala si toka juu ku elekea chini. Moto ulio kwenye mimbari waweza tu kuleta (toba) udhibitisho wa hatia ya makosa. Moto una takiwa uanzie kwenye viti, na tokea hapo uta enea kwa sehemu zingine za makundi ya kanisa na halafu uta fikia kuya washa kanisa lote nzima.

Tuta wezaje kufikia hapo? Jibu lililo rahisi zaidi niwezalo kulitoa kwa ulizo hili ni kwamba, kila jambo katika

kumutumikia Bwana daima hutokana na mambo mawili: kusoma Neno na ku omba. Ila hayo mawili hu anzia kwanza kwa Neno sababu Neno la Mungu ni kisima cha Mamlaka. Ni Neno la Mungu ndilo lililo iumba dunia nzima na ni Neno la Mungu ndilo litakalo uleta uamusho ili, mwishoni, ni Mungu ndiye atakaye pokea utukufu, wala si mtu yeyote mwengine.

Neno hukupa ujuzi na kuelewa. Hukupa pia hekima katika kumcha Bwana pamoja na kujuwa ku yatambua mambo ya rohoni. Huku osha na uchafu na hukupa pia nguvu yak u ishinda dhambi. Hukupa mwanga ili uone na masikio ili uweze kusikia… na tena hukupa nguvu yaku omba.

Ikiwa kama uta omba, una takiwa uamini kile ambacho unacho kiombea, bila hivyo kuomba kwako hakuta kufaidia lolote sababu pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu (Hebrania 11:6). Na imani tuna ipata wapi ? Imani huja kwa ku sikia. (Warumi 10:17). Halafu, ni Neno la Mungu ndilo hukupa imani ili uweze ku omba.

Ila kusudi uuwashe moto, una hitaji kuwa na mafuta na pia kuwa na cheche la moto. Kila kimoja kikibaki chenyewe haki washi moto juu, ila ukiviweka pamoja, utakuwa ume anzisha moto.

Unapo chukuwa imani ile uliyo ipata kwa njia ya kulisoma neno la Mungu na kuipeleka hadi kwenye kiti cha Enzi cha Mungu kwa njia ya maombi, Neno pamoja na Roho watakubaliana (1 Yohana 5 :7) na hapo Roho wa Mungu ata shuka. Na hapo sasa chukuwa Yule yule roho uliye mpokea kwa njia ya maombi na kwenda naye tena katika kulisoma Neno nawe uta shuka ndani zaidi ya Neno. Na unapo kuwa

umeshuka ndani zaidi, masikio yako yatafikia ku funguliwa zaidi tena na hiyo ita iongeza imani yako. Halafu chukuwa ile imani iliyo ongezeka zaidi kwenye maombi nawe utakuta kuwa umepanda juu zaidi. Na unapo panda juu zaidi utapokea mengi zaidi toka kwa Roho. Sasa peleka Roho yule katika Neno mara tena, nawe utakuwa umeshuka ndani zaidi tena katika Neno. Na halafu panda juu zaidi kwenye Kiti cha Enzi kwa njia ya maombi, na halafu shuka chini zaidi tena katika Neno ; na juu zaidi katika maombi ; na chini zaidi katika Neno ; halafu fanya hivyo tena na tena hadi pale moto utakapo anza ku panda juu ndani ya moyo wako kiasi cha ku uwasha utu wako wote ! Hivyo ndivyo inavyo tendeka.

Na wakati ambao utu wako wote unapo washwa moto wa Mungu, uta wapa moto pia wengine, nao pia wata wapa moto watu wengine wengi… na moto uta enea kanisani mwenu kama moto ulio waka kwenye msitu mkavu. Na moto unapo waka kanisani mwenu lita ueneza huo moto hadi kwenye jamii. Na jamii yenu inapo waka moto, moto huo uta endelea ku waka hadi uamusho utapo shuka toka juu. Na hapo hakuna kiwezacho kuuzuiya. Na hayo yote huanzia kwa hatua ya kulisoma Neno la Mungu.

Arusi ya Kana

Katika habari ya arusi ya Kana huko Galilaya jinsi inavyo elezwa katika Yohana mlango wa pili, Mungu ame tuachia maagizo halisi kuhusu jinsi gani twaweza ku wezesha utendaji wa Roho kanisani. Yesu na wanafunzi wake waalikuwa wamealikwa kwenye karamu ya arusi ila waka pungukiwa na divai. Karamu ya arusi ni mfano wa Kanisa na divai ina wakilisha Roho wa Mtakatifu, na halafu karamu ya

arusi isiyo na divai ni kama kanisa lisilo kuwa na Roho wa Mungu ndani yake.

Maria, hali akimfahamu mwanawe, akawa ambia wanafunzi kwa sauti ya kuwapa amri, «chochote atakacho waambia, ***fanyeni hivyo*** !» (kume ongezwa uzito wa maneno). Mnataka uamusho ? Halafu chochote atakacho waambia, litendeni.

Na Yesu ali waambia wafanye nini ? Yesu ali waambia, « Jazeni vyombo maji.”

Siku zote maji huwakilisha Neno la Mungu. Tuna liona jambo hili katika ujumbe wa Waefeso 5:26 ambao una zungumza kuhusu ku oshwa kwa maji ya Neno la Mungu. Ndivyo tuonavyo pale ambapo Mwamba ulipo yatowa maji, katika Bakuli la Shaba katika hema, na pia mahali pengine pengi. Tena ni jambo la ku kumbukwa kuwa palikuwepo na vyombo sita vya mawe vya ku wekea maji hapo. Sita ni namba inayo muwakilisha mwanadamu, na vyombo hivi vina wawakilisha washiriki wa kanisa, vyombo vya udongo vilivyo finyangwa na Mfinyaji Mkuu.

Na halafu ni nini Yesu anacho tu alika kukifanya hapa ? Jazeni washirika wa kanisa hadi kiasi cha wao kufikia ku furika kwa maji ya Neno la Mungu – siyo kwa kiasi cha nusu-kipimo ao karibu na ku jaa, bali kujaza hadi juu kabisa ! Wakati ambao vyombo vinapo jazwa hadi juu kabisa, Roho na Neno vita kubaliana kufanyika kitu kimoja na hapo maji yatageuka kuwa divai !

Je kunaweza kuwepo na agizo lililo wazi kuliko hili ? Je

hatu elewi kuwa mamulaka yote hayatoke popote pale isipo kuwa kutokana moja kwa moja kwenye Neno la Mungu ? Na je hatu elewi kuwa wakati ambapo mamulaka yatokayo kwenye Neno yanapo bubujika kupitia maombi yata uwasha moto. Huo hautokani na vitabu, ma semina, video, kuimba au ku cheza, wala kushikilia wazo nzuri, ao kupitia mwanadamu muwakilishi mwengine yeyote – unatokana na Mungu pekee, Yeye awezaye ku iwekea dunia misingi yake, ku umba ulimwengu tu uonao na ule tusio uona, Yeye awezaye ku anzisha uhai, na halafu akaenda Msalabani kusudi aimwage damu yake ili ku komboa na ku takasa. Huwezi kufikia jambo hilo kwa njia nyingine sababu hakuna aina nyingine yoyote ya mamulaka yawezayo ku uanzisha uamusho ndani ya kanisa lako. Yesu mwenyewe ali sema kuwa pasipo Yeye, hamu wezi lolote… na Yeye ndiye Neno la Mungu.

Je unataka Moto wa uamusho kuwaka kanisani mwenu ? Basi lisome Neno la Mungu. Soma, soma, soma na soma tena hadi unapo fikia kulijaa hadi ku furika kwa mamulaka ya Neno la Mungu, na halafu nenda na umupelekeye divai yule aliye bwana wa karamu.

Moto juu ya Mlima

Neno la Mungu ni la mhimu kwa kila uamusho. Haijalishi ikiwa ni vigumu kiasi gani wewe kupata jinsi ya kusoma, hakuna jinsi ya kuleta visababu. Uamusho hauta fika bila Neno la Mungu kuchukuwa nafasi iliyo kubwa zaidi katika maisha yako na pia katika kanisa lenu. Lile dhihirisho alilo lionyesha Elia mbele ya Ahabu na mbele ya macho ya Waisraeli ni mfano ulio wazi sana kuhusu jambo hili.

Eliya alikuwa ame waita Mfalme Ahabu na Israeli wote

hadi huko juu ya Mlima Karmeli ili kuwa weka ma nabii wa Baali mbele ya mtiani. Mungu ambaye angali weza kujibu kwa moto alikuwa ndiye Mungu wa Israeli. Mchana kutwa, manabii wa Baali wali cheza waki izunguuka sadaka yao ya ku teketeza, waki paza sauti na kuji kata-kata wenyewe, ila Baali haku wajibu.

Halafu Elia aka yatengeneza madhabau na aka waomba wamuletee pipa ine za maji. Kisha aka omba zingine ine ziletwe. Na aka omba tena zingine pipa inne – zote kwa jumla zikiwa pipa 12 ! Sasa kumbuka, huu ulikuwa ni wakati wa ukame mkubwa na mito yote ya maji ilikuwa ime kauka. Na zaidi ya hii shida, kumbuka kuwa walikuwa huko juu ya mlima. Wangeli takiwa kushika njia hiyo ndefu kushuka mlima hadi kuji elekeza kwenye bahari na halafu kuja na hayo maji na kupanda hadi kilele kile cha mlima Karmeli. Ili wa bidi kutumia bidii ya pekee ili kuya fikisha maji hapo.

Kama na vile maji yana wakilisha Neno la Mungu, kile tunacho kiona hapa ni Nabii Elia aki ichovya dhabihu ndani ya Neno la Mungu. Haijalishi ikiwa ni vigumu kiasi gani wewe kupata jinsi ya wewe kuweza kuli soma Neno la Mungu. Ikiwa wewe una taka ku uona uamusho, kuna gharama inayo takiwa kulipwa. Mamulaka yatakayo uleta uamusho hayatoki ndani yako wewe, yatoka kwenye Neno la Mungu. Pasipo hilo Neno hapawezi kuwepo na mamulaka, hakuna undani wa mambo, hakuna hekima, hakuna imani wala uweza wowote wa ku weza ku chukuliana na utendaji wa Mungu.

Moto wa Mungu hauwezi ku shuka juu ya sadaka yako isipokuwa iwe ime chovywa kabisa ndani ya Neno la Mungu.

Ufunguo wa uamusho – Isaya 58

Muongozi mmoja mashuhuri ali wahi kuniomba kuutoa ujumbe kuhusu uamusho kwenye kikao kikuu cha waongozi wa makanisa huko Nigeria sababu, ingawa kama walikuwa wame funga na kuomba na kumu lilia Mungu alete uamusho, hakuna kilicho tendeka. Kulipaswa kuwepo na kasoro na wao walitaka kufahamu, ni nini hasa ilikuwa ndiyo sababu ya hali hii. Nimesha wahi kuwasikia mapasta wengi wakisema kuwa wamekwisha kujaribu kwa kila njia ili ku uanzisha udhihirisho wa utendaji wa Mungu makanisani kwao, ila hakuna kilicho onekana kuleta matukio yaliyo tarajiwa. Shida ni kwamba wao hulifanya bila ku utumia ufunguo wa jambo hilo.

Hebu kumbuka lile andiko nililo lizungumzia kuhusu Yoeli 1:11 na ambalo nime sema kuwa ndiyo makaripio makuu sana yaliyo juu ya Kanisa. Bwana anatueleza tu one aibu kwa kuwa sisi ndio watendakazi tunao takiwa kujihusisha na kuyavuna mavuno, na kumbe mavuno yanaharibikia shambani. Mungu Yeye anatu laumu kwa ajili ya nafsi ambazo bado hazija fikia ku okolewa. Laana zote, ukame, na njaa kuu tunavyo viona kwenye sura hiyo ya kwanza ya Yoeli na ambayo ime liangukia Kanisa ni matukio yanayotokana moja kwa moja na hali yetu sisi kukosa kuondoka tulipo na kwenda kuzitafuta nafsi za walio potea. Huo ndio ufunguo. Tuki sahihisha hali hii ya mambo, tunaweza kuanza kuona jinsi ngano, divai na mafuta vitakavyo fanywa upya. Pasipo ku sawazisha hali hii, kupaza kwetu sauti pamoja na machozi yetu yote havita leta chochote. Sio wasikiaji wa neno ndiyo husesabiwa haki bali watendaji.

Isaya 58 hutuonyesha picha iliyo wazi kuhusu kile

tunacho takiwa kuki fanya. Sura hii ya Biblia ina anza nayo amuri Mungu anayo mtolea nabii wake ya kwamba apaze sauti kwa nguvu kulielekea Kanisa na ku li eleza namuna gani kanisa lime ivunja sheria. Kanisa limeshindwa kutambua shida ina tokana na nini.

"Husema, Mbona tumefunga, lakini huoni ? Mbona tumejitaabisha nafsi zetu , lakini huangalii ? Fahamuni, siku ya kufunga kwenu mnatafuta anasa zenu wenyewe, na kuwalemea wote watendao kazi kwenu." (Isaya 58:3)

Kanisa huendelea ku nungunika eti wana endelea kuutafuta uso wa Mungu siku baada ya siku, waki zifurahia Njia zake, wame zishika amri zake nao wame funga na kuji taabisha nafsi zao… ila Mungu hawajibu. Ni kwa sababu gani Mungu haleti jibu ? Hii ndiyo aina ya kilio tunacho kisikia popote pale katika ulimwengu wa makanisa leo hii. Kwa nini makanisa yetu yana pungukiwa uhai kiasi hiki ? Tuna takiwa ku fanya nini ili tu ya amushe ? Kanisa lina fikiri kuwa wao wame fanya kila kitu wanacho takiwa kukifanya, mbona basi uamusho hautokei? Hebu lakini, ni jambo gani ndilo sababu ya nyinyi kufanya maombi na mafungo? Je ni kwa ajili yenu nyinyi ao kwa ajili ya wengine?

"Je siyo ndio maombi ya kifungo nilio ichagua, siyo ya namuna hii ? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walio onewa, na kwamba muvunje kila nira ?" (Isaya 58:6)

Dunia ipo katika giza na watu wamefungwa kwa minyororo nao wanalemewa chini ya mizigo mizito ya dhambi. Je ume jitahidi kuvi fungua vifungo vya uovu na

kuikata kamba ya hiyo mizigo mizito kwa njia ya kuwaleta wale watu waupokeye wokovu? Je ume waacha walio onewa kuwa huru na kuivunja nira ya dhambi kwa njia ya kuwapelekea injili walio kizani?

"je siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaletea maskini walio tupwa nje nyumbani mwako ? Umuonapo mtu aliye uchi , umuvike nguo; wala usijifiche mtu mwenye damu pamoja nawe?" Isaya 58:7

Je ume wapelekea walio njaa Mkate wa Uzima? Je umewaleta walio maskini wa Roho kuingia Nyumbani mwa Bwana? Je mulipo waona walio uchi muli wavika kwa vazi la haki? Ao nanyi muli waacha kando ya njia sawasawa na walivyo fanya ule kuhani pamoja na yule Mlawi katika ile habari ya Msamaria mwema ?

Ikiwa mutayafanya haya mambo ambayo Mungu anayo waomba ninyi ku yafanya, halafu hizi hapa ahadi zake :

«*ndipo nuru yako itakapo pambazuka kama asubui, na afya yako itatokea mara ; na haki yako itakutangulia ; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde*. » (Isaya 58 :8)

Roho wa Bwana atakuangazia, ata ku zunguka pande zote na kukulinda. Uta ingia katika baraza na haki yako itakutangulia; wale walio kando yako watajuwa kuwa wewe ni wa Bwana sababu ya ule uwepo wa Roho wa Mungu utakao kuwa juu yako.

"Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, naye atasema, mimi hapa. Kama ukiindoa nira; isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu." Isaya 59:9

Je una lilisikia neno hili vizuri? Halisemi kwamba labda, ao mara fulani… linasema ATAITIKA. Na unapopaza sauti ata sema, « Mimi hapa ».

Je munataka Mungu awape majibu ? Hayo ndiyo maongozi na ahadi anazo zitoa kwako. Hiyo hapo njia iliyo wazi ili kuiona heshima itokayo kwa Bwana. Heshima siyo daraka fulani ao cheo cha huduma ya kanisani – heshima, heshima ya kweli, ni wakati ule Bwana anapo sikia maombi yako na kuyajibu. Hiyo ndiyo heshima. Na heshima hii utaipata wakati unapo waonea huruma wale walio potea.

Na Neno la Mungu linaendelea kueleza …

« na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyo teswa ; ndipo nuru yako itakapo pambazuka gizani ; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. » Isaya 58 :10

Ukizilisha nafsi hizo zilizo na njaa kwa Neno la Mungu, ambao ni Mkate wa Uzima, isitoshe kuwa ataku inua na ku kuheshimu, ila pia utangaa kwa utukufu wa Mungu.

« *Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako ; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.* » (Isaya 58 :11)

Atakuongoza siku baada ya siku – Oh, uzuri gani kuongozwa na Roho wa Mungu siku baada ya siku – na Yeye ata iburudisha nafsi yako katika majira ya ukame na kuipa mifupa yako afya. Hata na katika wakati wa njaa ya kiroho, wewe utakuwa kama mti ulio pandwa kando ya Maji yalio Hai. Kwa nini ? Sababu ume jitolea ku shugulika na Kazi Kuu aliyo tuachia Yeye kuwatafuta walio potea.

Ila hapa tunapo fikia ndipo palipo sehemu nzuri zaidi ya ujumbe huu napo pana patikana ahadi iliyo fichwa kuhusu uamusho.

« Na watu wako watapajenga mahali palipo kuwa ukiwa ; utaiinua misingi ya vizazi vingi ; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka ; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia » Isaya 58 :12

Ikiwa utaubeba huu mzigo mabegani mwako, Mungu anasema kuwa wale walio toka ndani yako, uzao wako wa kiroho, utazijenga nafasi za mabomoko ya zamani, na kuiinua misingi ya vizazi vingi. Ona ahadi hizi nzuri kiasi hiki kwa ajili ya uamusho ! Kumbuka jinsi Nehemia alivyo utazama ule ukiwa wa mabomoko ya Yerusalemu, picha ya ukiwa wa kiroho ndani ya Kanisa ? Ni kwa ajili ya hali kama hii ndio uamusho huja, ili kuzijenga zile nafasi zilizo ukiwa na kulirudisha Kanisa kwa nafasi linapo stahili na kumuletea Mungu utukufu. Ikiwa uta ondoka na kuzivuta nafsi zilizo potea na kuwaonea huruma wale ambao bado hawaja okoka, wale unao waleta kwa Bwana wataijenga upya misingi ya zamani ilizo bomoka ndani ya Kanisa na ku isimamisha upya katika njia ambayo Kanisa linavyo takiwa lijengwe.

Na bado kuna heshima iliyo kuu zaidi – utaitwa

mtengenezaji wa njia zinazo takiwa kubaki ndani. Sioni heshima iliyo kuu zaidi kuliko kualikwa na Mungu ku yafanya upya mapito ili Kanisa liyafuate. Je katika ile milele, heshima itakuwa juu yako, ya kwamba wewe ni mmoja wa wale watengenezaji walio zijenga upya nafasi ndani ya Kanisa na ku usimamisha ukiwa na ku uleta moto wa uamusho kurudi tena Kanisani ? Ao utakuwa mmoja wa wale walio usikia mwito na ambao walishindwa ku simama na kuchukuwa uamuzi ku jibu kwa ule mwito ?

Hakuna kutoa visababu. Hakuna anaye jibu kwa nafasi ya mwengine . Hakuna uwezekano mwengine.

VI. HATUA ZA KI VITENDO

Zifuatazo hapa ni hatua zimoja za ki vitendo ili kutuweka katika njia ifaayo :

1. Lisome Neno kila siku

Hatua ya kwanza ya ki vitendo ni kujuwa jinsi ya ku jiweka mtu binafsi chini ya utii wa kuisoma Biblia. Chombo kilicho cha mhimu zaidi ambacho Mungu ame wahi kututolea ni Neno lake. Ni katika kulisoma Neno la Mungu ndipo tunapo ipata nguvu ili kuingia katika Uamusho. Uweza wetu hutokana na Neno la Mungu. Pasipo hilo, hatuwezi kuwa na uweza hata ule wa ku omba, haijalishi ni nini tunacho hitaji kuli ombea.

Mungu Yeye huku shugulikia ni kupitia Neno Lake kuhusiana na yale mambo utakayo kutana nayo siku ile. Siku yako ita pita kwa utulivu na kwa urahisi tokana jinsi ulivyo ianza siku

hiyo mpya katika Neno la Mungu. Wakati hufanyi hivyo, si kwamba tu uta tambua kuwa kila kitu chaonekana kukutia shaka na kigumu zaidi, ila pia uta tambua kuwa mda mwingi huwa umepotea bila kuzaa matunda.

Hapa kuna hatua za ki vitendo ili uweze mara moja kuanza kulisoma:

***Soma shahiri moja la Kitabu cha Mizali kila siku* :**

Ili kukusaidia ku juwa kile unacho weza ku anza kukisoma kila siku bila ku chelewa, soma sura moja ya Kitabu cha Mizali. Kuna siku 31 katika mwezi na pia Kitabu cha Mithali inazo sura 31. Uianze siku yako kwa kuisoma sura hiyo inayo ambatana na tarehe ya siku hiyo. Mizali ita kupa hekima na busara. Mithali hii takuwa iki kuzungumza hata na wakati unapo jikuta katika hali zilizo ngumu.

Katika Mithali, Bwana anasema kuwa wale wanao mtafuta mapema watamuona Yeye. Jitiishe mwenyewe chini ya utaratibu wa kuli tenda jambo hili liwe la nafasi ya kwanza mbele ya yote asubui uamukapo. Ukifikia kiwango cha kulifanya jambo hili kugeuka kuwa tabia iliyo jengeka, wewe binafsi uta tambua utofauti ndani yako.

Ingawavyo, la muhimu zaidi, wakati ambapo tayari Biblia ume ifungua, ni rahisi zaidi kumu uliza Bwana ni sehemu gani ya maandiko anataka uisome baadaye, na halafu endelea tu kusoma. Utakuwa tayari umesha shinda kipindi kilicho kigumu pale ulipo faulu kuketi na kukifungua kitabu cha Mithali. Wakati ambao umekwisha ku anza kusoma ni rahisi zaidi ku endelea. Hivi ndivyo tuwezavyo ku uanzisha moto ndani ya mioyo yetu.

Anzisha Vikundi vya Kusoma Biblia

Jambo hili laweza kweli kukupa furaha na papo hapo pia kuweza kuwatia nguvu nyinyi kwa nyinyi na kulitia Kanisa lote nguvu. Kuna njia mbili ya ku lifanya jambo hili :

Kuwa na jioni moja iliyo tengwa kwa ajili ya Mchungaji au mutumishi mwengine aliye katika uongozi ili atoe fundisho la Biblia. Hii ni aina ya uanafunzi kabisa kabisa. Munatakiwa kuwa na Muongozi ambaye anaye lifahamu vema Neno la Mungu na ambaye ana kiwango fulani cha mamlaka ili kwamba kikao kisije kikaharibika kwa kugeuka fasi ya mijadala au kisije kikageuka kuwa nafasi za washirika wasio imarika kutoa hoja zisizo faa kiasi cha ku anzisha ubishi usio na faida.

Wazo lingine linalo faa ni uundwaji wa makundi madogo madogo yanayo ingia na kukutana nyumba kwa nyumba ili ku changia chakula pamoja na Neno la Mungu. Kila mmoja aweza kuleta kitu kidogo kwa ajili ya chakula hicho cha ku changia. Hebu fikiria jinsi jambo kama hili linavyo toa nafasi nzuri ya kushiriki pamoja ! Inawapa nafasi nzuri ya kugawa mkate pamoja na ndugu zako na dada zako, kuchangia chakula kizuri na pia ku izunguuka meza na kukomboana katika ku isoma sura fulani ya Biblia. Punde si punde muta anza kutamani kuwa na «karamu» ya aina hii kila wiki. Mutapata ku uimarisha ujuzi wenu wa Neno, ku komaza ushikamano wa ushirika wenu kanisani, ku tiwa moyo toka kwa ndugu na dada na itawapa tena nafasi nzuri sana kuweza kuwaalika wengine waweze kujiunga nanyi. Kunazo nafsi ambazo bado hazija upokea wokovu ambazo nazo zaweza ku fika ili ku changia chakula na halafu zikaja, kwa njia hii, kufikia kiasi cha ku upokea wokovu. Walio bado

wakristo wachanga waweza ku jikuta kuwa wanaogelea katika ushirika wa jamaa jipya lenye upendo unao walea. Jambo hili lina fanya kazi kwa ngazi mbali-mbali.

2. Jitengee mwenyewe Saa ya Upekee kwa ajili ya maombi

Usemi huu wa zamani ni wa kweli «ikiwa huombi, basi wewe huta dumu ». Bila kujitengea na ku jitiisha mwenyewe kuwa na saa ya maombi unayo iheshimu, siku zote fikara zako zita yumbishwa yumbishwa au zita pelekwa na kuzuiwa kwa ajili ya kutenda mambo haya au yale. Kamwe shetani hataki upate wakati wa kujitolea kwa maombi !

Kama na nilivyo sema, Bwana anatualika kumutafuta mapema. Uki tazama jinsi walio tungulia walivyo ishi, utakuta kwamba waume ao wanawake mashujaa katika kazi ya Mungu walikuwa watu walio amuka mapema sana ili kuutafuta uso wa Mungu – kila mmoja wao alikuwa hivyo! Ukingojea mpaka utakapo pata mda ulio faa, utakuja kujikuta unaishi maisha yasiyo na maombi.

Jichaguliye mwenyewe wakati uwezao ku uweka kando. Unahitajika kuamuka na ku anza kuomba kwa wakati ule. Ukiona hii kuwa shida kwako, basi tafuta ndugu au dada ambaye mutakubaliana naye kuamuka na kukutana kanisani au mahali pengine pa upekee ili ku omba pamoja kila siku. Yawezekana hata kuwa muta pata sehemu fulani ya wengine wanao hitaji mapatano ya pamoja kwa ajili ya kujiwekea utaratibu wa pamoja na mwaweza ku anzisha kundi la maombi litakalo anza ku vivunja vibambazi vya zamani vya mambo ya mwili na udhaifu vilivyo yazuiya maombi yenu

hapo mbeleni. Sasa oneni mamulaka ya Mbingu yakianza kutenda kazi kwa ajili yenu kwa kiwango ambacho hata hamuku kitazamia. Huu ndio mwito ambao Mungu anao utoa kwa sauti kuu pale kwa sura ya 2 ya Unabii wa Yoeli, na hili ni jambo na muhimu sana ili kuwepo na uamusho wowote ule.

Wakati ambapo mwendo wa maombi tayari umeanza kusonga mbele, anzeni kutafuta jinsi ya kuunga uhusiano na waamini wengine katika makanisa mengine yaliyo katika mahali penu ili kuwa na vipindi vya ma saa 24 / siku 7 ao juma la mpangilio mzima wa maombi. Jambo hili litayafunga pamoja makanisa katika mahali penu na ita pelekea kuwepo kwa kambi la mapambano ili kuweza ku kabiliana na nguvu za giza. Fikiria huu jinsi ulivyo ushuhuda mkuu na wenye nguvu kiasi hiki! Si kwamba tu ita iweka nguvu jamii lote la mahali bali pia ita zima jitihada za shatani kutaka kuleta matengano katika Mwili wa Kristo. Nabii Yoeli alipo zungumuza kuhusu jeshi la Wakristo katika siku za mwisho husema kuwa hawata sukumana wao kwa wao wala hawata uvunja mstari wa kikosi chao.

Kuna kitu cha pekee kinacho mtikisa Mungu katika vipindi vya maombi ya saa 24 / ao yale ya siku 7. Sherti ayafurahie manukato ya uvumba utokanao na maombi ya wana Wake. Chochote kile kinacho lisababisha, naweza ku shuhudia kuwa jambo hili lina mugusa Yeye na hilo lita lianzisha gurudumu la uamusho kuanza kwenda mbele.

3. Ku iosha Miguu na Ushirika Mtakatifu

Kuna kitu kilicho na nguvu ya ajabu kitokanacho na

ushirika wa kanisa unao wafunga watu pamoja katika Roho. Njia moja kati zilizo bora zaidi ili kufikia jambo hili ni kwa njia ya mfano ule wa zamani wa kuiosha miguu. Yesu alituonyesha mfano wa kuiga katika Yohana sura hiyo ya 13 naye akatutolea amri yaku oshana miguu yetu sisi kwa sisi.

Biblia hutufundisha kuwa kila wakati tukiwepo shida kati yetu na dada fulani ao kati yetu na kaka fulani, tunatakiwa kumuendea yule mtu na ku jinyenyekeza wenyewe ili tu hakikishe tume tengeneza mambo kati yetu na huyo dada au kaka. Haijalishi ni nani aliye anza kumu kosea mwingine au ni nani aliye na hatiya. Dhambi ya majivuno ya kiroho haitofautishi. Ni katika njia hii ndio shetani huleta magawanyiko ndani ya kanisa na, anapo fanya hivyo, huharibu tumaini lolote la uamusho.

Umuendee yule mtu ambaye kulikuwepo shida kati yako na yeye, na kumuomba akusamehe ikiwa kama ume mutendeya au kumu eleza jambo mbaya, na halafu kuwaomba kuwa osha miguu yao. Jambo hili litayafanya majivuno ya moyo wako yapondeke kwa kiwango ambacho hakuna kitu kingine kiwezacho kukifikia. Ingawavyo, utakapo kuwa tayari umefanya hivyo, matangukano ao makosa yoyote ile itakuwa imetoweka kabisa na tena ushirika uta undwa kati yenu na hali hiyo ita funga mlango kwa lolote lile ambalo Shetani ali kusudia kuzusha.

Hebu fikiria sasa matengenezo ya aina hii iki tendeka kwa eneo ya kanisa. Chukua mda, likusanye kanisa lote nzima pamoja, kusanyeni beseni na taulo ya kupanguza maji na oshaneni miguu nyinyi kwa nyinyi. Muta jionea wenyewe kanisa nzima liki safika na uhuru utakao ingia kwenye mioyo

yenu utaiwezesha imani yenu ku komaa. Hii ita muachiya Roho wa Mungu ku bubujika.

Ushirika wa meza ya Bwana una fanya huduma iliyo kama na hiyo. Kumbuka kuwa hatutakiwi kuwa na ushirika wa Damu pekee yake ila ni ushirika pia wa Mwili – ambao ni ndugu na dada zako katika Kristo. Mbele yaku ingia ku jiunga na Ushirika wa Meza ya Bwana, chukueni wakati ili kila mmoja awe na mda wa kuenda kuonana na kila mtu waliye na matatizo naye ili kuwaomba msamaha. Mara tena ina omba kukumbuka kuwa, jambo hili halijalishi ni nani aliye mkosea mwenzake au ni nani aliye kosewa, ila lengo ni ku viponya vidonda vilivyo katika Mwili pamoja na ku ziba magawanyiko ambayo yule Mshitaki wa watakatifu amejaribu ku ya anzisha. Katika barua ya kwanza ya Paulo kwa Wakorinto kwenye sura ya 11 tuna onywa kuhusu kuishiriki Meza ya Ushirika hali tukiwa na zambi mioyoni mwetu ya kuwa hiyo ita tufanya kuwa wadhaifu na wagonjwa. Chuki na hasira kuwaelekea ndugu au dada zako ni dhambi hatari sana mbele ya macho ya Mungu sababu Yeye anasema kuwa ni ule upendo tunao udhihirisha kuelekea wengine ndio unao wafanya walio nje wamufahamu Mungu.

4. Waangalizi na Wakristo wachanga

Mchungaji hawezi na wala hapaswi kutazamiwa kuwa ndiye atakaye shugulikia mambo yote. Sherti kuwe na waangalizi ndani ya Nyumba ya Mungu ili waweze ku kesha kwa ajili ya kanisa, wanaume na wanawake wakomavu walio na uweza wa kufanya uchunguzi wa kiroho ili kutambua yaliyo mema na yaliyo mabaya. Ni ku hatarisha mambo yaliyo ya muhimu ikiwa kama jambo lolote lile litaruhusiwa

kujipenyeza bila kutambulika au bila ku pangiliwa. Majukumu yao yamo ndani kulitunza kanisa, kuya shugulikia mahitaji ya watu, na pia kukesha kwa ajili ya viwango vya mazaifu ya kuivuka mipaka viwezavyo ku ji penyeza kati ya kondoo, hasa kati ya walio bado vijana na walio wazaifu. Hakikisheni kuwa kuna watu walio wekwa ili kukesha juu ya afya njema ya kanisa.

Yesu amesema kuwa yatubidi kuzaa matunda mengi na tena yawe matunda ya kudumu. Ina faida gani ku zileta kwenye nuru nafsi zilizo kuwa zimepotea na kisha kuziacha ziangukie kando ya njia tokana na kwamba walio makanisani hawaku jali vya kutosha ili kuwa shugulikia? Tuna takiwa kuwa shugulikia walio wachanga katika Kristo sawa na jinsi tunavyo takiwa kuwa shugulikia wana wetu. Katika Matayo sura ya 28, sehemu ya mwisho ya Kazi Kuu aliyo tuachia Bwana ni kuwafundisha wale walio wapya katika imani jinsi yaku yashika yote Aliyo tufundisha sisi.

Kila nafsi ambayo ingali bado imefikia kuupokea wokovu inatakiwa iwe na mukristo mmoja aliye komaa na ambaye amepewa jukumu la kuwashugulikia ili kuwasaidia katika kuwaonyesha jinsi ya kumutumikia Mungu. Kazi yake huyo yatakiwa iwe, sawasawa na jinsi ilivyo kwa marafiki wa siku nyingi, kujitoa kulisoma Neno la Mungu pamoja, kuomba pamoja, kuondoka pamoja katika safari za kutoa ushuhuda na ku endelea kuwa waangalizi wao. Siyo shurti kwamba jukumu hili lipewe Mzee wa kanisa au Muinjilisti, ila mkristo yeyote yule ambaye ameupokea wokovu kikamilifu tokea mda fulani wa kutosha, kiasi kwamba ame elewa mambo ya kimusingi kuhusu jinsi yaku mtumikia Bwana. Ni moja kati ya baraka za pekee kupata nafsi ya kuwa Mkristo aliye komaa na

kuwa mwangalizi wa Mwamini mpya katika kukomaa kwake ndani ya Bwana.

Tusipo washugulikia waamini wapya, twawezaje ku tazamia kuwa Mungu ata zituma nafsi anazo ziona kuwa za bei ghali zije kwetu? Hicho ndicho kiini cha Uamusho – kuzitafuta nafsi zilizo potea na kuzitunza nafsi nyipya zinazo okoka.

5. Ku shuhudia na Mikutano ya Hadharani

Shabaa moja tu na kiini cha uamusho ni kuzivuta nafsi zilizo potea. Lengo la Uamusho siyo kuwapelekea waamini wajisikie vizuri, wala kuwa na ibada nzuri ajabu, ao siyo hata kuiona miujiza iki tendeka. Uamusho huja kwa ajili ya kuwatafuta walio potea. Ili kulitimiza jambo hili, una takiwa kugawa Ujumbe wa Injili pamoja na walio potea. Jambo hili silo la kutaka au kuto kutaka, wala silo jambo tuwezalo kulipuuzia. Ndicho hasa kiini cha habari Njema ya Wokovu. Mara kwa mara nime wahi kushugulika kulieleza jambo hili kwa upekee, huku niki itumia versi baada ya versi ndani ya Biblia ili ku onyesha kuwa, kufutana na ushuhuda wa Neno la Mungu, ikiwa kama wewe hauwaonei huruma wanao potea, yawezekana siku moja ujikute mbele ya Kiti cha Rehema cha Kristo bila kuipokea rehema ya kutosha ili kuvuka upande wa pili. Ikiwa una utaka uamusho, ni kwa ajili ya hilo ndiyo Mungu hu utuma uamusho. «Nipe nafsi zilizo potea au kama sivyo, kufa na'nife !»

Usi danganyike kufikiri kuwa ku shuhudia Neno la Mungu ni jambo ngumu. Usi jisumbue fikara zako kujiuliza wawezaje kuwa muhubiri, ku yafahamu sana maandiko, kuwa na majibu kwa kundi la maulizo yaliyo magumu kuyajibu, au

hata kumuzungumza mtu fulani kiasi cha kumuelewesha aukubali wokovu. Jambo unalo takiwa ku lifanya ni kuwaalika tu waje kanisani. Ndivyo ilivyo ! Wewe waalike tu waingie. Ni rahisi na vyepesi.

Sherti tuelewe kuwa inabidi kwanza tuwe na moto unao waka makanisani, kama sivyo hata zile nafsi zinazo ingia zikitokea nje, yawezekana zirudi kule nje mara tena. Nafsi hizi zina hitaji mambo makuu, siyo mambo yasiyo na uzito na yakuigiza (theatre). Ila moto unapo waka, itakuwa rahisi kuzivuta nafsi zilizo potea ikiwa tayari muna uchangamufu kuhusu yale yanayo tokea kanisani mwenu ! Je una lielewa hili? Si kwamba wao husikiliza tu maneno ambayo hu hubiriwa ao husoma vi karatasi vya ki Injili unayo wapa kuvisoma popote pale ila hasa huyafuata yale wanayo yaona ndani yako. Wakati unapo changamka, wao waweza kuiona kwa kuyatazama macho yako. Ni moyo wako ndio husema hasa na wao kuliko kitu chochote kile.

Hupaswi kutegemea vikaratasi vyenye michoro, na vyenye bei ghali vinavyo ubeba ujumbe wa Injili. Sisi tume zivuta nafsi 100 000 kwa Yesu hali tukiwa tu na muhuri ulio fanyizwa katika mpira ambao tuli utia chapa yake kwenye karatasi ambazo tuli zikata kwa vipande vidogo vidogo vyenye umbo ya miraba na ku vitolea watu kwenye mitaa. Je wewe huna pesa ? Na sisi pia hatukuwa nazo. Na kwa vyovyote, yawezekana uka jisikia vema zaidi kuondoka kuingia kazini hali ukiwa huna mambo yale ya ki umaridadi umaridadi ya ki dini. Unaweza uka fanye hivi : wewe chukua tu mhuri ulio fanyizwa kwa mpira na unao maandishi ya anwani ya kanisa lenu, mpangilio wa saa za ibada na pia namba ya simu. Chapa hesabu fulani ya vikaratasi vya

maaliko na halafu nenda mara moja mitaani. Kile utakacho kifanya ni ku vigawa tu hivyo vikartasi na ku endelea mbele. Kukiwepo na yule anaye ku simamisha ili kukuuliza swali, hapo ni sawa kabisa ! Na ikiwa hakuna anaye uliza, wewe endelea tu. Hivi vikartasi vya mialiko vita chukua pumzi ya uhai ya aina yake yenyewe na halafu Mungu mwenyewe Ata vitumia ku pelekea mioyo aliyo iweka njiani mwako ku jitambua. Kile unacho hitaji wewe kukifanya ni kuwaalika. Mungu atajishugulisha kuitenda sehemu ya kazi inayo muhusu Yeye … Ikiwa kama uta muachia Wakati.

Mikutano ya injili ya hadharani hutendeka vizuri zaidi barani Afrika kuliko jinsi ilivyo Marekani. Hata hivyo, tayari nyakati zimebadilika, na taratibu pia zimebadilika. Ikiwa kama watambua kuwa, kwa upande wako Mikutano ya hadharani inaendeka vizuri, basi wewe endelea kuipanga. Na ikiwa hai endeki vizuri, halafu fuata utaratibu tofauti. Kwa vyovyote hakikisha kuwa una mushuhudia Yesu. Hilo ndiyo tegemeo la maisha yako.

6. Uwe na maono.

Biblia inaeleza kuwa pasipo maono, watu hupotea. (Mithali 29:18). Una takiwa kuwa na maono ili kufahamu mahali unako elekea; na hiyo ita kusaidia kuvivuka vizuio ambavyo vita wekwa kwenye njia yako. Kuna takiwa kuwa na nia kuu moyoni mwako ili nia hii ikupe uweza wa ku utawala mwili wako na kama sivyo wewe huwezi kufanya hatua yoyote pamoja na Bwana. Yesu ana tualika kuji kana wenyewe, ku uchukuwa msalaba na ku Mufuata. Maono Yake Yeye yalielekea Msalaba na ule ushindi ulio patikana ili kuzitolea wokovu nafsi za wanadamu wote. Tuna wezaje

kumufuata Yeye ikiwa kama hatuna maono tuliyo ya weka mbele ya macho ili kujitolea kuya fikia? Tuna hitaji kuwa na maono na kama sivyo, unyonge wetu wenyewe uta utuharibu.

Maisha yetu yanazuilika mara kwa mara na mtazamo wa umbali tu wa yale macho yetu yawezayo kuyaona kama ndiyo yanayo tuzunguuka, bali ikiwa unataka Uamusho halisi wa Roho Mtakatifu, unatakiwa kuinua mtazamo wako kufika umbali zaidi ya yale macho yako yawezayo kuyaona kama ndiyo yanayo kuzunguuka wewe, kiasi cha ku ufikisha mtazamo wako hadi nafasi ambapo waweza kupaona kwa njia tu ya macho yako ya imani. Tenda kama mtu anaye iamini Biblia. Jipe moyo mkuu kiasi cha ku muamini Mungu, na umutazame sawasawa na jinsi lilivyo Neno Lake. Ni hapo tu ndipo njia itakuwa wazi mbele yako ili kukuongoza kwenye ushindi.

Katika Habakuki 2:2, Bwana ana alika ku ya andika maono, na ku yaweka wazi kwenye vibao, ili yaweze kusomeka kwa haraka, kwa urahisi. Uyaandike ! Wakati bado hayaja wekwa kwenye karatasi, bado hayaja kuwepo hata kidogo. Halafu uya bandike mahali ambapo itakapo weza kuwa ushuhuda mbele ya uso wako. Sasa una fahamu ni nafasi gani unapo taka ku fikia na una fahamu ni kwa sababu gani una taka kufikia nafasi hiyo. Sasa unacho chombo cha ku linganishia kitakacho ku ongoza kuelekea mwendo utakao ufuata ili kutimiza mwito wako katika Bwana.

Na ndivyo ilivyo kwa kanisa. Kanisa lako nina takiwa kuwa na maono yanayo fafanua shabaa kuu zaidi munayo taka ku itimiza. Muibandike kwenye kibambazi cha kanisa mahali

ambapo kila mmoja aweza ku iona. Sasa kanisa lenu lina lengo, lina muelekeo na lina nia kuu ambalo lime wekwa mbele yenu ili muweze ku fahamu yale munayo yafanya na kufahamu ni kwa sababu gani muna yafanya.

Gharama inayo hitajika ili ku upokea uamusho ni kubwa, na bila wewe kuwa na maono, hutapata kiu kikuu kitakacho kuwezesha kuilipa hiyo gharama.

VII. Jibu

Usiogope, Ee inchi, ufurahi na ku shangilia; kwa sababu Bwana amefanya maneno makubwa.

Musiogope, ninyi nyama za porini, kwa maana malisho ya jangwa yanatoa upesi, kwa maana mti unazaa matunda yake, mutini na muzabibu inatoa nguvu zao.

Furahini, basi ninyi watoto wa Sayuni, na furahini katika Bwana, Mungu wenu, kwa sababu anawapa ninyi mvua ya kwanza na mvua ya sasa kwa kipimo cha haki, na anafanyiza mvua ya kwanza na mvua ya sasa kuwaangukia ninyi, katika mwezi wa kwanza.

Na sakafu zitajaa na ngano; na mashinikizo yatafurika kwa mvinyo na mafuta.

Nami nitawarudishia ninyi miaka ya nzige ziliyo kula, na funza, na wadudu wage, na mapanzi, jeshi langu kubwa nililo tuma katikati yenu.

Na mutakula tele na kushiba, na mutasifu jina la Bwana, Mungu wenu aliyewatendea ninyi kwa mushangao, na watu wangu hawata fedheheshwa kamwe. Yoeli 2:21-26.

Kile Mungu anacho ki ahidi ni kwamba, sisi tuki utafuta uso wake kwa njia ya toba ya kweli, Yeye ata tusikia, ata tujibu na ata tuonyesha mambo yaliyo makuu tusiyo yajuwa. Nia aliyo nayo Mungu kutu takia tu upokee uamusho ni kuu kuliko jinsi sisi wenyewe hu utaka.

"Bwana akajibu aka waambia watu wake, tazameni nita waletea nafaka na divai, na mafuta, nanyi mutashiba kwa vitu hivyo" Yoeli 2: 19

Hukumu za Mungu zimeikatiza ngano, divai pia na mafuta Kanisani, ila hukumu za Mungu zimetolewa siyo tu kama malipizi kwa ajili ya dhambi, bali pia ni mwaliko ili watu waufikie utakatifu. Ana ahidi ku rudisha tena upya ngano, divai, na mafuta ambavyo vili ondolewa toka nyumba ya Mungu.

Kujitenga kwetu na Mungu kume tuzuiya sisi ku gundua siri na hazina iliyo lala ndani ya Maandiko na ambayo ni Roho pekee Yake ndiye awezaye ku tuifunulia. Hiyo ndiyo ngano iliyo kosa kushugulikiwa. Hebu fikiria utajiri tulio kosa ku ushugulikia kwa ajili ya kuto kutemebea kwetu katika ushirika wa ndani pamoja Naye! Ila sasa fikiria ile furaha kubwa yaku jionea ule mto wa hekima itakayo funuliwa kwetu wakati tunapo shuka na ku zamisha mafikara na moyo wetu ndani ya Neno lake Mungu. Imani huja kwa kusikia, na kile tunacho kisikia hutoka kwenye Neno la Mungu, ila masikio yetu yame zuiliwa kusikia kwa ajili ya kushikamana kwetu na

mambo ya ki dunia. Sasa masikio yetu yata sikia, na imani yetu ita vifikia viwango vipya na hiyo ita fungua milango kuhusu mambo yasiyo ya ukawaida ndani ya maisha yetu na pia ndani ya maisha ya wale tutakao wasiliana nao.

Divai ya Bwana ni huo uhusiano wa ndani pamoja Naye kwa njia ya maombi. Tume wahi kusoma kuhusu jinsi baba zetu walio tutangulia waliishi maisha yaku sihi katika kuomba kwa moyo wa machozi mda wa masaa, au hata mda wa usiku mzima pamoja na kuwa karibu na Mungu. Watu hawa hawaku pata uweza wa ku omba kiasi hiki sababu tu walikuwa na utashi wa nia kuu au kwa ajili ya uzoefu wa kujuwa kutii. Hilo ni jambo ambalo lina hitaji uweza toka Mungu. Roho wa Mungu aliwapa msukumo na nia yaku endelea hadi kuivuka mipaka ya ki mafikara ya kawaida na mipaka ya mwili na nyama hadi ku weza ku ingia kwenye maombi ya kiasi hiki. Kwa sehemu kubwa, musukumo huo ume toweka kanisani leo, ila Mungu ana sema kuwa ata uanzisha pia huo musukumo.

Mushtuko wa furaha ya kupenya hadi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu baada ya maombi ya nguvu na ku jitahidi hauwezi ku linganishwa na jambo lolote lile ambalo una weza kuli fikia kwa njia ya "kuwa na mazungumzo mafupi tu pamoja na Yesu". Mushtuko kama huo hukupa ushindi na furaha vinavyo tia nguvu mwendo wako wa ku tembea na Mungu. Sasa uta kuwa ukizipiga hatua ya shujaa ili ku vivunja vibambazi vyote vya adui. Ujasiri wako kuhusu jinsi maombi yanavyo jibiwa utakuwa hauna mipaka, na hata milima ita weza kutupwa baharini sababu sasa wewe si kwamba tu una mu amini Mungu, bali unayo ile imani ya Mungu, sababu wewe umekuwepo katika uwepo wake Yeye,

na ule uregevu wa hali ya ukawaida wa ki dunia sasa utakuwa ume ondolewa. Hapo una uweza wa ku lisimamisha juwa, wa ku izuiya mvua, wa ku ualika moto ushuke toka juu, na halafu ku ialika mvua ya mwisho ya uamusho ishuke toka juu.

Kume pita mda mrefu sana tangu ilipo anza kuonekana hali ya kupungukiwa mafuta yale ya upako wa Roho Mtakatifu ambayo Nabii Yoeli ali tabiri kuwa Mungu ata yarudisha tena. Mda ambao haya mafuta yame kosekana ni mrefu sana kiasi kwamba tumefikia hata kuto kutambua kile tunacho kipungukiwa. Matokeo ya hali hiyo ni kwamba, tuna jisikia kama tuna tosheka na mahubiri makavu, tuna tosheka na mafundisho ya ki elimu ya mwili na tuna tosheka na kanisa la mipangilio mipangilio. Tume fikia kiasi cha ku ji fariji kuwa elimu ya ki théolojia na ma shahada ya ki elimu inatosha. Leonardo Ravenhill aliwahi kusema kuwa ‘kuna wakati ambao tulikuwa na wahubiri ambao hawakuwa na vyeti vya shule ila kulikuwepo na moto tele kanisani, lakini sasa tunao wahubiri walio na vyeti tele vya ma shule basipo kuwa na moto. Ule upako ambao watu wame upungukiwa uta anza mara tena ku bubujika na pumzi mpya ya uhai ita ingia kanisani. Hebu fikiria ule mchangamko mkubwa wa kufurahiya ujumbe unao hubiriwa kiasi kwamba hamuta weza tena ku ngojea mipangilio ya kawaida ya ibada, kiasi cha ku anza hata kuwa na ibada za kanisani kila siku. Katika wakati kama huo, ibada za jumapili hazita tosheleza kiu cha watu. Nawe uta kuwa uki muelezea yeyote yule unaye kutana naye jinsi jambo hilo linavyo leta ku changamka. Na kwa mwisho, nafsi zilizo potea zita fikia hatua yaku upokea wokovu, sio tu kwa sababu ya mafundisho na imani yetu, ila kwa sababu wana uona moto uki meta-meta kwenye nyuso zetu. Huu

ndio uamusho, huu ndio ule uvuvio anao uzungumzia Isaya katika sura ile ya 32:15.

"*Furahi basi, enyi watoto wa Sayuni, na furahini katika Bwana, Mungu wenu; kwa kuwa Yeye anawapa ninyi mvua ya kwanza, kwa kipimo cha haki, na anafanyiza mvua ya kwanza na mvua ya sasa kuwaangukia ninyi, katika mwezi wa kwanza*" (Tafsiri ya Alliance Biblique Universelle - Swahili Congo)

Ni mvua ya kwanza gani hiyo ambayo Mungu ame tupatia kwa utulivu? Yaweza tu kuwa ni Pentekoste. Hiyo ilikuwa ni mvua ya kwanza. Kushuka kwa Roho Mtakatifu kulifanyika kwa nguvu sana kiasi kwamba kwa siku ile ya kwanza pekee yake, nafsi elfu tatu zili upokea wokovu, na Kanisa lilipokea nguvu yaku endelea mbele na ku itangaza Injili ulimwenguni. Na sasa Yeye ana lizungumzia jambo hilo kuwa lilikuwa tulivu? Ikiwa kama Pentekoste ilikuwa ndio mvua ya kwanza na ikiwa kama kwa mtazamo wa Mungu Yeye ame ihesabu kuwa ni tulivu, itakuwaje halafu wakati ambapo Mungu anapo imwaga kwa mara moja mvua ya kwanza na ile ya mwisho yote pamoja? Mimi nina amini kuwa kunako Siku nyingine ambayo ni Siku inayo lijia Kanisa la Mungu, nayo ni Siku ya 2 ya Pentecoste ambayo itakayo kuwa kubwa zaidi mno kuliko ile ya kwanza. Mutini pamoja na mudhabibu vita rudishiwa tena nguvu zao, na pale ambapo maji yale ya mudhabibu yatakapo bubujika yakipita ndani yetu kama matawi, tutazaa matunda mengi sana nasi hatuta kuwa tena wanawake wasio zaa, wamama tasa. Ni ile mvua itakayo yesha ndiyo itakayo pelekea tena uhai ku dhihirika jangwani. Na si mvua pekee yake, kwa kuwa Yeye atatuma mvua ile ya kwanza pamoja na mvua ya mwisho, Ndugu zangu, si kwamba itanyesha tu - bali ita bubujika!

Wakati Elia anapo mu elezea Ahabu kuwa “kuna sauti ya mvua nyingi”, sauti hiyo ni sauti ya kilio cha pamoja cha maombi ya watakatifu yaki paa hadi Mbinguni kumu lilia Mungu kwa ajili ya wokovu wa nafsi za wanao potea. Unapo sikia sauti ya namna hiyo, fahamu kuwa hivi karibuni mvua ina kuja. Uamusho unao kuja uta pulizwa na kiu kikuu kisicho cha kawaida na ambacho hakija wahi ku tokea watu waki muomba Mungu atu samehe, atufanye upya, pamoja na kiu cha ku zitafuta zile nafsi ambazo mbeleni tulikuwa tume zi puuzi. Itakuwa ni sauti yenye nguvu nyingi. Na jibu kwa ile sauti itakuwa ni mububujiko wa mvua ya pekee ambayo kamwe haija wahi kuonekana.

“na sakafu zitajaa ngano…” Yoeli 2:24

Ni sakafu gani hizo zitakazo jaa ngano ? Sakafu zilizo za ku puria ngano za makanisa yetu ! Nafsi za walio potea ndiyo mavuno ambayo Yesu ali yazungumzia alipo sema na wanafunzi wake. Mavuno hayo yanapaswa yaletwe kwenye sakafu zilizo za ku puria ngano ambako kutakuja kufanyika kutenganishwa kwa makapi na ngano. Hii ni jukumu la Kanisa kuzalisha zile mbegu halisi zilizo safi na zisizo kuwa na makapi ndani yake. Si kwamba sakafu zita jaa upande mmoja, au zita kuwa karibu kujaa – zita jaa kabisa kabisa na nafsi za watu wanao fika ili kumualika Yesu Kristo awe Mwokozi wa maisha yao. Madhabau yatajaa, viti vitajaa, na mara tena kuta kuwa nafasi inayo ngoja jinsi watu wanavyo mkimbilia Mungu, wakiwa na kiu kikuu cha kuupokea wokovu.

“na walio wanene watafurika kwa divai na mafuta.”

Si divai na mafuta mengi, ila divai na mafuta vinavyo furika! Roho wa Mungu ata furika kiasi cha ku tupelekea ku jisahau hali tukiwa katika kusifu. Ni watu wachache sana siku hizi wanao fahamu maana ya mtu kushukiwa na mububujiko wa Roho wa Mungu kiasi cha kujisahau mwenyewe. Huwezi kusimama, huwezi kufikiri, huwezi kunena jambo lolote isipokuwa kuyarudilia maneno ya kuzitangaza sifa za Mungu. Hapo una fikia kabisa kabisa maana ya ku lewa tokana na ujazo wa Roho. Hata hewa inayo kuzunguuka ita anza ku meta-meta tokana na utukufu wa Mungu.

« …*Nanyi muta kula chakula tele na kushiba, na kulihimidi jina la BWANA Mungu wenu, aliye watendeya mambo ya ajabu* »

Hebu jaribu ku elekeza ma fikara mbali sana uwezavyo, ila mambo ambayo Mungu Yeye atakayo yafanya bado yatakuwa ni *ya ajabu* mbele ya macho yako. Ata yafanya mambo ambayo kamwe hatuja wahi kuona au hata ku fikiria. Uamusho huu utakuwa na mambo ya miujiza inayo pita akili za ki dunia … na ya kushangaza.

Ata irudisha hiyo miaka iliyo liwa bila kuleta faida. Ata liinua bonde la mifupa iliyo mikavu sawa na isemavyo Ezekieli 37. Ata mu inua Bibiye Arusi amupendaye ili amu karibishe Kwake Yeye katika habari nzuri kuliko habari zote ambazo zime wahi kuelezwa kuhusu upendo wa arusi.

Kwa kumalizia

Mambo haya yote ambayo nime wazungumzia yana andikwa katika Neno la Mungu, nayo yata tendeka. Kumesha

wahi kutokea vipindi vikubwa vya uamusho katika miaka iliyo pita, ila uamusho mkubwa tunao ahidiwa katika unabii wa Yoeli na katika unabii wa Isaya hadi sasa una ngojewa ku timizwa. Nabii Yoeli ana rudilia mara sita mfululizo aki fafanua kuwa mda wa uamusho huu utakuwa ni mbele tu ya « Siku ya Bwana ».

Mpangilio huu wa wakati una eleweka wazi kwa kuwa hali ya kiroho itakuwa sawa sawa na jinsi ilivyo kuwa wakati wa kuja Kwake mara ya kwanza. Isaya 53 :2 ina eleza jinsi Yesu alivyo kuwa mzizi ulio mea toka ardhi iliyo kuwa kavu. Ulikuwa ni ukame wa kiroho ambao uli liweka taifa nzima la Israeli katika kiu kikubwa cha ku uona utendaji mpya toka kwa Bwana. Kulikuwepo na Sinagogi na pia Mafarisayo katika kila muji, bali habari tu ya uvumi kuhusu huyu nabii aliye jitokeza katika Israeli ili wapelekea maelfu ya wakulima wa kawaida tu, kuyatupa chini majembe yao na kushika njia ku elekea kwenye pwani ya mto Yordani ili wapate kulisikia maneno Yake. Ukame utakao tangulia kuja Kwake mara ya pili utakuwa mukubwa hata zaidi ya huo ulio kuwepo– hiyo ndiyo hali inayo tangulia uamusho. Mimi sijuwi kipindi hicho kita chukuwa mda gani, wala ikiwa ni wakati gani lita ripuka, ila ninalijua jambo moja nalo ni kwamba : sasa liko njiani.

Hata hivyo, halita ujilia ulimwengu wa makanisa kama na jinsi tuujuwavyo leo. Mungu ata yapatia makanisa mda fulani ili wabadilike toka hali waliomo sasa, ila makanisa hayata taka ku badilika. Kwa sababu gani wabadilike ? Kwanza hawaji sikie kuwa wana hitaji ku badilika. Ingekuwa vizuri ku pokea uamusho, lakini wao hawaji hisi kuwa wanacho kiuu kikubwa cha ku upokea kiasi cha kuwa tayari kujitolea kwa gharama yoyote ile itakayo hitajika. Jambo la ku sikitisha kuhusu hali ya kuikana imani ya kweli ni kwamba,

vazi la kujisikia vizuri na kutaka vitu vya urahisi-rahisi ambalo kanisa limejivika, ndilo hilo hilo vazi ambalo lina lizuia kanisa kuwa na macho ya kuona. Lime pungukiwa uweza wa ku elewa jinsi tayari limekufa, ingawa kama wote walio kando kando yake wanatambua wazi-wazi jinsi hali ilivyo.

Hali ya Kanisa la Laodikia ime simama ndani ya makanisa yetu leo. Nalo lina fikiri liko tajiri na kwamba limesha tajirika kwa kubarikiwa na Mungu, na kumbe limepigwa upofu unao tokana na hizo starehe zake na lina sindwa kuona kiasi gani tayari limesha poteza nafasi pale ambapo lilikuwa linasimama wakati ulio pita. Makanisa ambayo yali zaliwa katika moto wa uamusho yame geuka kuwa miungano ya ki jamii – yenye mipangilio yenye taratibu taratibu nyingi zisizo eleweka, yenye utajiri, na iliyo sawazishwa ki théolojia, huku waki jivunia uridhi ambao tayari wamesha upoteza. Majivuno yao hayata wapa njia ili watubu na ku geuka, na vinara vyao huendelea kufifia polepole sawa na njisi wanavyo endelea ku kaa katika kivuli kinacho wafunika pande zote huku waki jisikia kuwa wana tosheka. Ule moto ambao ulikuwa uki waka kwa joto kali siku zile za nyuma, umezimika na kugeuka makaa na majivu ambavyo sasa vimeleta uvuguvugu mtupu.

Mungu Yeye ata yainua mawe ili yaifanye kazi walio takiwa ku ifanya. Kwenye eneo la inchi kuna kizazi cha Gideoni wapya wanoa hitaji kuona kitu kipya wala sio tu "ukawaida wa kuingia na ku toka ». Hawa ndio watu ambao Mungu ata waita kutoka ndani ya mashirika yaliyo geuka kuwa mafu ili ku jiundia Jeshi alilo litabiri Yoeli na ambalo lita kuwa tayari kuingia katika pambano kati ya Mungu na Shetani kwa ajili ya ku shindania wokovu wa mioyo ya watu.

Uamusho huu mkubwa na wa mwisho uta kuja, bila

shaka. Uta kuja. Ulizo ni hili : je uta ukubali mwito ? Ikiwa huta ukubali, basi utajikuta ume simama kando na ku tazama kwa macho yako jinsi ambavyo moto wa Mungu utakavyo lishukia kanisa jirani ambalo lilikuwa tayari kuyatenda yale ambayo wewe hukukubali kuyatenda. Ni kwako kuchagua.

Wapendwa, sisi tuna ishi katika wakati ulio wa pekee tangu historia ilipo anza. Vita navyo viko njiani – vita vya kiroho, tena vya hatari – na ni kwa ajili ya wakati kama na huu ndiyo sababu tuna alikwa ku simama imara katika pambano hili la mwisho. Hiki ndicho kipindi cha mwisho cha muzozo ambao umekuwa uki endelea tangu ku umbwa kwa dunia. Mashujaa wata tambulishwa katika pambano hili la mwisho ambalo nuru ya ushindi wake ita ngaa milele na milele.

Sema sasa : « mimi ni hapa ! » ; simama ukabiliane na vipingamizi, na uamini yale asemayo Mungu kwa ajili ya kipindi cha Uamusho mkubwa kuliko vipindi vingine vyote ambavyo vili wahi kutokea.

Dalen Garris

Revival Fire Ministries
P.O. Box 822 Waxahachie, Tx 75168
(972) 938-8502

tafsiri toka Kiingereza imefanywa na
Michel M. Igunzi NDAHASHUBA
bamwiji@yahoo.fr
+243 990 660 793/ +243 853 318 053